# ILANI YA CHAMA CHA MAPINDUZI YA UCHAGUZI MKUU WA MWAKA 2025




*Kazi na Utu, Tunasonga Mbele*

# ILANI YA CHAMA CHA MAPINDUZI YA UCHAGUZI MKUU WA MWAKA 2025

*Kazi na Utu, Tunasonga Mbele*

Mei 2025



# Yaliyomo


Ujumbe wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi na Mgombea wa Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania v

**Sura ya Kwanza**

Dira, Misingi na Mafanikio ya CCM 1

**Sura ya Pili**

Ahadi na Maelekezo ya CCM (2025 – 2030) 10

2.1 Kuchochea Mapinduzi ya Uchumi wa Kisasa, Fungamanishi, Jumuishi na Shindani Uliojengwa Katika Msingi wa Kuongeza Thamani Rasilimali Zinazozalishwa Nchini 11

*2.1.1 Kuimarisha Ukuaji Jumuishi wa Uchumi 12*

*2.1.2 Kuimarisha Sekta Binafsi 13*

*2.1.3 Kuimarisha na Kukuza Sekta za Kimageuzi za Uzalishaji 13*

2.2 Kuongeza Fursa Za Ajira Kwa Vijana, Kuongeza Kipato Kwa Wananchi Na Kupunguza Umaskini 21

2.3 Kuboresha Maisha Ya Watu Na Ustawi Wa Jamii 23

*2.3.1 Kuinua Ubora wa Elimu Katika Ngazi Zote 23*

*2.3.2 Kuendelea Kuimarisha Huduma Bora za Afya 24*

*2.3.3 Kuimarisha Upatikanaji wa Maji kwa Wananchi Wote 25*

*2.3.4 Kuimarisha Familia na Ustawi wa Makundi Maalumu 26*

*2.3.5 Kuimarisha Hifadhi ya Jamii Kwa Wote 26*

*2.3.6 Kuboresha Makazi ya Wananchi na Kuendeleza Miji 27*

2.4 Kuimarisha Miundombinu ya Usafiri na Usafirishaji 28

2.4.1 Kuendelea Kupanua na Kuimarisha Ujenzi wa Barabara na Madaraja 28

2.4.2 Kuendelea na Ujenzi wa Miradi ya Reli 29

2.4.3 Kuimarisha Bandari 30

2.4.4 Vivuko na Meli 30

2.4.5 Kuendelea Kuimarisha Usafiri wa Anga 30

2.5. Kukuza Matumizi ya Sayansi na Teknolojia Katika Shughuli za Kiuchumi na Kijamii 31

2.6 Kudumisha Demokrasia na Utawala Bora 32

2.7 Kudumisha Muungano, Amani, Utulivu na Usalama na Diplomasia ya Kimataifa 33

2.8 Kudumisha Utamaduni wa Taifa na Kukuza Sanaa na Michezo 35

2.9 Kuongeza Kasi ya Maendeleo Vijijini 35

**Sura ya Tatu**

Mazingatio Maalumu ya Ilani Kuhusu Zanzibar 38

Ujumbe Wa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Zanzibar Na Mgombea Urais Wa Zanzibar 39

Ahadi Na Maelekezo ya CCM Kwa Upande wa Mapinduzi Zanzibar (2025 – 2030) 41

3.1 Kuchochea Mapinduzi ya Uchumi wa Kisasa na Endelevu 42

*3.1.1 Kuendelea Kuimarisha Hali ya Uchumi 42*

*3.1.2 Kuimarisha Usimamizi wa Sera za Uchumi, Fedha na Mapato 42*

*3.1.3 Kuimarisha Sekta Binafsi 42*

*3.1.4 Kuimarisha na Kukuza Maendeleo ya Sekta za Uzalishaji 43*

*3.1.5 Uchumi wa Buluu 48*

*3.1.6 Uhifadhi na Urithi wa Kale 52*

*3.1.7 Hifadhi ya Mazingira, Mabadiliko ya Tabianchi na Kukabiliana na Majanga 52*

3.2 Kuongeza Fursa za Ajira, Kipato na Kupunguza Umaskini 54

*3.2.1 Kuongeza Fursa za Ajira Kwa Vijana 54*

*3.2.2 Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi 55*

*3.2.3 Maendeleo ya Sayansi na Teknolojia 56*

*3.2.4 Uchumi wa Kidijitali na Uvumbuzi 57*

*3.2.5 Utafiti na Ubunifu 57*

3.3 Huduma za Habari na Mawasiliano 58

*3.3.1 Habari 58*

*3.3.2 Mawasiliano 58*

3.4 Kuboresha Maisha ya Watu na Ustawi wa Jamii 59

*3.4.1 Elimu 59*

*3.4.2 Afya 61*

*3.4.3 Maji 63*

*3.4.4 Ustawi wa Makundi Maalumuu 64*

*3.4.5 Hifadhi ya Jamii 65*

*3.4.6 Maendeleo ya Mipango Miji, Nyumba na Makazi 66*

*3.4.7 Utamaduni Sanaa na Michezo 66*

3.5 Kuimarisha Miundombinu ya Usafiri na Usafirishaji 68

*3.5.1 Miundombinu na Usafirishaji 68*

**Sura ya Nne**

Ufuatiliaji na Tathmini ya Utekelezaji wa Ilani 70

**Sura ya Tano**

Ubora, Uwezo na Uzoefu wa CCM Katika Kutoa Uongozi wa Nchi 74



# Ujumbe wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan

*Mwenyekiti wa CCM na Mgombea Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 2025*

## *Ndugu Wananchi Wenzangu,*

Ninawakaribisha katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025. Ilani hii ndiyo ahadi ya CCM kwa Watanzania juu ya hatua tutakazochukua katika miaka mitano ijayo ili kuendelea kukuza uchumi na kipato cha wananchi, kuinua hali za maisha ya Watanzania wote, kuimarisha ustawi wa jamii, kulinda amani, usalama na utulivu katika nchi, na kudumisha demokrasia na utawala bora.

Kwa niaba ya CCM na Serikali yake, ninawashukuru sana Watanzania wote kwa imani kubwa mliyotupatia kupitia Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 uliotupatia uhalali wa kuunda Serikali. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, na katika kipindi chote cha uongozi wake, CCM imeendelea kusimamia mageuzi makubwa ya kiuchumi, kisiasa, kijamii na kiutamaduni. Ninawaahidi kuwa tutaendelea na mageuzi haya kwa lengo la kutokomeza umaskini, kuinua hali za maisha ya Watanzania wote na kuinua ustawi wa jamii na Taifa letu. Ninaomba muendelee kuiamini CCM na kuwachagua wagombea wake wote kwa nafasi za Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Urais wa Zanzibar, Ubunge, Ujumbe wa Baraza la Wawakilishi na Udiwani.

***Ndugu Watanzania Wenzangu,*** Mtakumbuka kuwa tulipoanza utekelezaji wa Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 Taifa letu lilipata msiba mkubwa kufuatia kufariki kwa aliyekuwa Mwenyekiti wa CCM na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, aliyefariki dunia tarehe 17 Machi 2021. Hayati Dkt. Magufuli alikuwa kiongozi jasiri, imara na mwenye uthubutu, sifa ambazo zilimuwezesha kutekeleza na kufanikisha mambo makubwa ndani ya muda mfupi alioongoza. Tutamkumba daima Dkt. Magufuli kwa mchango wake alioutoa katika maendeleo ya nchi yetu. Ninakushukuruni Watanzania wote kwa jinsi mlivyoniombea na kusimama nami katika kipindi cha majonzi na mpito kufuatia msiba huo. Ninamshukuru Mungu kwa jinsi ambavyo ametuwezesha kutunza amani na umoja wa Taifa letu katika kipindi hicho cha mpito. Ninaendelea kuwaahidi kuwa tutaendelea kusimamia utekelezaji wa yote mema ambayo Dkt. Magufuli aliyaanzisha, na kufanya mengine mengi mapya.

***Ndugu Watanzania Wenzangu,*** Mwaka huu Taifa letu limetengeneza Dira mpya itakayoongoza mipango ya maendeleo ya nchi yetu kwa kipindi cha miaka 25 ijayo. CCM inaunga mkono matarajio yote yaliyoanishwa katika Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, na tunaahidi kuyatekeleza kikamilifu. Ilani hii imezingatia kikamilifu maudhui na vipaumbele vilivyobanishwa katika Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050. Kwa kipindi cha miaka mitano ijayo (2025-2030), CCM itaisimamia Serikali ili kuhakikisha kwamba tunaendelea kujenga uchumi imara, jumuishi na shindani; kulinda amani usalama na utulivu; na kuimarisha ustawi wa Watanzania kwa kuwawezesha kiuchumi na kufungua fursa zaidi za ajira na biashara.

Maudhui ya Ilani hii yamezingatia maoni na matarajio ya wanachama wa CCM, wananchi na wadau mbalimbali walioshiriki kutoa maoni yao kuhusu mambo ya kuzingatiwa katika Ilani ya Uchaguzi wa CCM ya Mwaka 2025. Kwa niaba ya CCM, ninawashukuru wote walioshiriki kutoa maoni yao, ikiwa ni pamoja na wanachama wa CCM, vijana, wanawake, Baraza la Wazee, vyuo vikuu, wasanii, Chama cha Muziki Tanzania, na Shirikisho la Asasi za Kiraia Tanzania.

Ninakishukuru kwa dhati chama changu CCM, kwa kuniteua kuwa Mgombea wa kiti cha Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kumteua Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kuwa mgombea wa kiti cha urais wa Zanzibar. Aidha, ninawashukuru wajumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM kwa kuridhia Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi kuwa mgombea mwenza. Ninaamini kwa pamoja tutaimarisha mafanikio tuliyoyapata na kufanya mengi mapya katika kufikia malengo tuliyojiwekea ya kuboresha maisha ya Watanzania kwa kuzingatia kauli mbiu yetu: ***Kazi na Utu, Tunasonga Mbele!***

***Ndugu Watanzania wenzangu,*** ninaomba kura zenu za NDIYO kwangu binafsi nikiwa Mgombea kwa nafasi ya Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa nafasi ya Urais wa Zanzibar, na wagombea wote wa CCM katika nafasi za ubunge, ujumbe wa Baraza la Wawakilishi, na udiwani.

***Kazi na Utu, Tunasonga Mbele!***

***Mungu Ibariki Afrika; Mungu Ibariki Tanzania***

***Kidumu Chama cha Mapinduzi***

**Dkt. Samia Suluhu Hassan**

**Mwenyekiti wa CCM na Mgombea Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mwaka 2025**

SURA

# 01.

# Dira, *Misingi* na Mafanikio ya *CCM.*

1. Mwaka huu wa 2025 **Chama Cha Mapinduzi (CCM)** kimetimiza miaka 48 tangu kuzaliwa kwake baada ya vyama vya TANU na ASP kuungana tarehe 05 Februari 1977. TANU ndicho chama kilichopigania na kuleta Uhuru wa Tanganyika tarehe 09 Desemba 1961, na ASP ndicho chama kilichopigania ukombozi wa Zanzibar na kuongoza Mapinduzi Matukufu ya tarehe 12 Januari, 1964. Aidha, katika kipindi hicho CCM kimefanikiwa kujenga Taifa lenye umoja na mshikamano bila kujali rangi, dini, kabila wala itikadi za kisiasa, sambamba na kulinda amani, utulivu na usalama wa nchi.

2. Kwa historia yake iliyotukuka, CCM ni chama chenye uongozi bora na uzoefu katika kuwaongoza na kuwatumikia wananchi kwa weledi na mafanikio makubwa. Aidha, CCM ndicho chama pekee nchini kinachobeba dhima na jukumu la kulinda misingi ya Taifa ambayo ni utu, umoja, haki, na usawa. Pia, CCM ni chama pekee kilichojipambanua katika kulinda Uhuru wa Taifa letu, Mapinduzi matukufu ya Zanzibar, na Muungano.

3. Dira ya CCM ni kuona ***Tanzania yenye ustawi kwa wote, nchi inayozingatia na kuheshimu utu, haki na usawa, na Taifa imara linalojitegemea.*** Katika miaka 48 ya uongozi wake, na katika Ilani zake saba za uchaguzi tangu mfumo wa vyama vingi uliporejeshwa nchini (1995 – 2025), CCM imekuwa ikiielekeza Serikali kutunga na kutekeleza sera, sheria na mikakati inatakayowezesha kufikia malengo ya dira hiyo. Katika kutekeleza maelekezo hayo, katika kipindi cha miaka mitano ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Mwaka 2020, mafanikio makubwa yamepatikana katika nyanja mbalimbali za kiuchumi, kijamii na kisiasa. Mafanikio hayo ni pamoja na:

***a. Kuimarisha uchumi na kuboresha maisha ya wananchi:***

i. Kuendelea kukua kwa uchumi kutoka asilimia 4.8 mwaka 2020 hadi asilimia 5.4 mwaka 2024, na hivyo kuhimili athari za janga la Ugonjwa wa UVIKO 19 na majanga mengine yaliyoikumba dunia;

ii. Kuendelea kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini ili kuchochea ukuaji wa uchumi. Kwa mfano, idadi ya miradi ya uwekezaji iliyosajiliwa na Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) imeongezeka kutoka miradi 207 yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 1,092.7 mwaka 2020 hadi miradi 901 yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 9,313 mwaka 2024, inayotarajiwa kuzalisha ajira 212,293;

iii. Kuongeza utoshelevu na usalama wa chakula nchini kutoka asilimia 114 mwaka 2020 hadi asilimia 128 mwaka 2024. Hali hii ilichangiwa na kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya chakula kutoka tani 18,665,217 mwaka 2020 hadi tani 22,804,316 mwaka 2024;

iv. Kuongezeka kwa tija katika uzalishaji wa mazao ya kilimo kwa kuchukua hatua zifuatazo:

   a. Kuongeza matumizi ya mbolea kwa wakulima nchini kutoka tani 586,604 mwaka 2020 hadi tani 1,213,729 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 107;

   b. Kuongeza eneo la kilimo cha umwagiliaji kutoka hekta 561,383 mwaka 2020 hadi hekta 983,466.06 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 82;

c. Kufufua Kampuni ya Mbolea Tanzania ili kuongeza upatikanaji endelevu wa mbolea kwa wananchi na kwa bei nafuu; na

d. Kuongeza upatikanaji wa mbegu bora kutoka tani 50,747 mwaka 2020 hadi tani 71,356 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 40.61.

v. Kupanda kwa bei ya mazao mbalimbali ambako kulichangia kuongezeka kwa kipato cha wakulima. Kwa mfano:

a. Bei ya korosho iliongezeka kutoka shilingi 2,707 kwa bei ya juu kwa kilo moja na shilingi 1,750 kwa bei ya chini mwaka 2020 hadi kufikia shilingi 4,195 kwa kilo moja kwa bei ya juu na shilingi 2,450 kwa bei ya chini mwaka 2024;

b. Bei ya kahawa aina ya Arabika iliongezeka kutoka shilingi 3,500 kwa bei ya juu kwa kilo moja na shilingi 2,500 kwa bei ya chini mwaka 2020 hadi shilingi 10,000 kwa kilo moja kwa bei ya juu na shilingi 7,500 kwa bei ya chini mwaka 2024; na

c. Bei ya pamba iliongezeka kutoka shilingi 1,200 kwa kilo moja mwaka 2020 hadi shilingi 1,700 kwa kilo moja mwaka 2024.

vi. Kuongezeka kwa mauzo ya nyama nje ya nchi kutoka tani 1,774 mwaka 2021 hadi tani 14,701 mwaka 2024 kulikochangiwa na kujengwa kwa minada ya kisasa 51 yenye thamani ya shilingi bilioni 17.5;

vii. Kuongezeka kwa uzalishaji wa umeme kutoka megawati 1,602.32 mwaka 2020 hadi megawati 3,077.96 mwaka 2024 kutokana na kukamilika kwa utekelezaji wa miradi mbalimbali, ikiwamo mradi wa kuzalisha umeme wa Julius Nyerere wenye uwezo wa kuzalisha Megawati 2,115 na kuingizwa kwenye gridi ya Taifa. Ongezeko hili limechochea ukuaji wa shughuli za kiuchumi kwa kuboresha upatikanaji wa nishati ya uhakika viwandani, kwenye biashara na shughuli nyingine za uzalishaji;

viii. Kuongezeka kwa idadi ya watalii wa nje ya nchi kutoka 620,867 mwaka 2020 hadi watalii 2,141,895 mwaka 2024 ili kuongeza mapato yatokanayo na shughuli za utalii kutoka dola za Marekani milioni 700 mwaka 2020 hadi bilioni 4 mwaka 2024;

ix. Kuongezeka kwa mchango wa sekta ya madini katika Pato la Taifa kutoka asilimia 6.8 mwaka 2020 hadi 9.0 mwaka 2024. Aidha, mauzo ya nje yanayotokana na madini yaliongezeka kutoka asilimia 53.8 mwaka 2021 hadi kufikia asilimia 56.2 mwaka 2023; na

x. Kuongezeka kwa mchango wa sekta ya viwanda katika Pato la Taifa kutoka asilimia 19.6 mwaka 2020 hadi asilimia 20.8 mwaka 2023. Aidha, jumla ya viwanda vipya 47,063 vimejengwa ambapo kati ya hivyo, vikubwa ni 365 na vya kati ni 1,360 na viwanda vidogo 45,338. Viwanda hivyo vimechangia kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa za viwandani nje ya nchi kutoka Dola za Marekani milioni 908.6 hadi kufikia Dola za Marekani milioni 1,363.3 mwaka 2024 kulikochangia kupunguza uhaba wa fedha za kigeni nchini.

***b. Kuwawezesha wananchi kuongeza kipato na kupunguza umaskini***

i. Kuendelea kutoa ruzuku kwa kaya masikini ili kuziwezesha kuongeza kipato cha kaya katika kuzisaidia kaya hizo kumudu gharama za mahitaji ya msingi. Katika kipindi cha mwaka 2020 hadi 2024 jumla ya Shilingi 961,496,032,731 zilitolewa kwa kaya masikini kupitia Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini (TASAF) na kunufaisha wananchi 5,202,655;

ii. Kutoa mikopo isiyo na riba kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu ambapo kiasi cha shilingi bilioni 240.9 zilitolewa kwa mchanganuo ufuatao: shilingi bilioni 96.3 kwa vijana 8,242, shilingi bilioni 45.1 kwa watu wenye ulemavu 1,196, na shilingi bilioni 99.5 kwa Wanawake. Aidha, mikopo yenye masharti nafuu ya shilingi 3,197,403,492 ilitolewa kwa vijana kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana;

iii. Kutengeneza ajira 8,084,203 katika sekta rasmi na isiyo rasmi. Kati ya ajira hizo, sekta isiyo rasmi ilizalisha ajira 7,037,024 na sekta rasmi ajira 1,047,179;

iv. Kutoa ruzuku ya mbolea ili kupunguza makali ya bei kwa wakulima. Katika kipindi cha mwaka 2020 hadi 2024 jumla ya Shilingi 693,631,308,093 zilitolewa kama ruzuku kwa wakulima 2,198,376 na hivyo kupunguza mzigo wa bei ya mbolea kwa wakulima hao; na

v. Kujenga masoko makubwa 33 na stendi 34 za mabasi. Hatua hii imechochea ukuaji wa biashara ndogondogo na za kati (SMEs).

***c. Kuboresha maisha ya watu na ustawi wa jamii***

- **Elimu**

i. Kuendelea kutoa elimu bila ada kuanzia elimu ya awali hadi kidato cha sita ambapo katika kipindi cha 2020 – 2024 jumla ya shilingi 1,308,900,040,500 zilitumika kwa ajili hiyo. Hatua hii imechangia kuleta mafanikio yafuatayo:

a. Kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi waliosajiliwa katika elimu ya awali kutoka 1,278,886 mwaka 2020 hadi 1,558,549 mwaka 2024, na darasa la kwanza kutoka 1,621,482 mwaka 2020 hadi 1,862,539 mwaka 2024;

b. Kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi waliojiunga na kidato cha kwanza kutoka 722,893 mwaka 2020 hadi 1,056,789 mwaka 2024, na kidato cha tano kutoka 78,434 hadi 127,008. Hatua hii imechochea kuongezeka kwa kiwango cha wanafunzi wanaojiunga na elimu ya sekondari kufikia asilimia 70; na

c. Kuwarejesha masomoni wanafunzi wa kike 10,864 katika shule za msingi na sekondari ili kuendelea na masomo yao.

ii. Kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi wanaojiunga elimu ya juu kutoka 233,734 mwaka 2020 hadi 334,854 mwaka 2024, ikiwa ni ongezeko la asilimia 43.3;

iii. Kuongezeka kwa kiwango cha ufaulu katika mitihani ya ngazi mbalimbali za elimu. Kwa mfano, kiwango cha ufaulu wa mitihani ya darasa la saba kilifikia asilimia 80.6 mwaka 2023, huku ufaulu wa kidato cha nne ukiongezeka kutoka asilimia 85.8 mwaka 2020 hadi 89.37 mwaka 2023, na kidato cha sita ukifikia asilimia 99.9 mwaka 2024;

iv. Kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi wanaopata mikopo ya elimu ya juu kutoka wanafunzi 142,170 mwaka 2020 hadi wanafunzi 245,799 mwaka 2024. Katika kipindi cha miaka minne iliyopita (2021/22 – 2024/25) jumla ya shilingi trilioni 2.760 zimetumika kuwapa mikopo wanafunzi wa elimu ya juu.

v. Kuanza kutoa mikopo kwa wanafunzi wa stashahada ambapo wanafunzi 9,959 wamenufaika katika fani za kipaumbele, ikiwamo afya, kilimo, usafirishaji, ualimu wa ufundi na ufundi stadi na uhandisi nishati na madini;

vi. Kuanzishwa kwa ***Samia Scholarship*** ambapo wanafunzi 3,696 wamenufaika hadi kufikia 2024; na

vii. Kuhuisha Sera ya Taifa ya Elimu na Mafunzo pamoja na mitaala yake ili kuwezesha kutoa wahitimu mahiri na wanaokidhi mahitaji ya soko la ajira.

- **Afya**

i. Kupungua kwa vifo vitokanavyo na uzazi na vifo vya watoto wachanga. Hivyo, vifo vya akina ma˚ma vitokanavyo na uzazi vilipungua kutoka 556 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2020 hadi kufikia vifo 104 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2024. Aidha, vifo vya watoto wachanga vilipungua kutoka 67 kwa kila vizazi hai 1,000 mwaka 2020 hadi kufikia vifo 43 kwa vizazi hai 1,000 kwa mwaka 2024;

ii. Kujenga vituo vipya 1,288 vya kutolea huduma za afya kama ifuatavyo:

» Zahanati 947;

» Vituo vya afya 277;

» Hospitali za Halmashauri 57;

» Hospitali za Mikoa 4; na

» Hospitali za Kanda 3.

iii. Kuimarika kwa hali ya upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi katika vituo vya kutolea huduma za afya vinavyomilikiwa na Serikali ambapo upatikanaji wa dawa muhimu za kipaumbele (aina 290) umefikia asilimia 89.3 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 75.6 mwaka 2020;

iv. Kuimarika kwa utoaji wa huduma za ubingwa na ubingwa bobezi nchini ikiwamo upasuaji wa moyo kwa njia za kisasa, upandikizaji wa uloto, huduma za upasuaji mgumu wa moyo bila kufungua kifua, upandikizaji figo, na upandikizaji wa vifaa vya usikivu kwa watoto. Hali hiyo imewawezesha wananchi wengi kupata huduma ndani ya nchi. Nchi yetu imeendelea kuwa chaguo la huduma za afya kwa wagonjwa kutoka nje ya nchi ambapo idadi ya wagonjwa kutoka nje imeongezeka kutoka 5,705 mwaka 2022 hadi kufikia 7,843 mwaka 2024.

- **Maji**

i. Kuongezeka kwa upatikanaji wa huduma ya maji kwa wananchi waishio vijijini kutoka asilimia 70.1 mwaka 2020 hadi asilimia 79.6 na kwa mijini kutoka asilimia 84 hadi asilimia 90 mwaka 2024. Ongezeko hilo limechangiwa na kukamilika kwa ujenzi wa miradi 1,633 ya usambazaji maji mijini na vijijini iliyowanufaisha jumla ya wananchi 12,547,526;

ii. Kukamilika kwa ujenzi wa vituo vya maji 107,819 na maunganisho katika kaya 196,160 vijijini;

- **Umeme**

i. Kuongezeka kwa idadi ya vijiji vilivyounganishwa na huduma ya umeme kutoka vijiji 8,587 mwaka 2020 hadi vijiji 12,318 sawa na asilimia 100. Aidha, vitongoji 33,657 kati ya 64,359 vimeunganishwa na umeme sawa na asilimia 52.3;

ii. Kuongezeka kwa kiwango cha kaya zilizounganishwa katika huduma ya umeme hadi kufikia asilimia 78 kutoka asilimia 39.9 mwaka 2020.

- **Mawasiliano**

i. Kuongezeka kwa wateja waliojisajili kwa ajili ya matumizi ya intaneti kutoka 28,470,506 mwaka 2020 hadi kufikia 48,028,227 kwa mwaka 2024, ikiwa ni sawa na asilimia 74 ya idadi ya watu nchini;

ii. Kuunganisha mifumo ya kutoa huduma (malipo, vibali na leseni) kwa njia za kielekroniki ili kurahisisha utoaji wa huduma kwa wananchi na kuziwezesha sekta binafsi kuwekeza, kuanzisha na kuendesha biashara;

iii. Kuongezeka kwa idadi ya wananchi wanaotumiahudumazamawasiliano ya simu kutoka 28,497,068 mwaka 2020 hadi 45,176,898 mwaka 2024 kulikochangiwa na kupungua kwa gharama za mawasiliano;

iv. Kuongezeka kwa kiwango cha upatikanaji wa mawasiliano ya simu za viganjani hadi kufikia asilimia 98 na upatikanaji wa intaneti yenye kasi umefikia asilimia 91 kutoka asilimia 45 mwaka 2020; na

v. Kuongezeka kwa kiwango cha upatikanaji wa huduma za mawasiliano na intaneti yenye kasi katika maeneo ya umma kutoka asilimia 23 mwaka 2020 hadi kufikia asilimia 57 mwaka 2024.

***d. Kuimarisha Miundombinu ya Kisasa ya Usafiri na Usafirishaji***

i. Kukamilika kwa ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) kipande cha Dar es Salaam hadi Makutupora (kilomita 722) na kuanza kutoa huduma ya usafiri wa abiria kutoka Dar es Salaam – Morogoro – Dodoma. Kukamilika kwa ujenzi na kuanza kutoa huduma kwa reli hiyo kumekuwa na manufaa makubwa kwa Taifa ikiwa ni pamoja na:

a. Kuzalisha ajira zaidi ya 30,176 za moja kwa moja na ajira zaidi ya 150,000 zisizo za moja kwa moja zilizotengeneza pato la shilingi bilioni 358.74;

b. Kutoa fursa kwa viwanda, wazabuni na wakandarasi ambapo hadi sasa jumla ya kampuni 2,460 zinashiriki katika mradi huu na kandarasi zenye thamani ya shilingi trilioni 3.69 zimetolewa;

c. Kuzalisha kipato ambapo hadi kufikia Desemba 2024 jumla ya abiria 1,200,000 walisafirishwa na kiasi cha shilingi bilioni 30 kupatikana; na

d. Kupungua kwa muda wa safari kati ya Dar es Salaam na Dodoma kutoka wastani wa saa kumi kwa basi hadi saa tatu na nusu kwa treni.

ii. Kuanza kwa ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) kwa vipande vya Mwanza – Isaka (km 341, umefikia 63.1%); Makutupora – Tabora (km 368, umefikia 14.44%); Tabora – Isaka (km 165, umefikia 6.8%); na Tabora – Kigoma (km 506, umefikia 7.3%).

iii. Kuongezeka kwa mtandao wa barabara za lami kutoka kilomita 13,235.1 mwaka 2020 hadi kilomita 15,366.36 mwaka 2024, na hivyo kuchangia kuimarisha kwa huduma za usafiri, biashara na shughuli za uzalishaji;

iv. Kuongezeka kwa mtandao wa barabara za vijijini kutoka kilomita 108,946.2 mwaka 2020 hadi kilomita 144,429.8 mwaka 2024;

v. Kujenga jumla ya madaraja makubwa 10 ikiwamo madaraja ya Tanzanite (Dar es Salaam), Wami (Pwani), Kiyegeya (Morogoro) na Kigongo – Busisi (Mwanza). Madaraja hayo yamerahisisha na kupunguza gharama za huduma ya usafiri kwa wananchi na usalama wao; na

vi. Kuendelea kuimarisha Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) ili kuboresha usafiri wa anga na kuongeza fahari kwa nchi. Hadi kufikia Oktoba 2024, jumla ya ndege 16 zimekwishanunuliwa na hivyo kuongeza safari za ndege za ndani, kikanda na kimataifa. Kuwapo kwa ndege hizi kumeongeza wigo wa utalii na idadi ya abiria wanaotumia usafiri wa anga kutoka milioni 2.4 mwaka 2020 hadi milioni 3.9 mwaka 2024.

### e. *Kudumisha Demokrasia na Utawala Bora*

Serikali ya CCM imeendelea kuweka mazingira mazuri ya kudumisha demokrasia na utawala bora, ikiwa ni msingi muhimu wa maendeleo ya Taifa. Katika kipindi cha utekelezaji wa Ilani ya 2020 ushiriki wa wananchi katika shughuli mbalimbali umeendelea kuimarika. Aidha, wadau wa demokrasia wameendelea kunufaika na haki zao za kidemokrasia ikiwamo uhuru wa kutoa maoni na kujumuika. Falsafa ya R4 imetoa msukumo wa kipekee katika kuimarisha upatikanaji wa haki za kidemokrasia na kijamii nchini. Kwa mfano, katika kipindi cha miaka mitano iliyopita:

i. Vyama vya siasa vimekuwa huru kutumia haki yao ya kufanya maandamano na mikutano ya hadhara bila vikwazo na kwa mujibu wa sheria za nchi;

ii. Kufanya mabadiliko ya sheria za uchaguzi na sheria ya vyama vya siasa kwa lengo la kuboresha mazingira ya uchaguzi katika mfumo wa vyama vingi. Kwa mfano, Bunge lilitunga Sheria ya Tume Huru ya Uchaguzi Na. 2 ya Mwaka 2024 ambayo, pamoja na mambo mengine:

   » imeondoa kifungu kilichokuwa kinaruhusu mgombea kupita bila kupingwa katika uchaguzi mkuu.

   » imeanzisha utaratibu mpya ya kuwapata mwenyekiti, makamu mwenyekiti na wajumbe wa Tume Huru ya Uchaguzi kwa njia ya usaili kabla ya kuteuliwa.

iii. Kuongezeka kwa ushiriki wa wanawake katika ngazi mbalimbali za maamuzi kutoka wanawake 2,390 mwaka 2020 hadi wanawake 2,660 mwaka 2024 ikiwamo Mawaziri na Naibu Mawaziri (10), Mabalozi (8), Wakuu wa Mikoa (7), Makatibu na Naibu Makatibu Wakuu (14), Makatibu Tawala Mikoa (12), Majaji wa Mahakama (48), Wakuu wa Wilaya (37), Wabunge (147), Makatibu Tawala wa Wilaya (51), Wakurugenzi wa Halmashauri (52), Madiwani (1,604), na Wakuu wa Idara kwenye Halmashauri (670); na

iv. Kuimarika kwa uhuru wa asasi za kiraia, vyombo vya habari, na mitandao ya kijamii.

***f. Kulinda na kuimarisha amani, utulivu na usalama wa nchi***

CCM inaamini kuwa amani, utulivu na usalama ni nguzo muhimu katika kuwawezesha wananchi kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo. Katika utekelezaji wa Ilani ya sita, Serikali ya CCM ilisimamia kikamilifu kuhakikisha kuwa Tanzania inaendelea kuwa nchi ya amani na yenye utulivu, na usalama wa nchi na raia wake unadumishwa. Aidha, Serikali ya CCM imeendelea kuimarisha diplomasia ya kikanda na kimataifa kama nyenzo muhimu ya kuimarisha ushirikiano na kutoa mchango katika jumuiya za kikanda na kimataifa pamoja na kunufaika na fursa za kiuchumi.

4. Kwa upande wa Zanzibar, mafanikio mahususi yaliyopatikana katika utekelezaji wa Ilani ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 ni kama ifuatavyo: -

a. **Amani, Umoja na Mshikamano**

Wazanzibari wote wameendelea kuwa wamoja na hivyo kuimarisha hali ya amani na umoja kwa wananchi na kupelekea ushiriki katika shughuli za kijamii, kiuchumi na kisiasa.

b. **Ajira kwa vijana**

Kufanikisha upatikanaji wa ajira 217,500 kupitia sekta rasmi na isiyo rasmi ndani na nje ya nchi, sawa na asilimia 72.5 ya lengo la shababa ya kutimiza ajira 300,000 ifikapo mwaka 2025.

c. **Miundombinu ya Kiuchumi**

Kuendelea na ujenzi wa barabara zenye urefu wa kilomita 100.9 (ambao umefikia asilimia 45), kilomita 275.9 (asilimia 60) Unguja na Pemba. Pia, huduma za bandari za Unguja na Pemba zimeimarika kutokana na uwekezaji uliofanywa katika Bandari ya Malindi, ujenzi bandari kavu Maruhubi na Fumba pamoja na uimarishaji wa bandari ya Mkoani Pemba. Aidha, huduma za usafiri wa anga zimeimarika kutokana na maboresho ya viwanja vya ndege vya Unguja na Pemba ikiwamo ujenzi wa jengo jipya la abiria katika Uwanja wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume.

d. **Elimu**

Kuimarisha mazingira ya elimu kuanzia ngazi ya msingi, sekondari na vyuo vikuu ambapo elimu inaendelea kutolewa bila malipo kuanzia ngazi ya awali hadi sekondari. Aidha, Serikali imekamilsha ujenzi wa skuli 41 za ghorofa zikiwamo 20 za msingi (Unguja 11 na Pemba 9) na skuli 21 za sekondari (Unguja 13 na Pemba 8). Uimarishaji huo, umechochea kiwango cha ufaulu wa wanafunzi kuongezeka kutoka asilimia 66.3 mwaka 2021 hadi 85.7 mwaka 2023 (kwa wanafunzi wa Kidato cha Nne) na kwa upande wa Kidato cha Sita ufaulu umeongezeka na kufikia asilimia 99.7 mwaka 2023 kutoka asilimia 98.8 mwaka 2021.

e. **Afya**

Kuimarisha miundombinu ya Afya kwa kukamilisha ujenzi wa hospitali 10 za kisasa za wilaya na hospitali moja ya rufaa ya mkoa. Sambamba na hilo, huduma za upatikanaji wa dawa na vifaa tiba imeimarika pamoja na kuimarishwa kwa huduma za mama na mtoto na huduma nyengine. Aidha, Mfuko wa Huduma ya Afya umeanza kutekelezwa kwa wafanyakazi wote wa Serikali. Kadhalika, wananchi wote wanaendelea kupata huduma za afya bila ya malipo.

f. **Maji**

Kutoa huduma ya maji safi na salama katika Shehia zote 388 za Unguja na Pemba na kufikia asilimia 88.22 ya uzalishaji wa maji. Upatikanaji wa huduma hiyo umechangiwa na ujenzi wa matenki 15 yenye uwezo wa kuhifadhi lita milioni 134 katika skimu saba. Aidha, kulikuwa na uchimbaji wa visima 64 vyenye uwezo wa kuzalisha wastani wa lita milioni 177 kwa saa pamoja na ulazaji wa bomba wa kilomita 466.9 kwa Unguja na Pemba.

g. **Nishati**

Kuunganisha huduma ya umeme katika vijiji 222 (Unguja 139 na Pemba 83) sawa na asilimia 72 ya vijiji 305. Aidha, gharama za uunganishaji huduma ya umeme zimepungua kutoka shilingi 464,000 hadi shilingi 200,000 kwa urefu usiozidi mita 30 na kutoka shilingi 1,700,000 hadi shilingi 200,000 kwa mteja mwenye nguzo moja.

h. **Uchumi wa Buluu**

*i.* ***Uvuvi;*** kukamilisha ujenzi wa kiwanda cha kusarifu dagaa katika eneo la Kama, Unguja; ujenzi wa diko na soko la kisasa la samaki katika eneo la Malindi sambamba na kuwekwa vifaa vya kisasa vya uhifadhi ya samaki ikiwamo mtambo wa kuzalisha vinoo vya barafu wenye uwezo wa kutoa tani 5 katika Soko la Malindi; na

*ii.* ***Kilimo cha mwani;*** kukamilisha ujenzi wa kiwanda cha kusarifu mwani katika eneo la Chamanangwe, Pemba. Uzalishaji wa zao hili umeongezeka kutoka tani 8,785 zenye thamani ya shilingi bilioni 5.387 kwa mwaka 2020 hadi kufikia tani 16,653 zenye thamani ya shilingi bilioni 16.5 kwa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 89.6. Mafanikio haya yametokana na juhudi za Serikali za kuwapatia wakulima wa mwani boti 1,027 na vifaa vya ukulima wa mwani.

i. **Utalii**

Kuongezeka kwa idadi ya watalii kutoka 260,644 mwaka 2020 hadi 638,498 mwaka 2023 sawa na asilimia 75 ya lengo la watalii 850,000. Mafanikio hayo yamechangiwa na kuimarika kwa miundombinu ya utalii, kuongeza idadi ya vivutio vya utalii na kutangaza vivutio vya utalii ndani na nje ya nchi kupitia filamu ya ***"Tanzania: The Royal Tour".***

j. **Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi**

Kutoa mikopo ya shilingi 32,663,903,234.56 kwa wananchi, miradi, vikundi vya ufugaji wa nyuki wa asali na makundi maalumu ambapo jumla ya wananchi 23,658 wamenufaika.

5. Pamoja na mafanikio makubwa yaliyopatikana katika kipindi cha utekelezaji wa Ilani ya CCM (2020 – 2025), na katika kipindi chote cha uongozi wa CCM, bado jitihada zinahitajika katika kuendelea kuchukua hatua mahsusi ili kufikia maelengo tuliojiwekea. Maeneo yanayohitaji kupewa kipaumbele na msisitizo ni pamoja na kuondoa umasikini wa kipato unaosababisha baadhi ya wananchi kushindwa kumudu kikamilifu gharama za maisha.

6. Katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2025 – 2030), CCM itahakikisha kwamba Serikali itakayoiunda inaongeza kasi ya ukuaji wa uchumi ili kuongeza kipato kwa wananchi walio wengi, na kuimarisha uwezo wa Serikali wa kujenga miundombinu na kutoa huduma za jamii kwa wananchi.

SURA

# 02.

# *Ahadi* Na *Maelekezo* ya CCM (2025 – 2030)

7. Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 ni ahadi na mkataba mama kati ya CCM na Serikali yake na wananchi katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2025 - 2030). CCM inaahidi kuendelea kuboresha uchumi, kuimarisha ustawi wa wananchi na kuhakikisha kuwa Serikali inayoiunda inaweka na kutekeleza mikakati thabiti ya kuinua hali za maisha za wananchi na kuboresha kipato chao.
8. Lengo kuu la Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 ni: ***Kukuza uchumi na kuimarisha ustawi wa wananchi***. Aidha, Ilani hii ni nyenzo ya CCM katika kuanza kutekeleza Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050. Katika kufikia lengo la Ilani hii, CCM itasimamia Serikali zake kutekeleza vipaumbele vinane vifuatavyo:
    i. *Kuchochea mapinduzi ya uchumi wa kisasa, fungamanishi, jumuishi na shindani uliojengwa katika msingi wa kuongeza thamani rasilimali zinazozalishwa nchini;*
    ii. *Kuongeza fursa za ajira kwa vijana, kuongeza kipato kwa wananchi na kupunguza umaskini;*
    iii. *Kuboresha maisha ya watu na ustawi wa jamii;*
    iv. *Kuendelea kuimarisha miundombinu ya usafiri na usafirishaji;*
    v. *Kukuza na kuimarisha matumizi ya sayansi na teknolojia katika shughuli za kiuchumi na kijamii;*
    vi. *Kudumisha demokrasia na utawala bora;*
    vii. *Kuendelea kudumisha amani, utulivu na usalama; na*
    viii. *Kudumisha utamaduni wa taifa, na kukuza sanaa na michezo.*
9. Kwa kuzingatia lengo na vipaumbele hivyo, Chama Cha Mapinduzi kinawaomba wananchi wote wa Tanzania kuendelea kukiunga mkono kwa kuwachagua kwa kura nyingi za NDIYO wagombea wake wa nafasi ya Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Urais wa Zanzibar, Ubunge, Ujumbe wa Baraza la Wawakilishi na Udiwani katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025.
10. CCM inawaahidi Watanzania kuwa itaendelea kuisimamia Serikali kutekeleza kikamilifu ahadi na maelekezo yaliyotolewa katika Ilani hii ili kufikia malengo yaliyowekwa. Aidha, CCM itahakikisha kuwa, katika utekelezaji wa Ilani hii, Serikali na vyombo vyake vyote inazingatia weledi, haki, na usawa, na kwamba rushwa na ubaguzi wa aina zote vinapigwa vita kama maadui wakubwa wa maendeleo ya jamii na Taifa.
11. Sehemu zinazofuata katika Sura hii zinaainisha kwa kina hatua na mikakati ambayo Serikali ya CCM itachukua katika kutekeleza vipaumbele nane vilivyobainishwa hapo juu.

## 2.1 Kuchochea Mapinduzi ya Uchumi wa Kisasa, Fungamanishi, Jumuishi na Shindani uliojengwa katika msingi wa kuongeza thamani rasilimali zinazozalishwa nchini

12. CCM inatambua umuhimu wa kujenga uchumi wa kisasa ambao ni fungamanishi, jumuishi, na shindani wenye wigo mpana na usiotegemea sekta moja katika kuchochea ukuaji wa uchumi na ustawi wa wananchi. Lengo

la sera za uchumi za CCM ni kukuza Pato la Taifa na kuhakikisha kuwa ukuaji huo unakuwa na athari chanya kwa wananchi kwa kuongeza pato la mtu mmoja mmoja, kupunguza umasikini na kuinua hali ya maisha ya Watanzania wote. Njia muhimu ya kufikia lengo hili ni kuimarisha programu za kuongeza thamani kwa rasilimali na mazao yanayozalishwa nchini ili kukuza ajira na kipato kwa wananchi. °°

13. Katika kuchochea mapinduzi ya uchumi wa kisasa, fungamanishi, jumuishi na shindani, maeneo yafuatayo yatazingatiwa:

    i. *Kuimarisha ukuaji jumuishi wa uchumi;*

    ii. *Kuimarisha sekta binafsi;*

    iii. *Kuimarisha na kukuza sekta za kimageuzi za uzalishaji;*

    iv. *Kuendelea kuimarisha upatikanaji wa umeme;*

    v. *Kuimarisha matumizi endelevu ya ardhi;*

    vi. *Kukuza utalii;*

    vii. *Kuimarisha mchango wa uchumi wa buluu katika kukuza Uchumi wa Taifa; na*

    viii. *Kuimarisha uhifadhi wa mazingira na ustahimilivu dhidi ya mabadiliko ya tabianchi.*

### *2.1.1 Kuimarisha Ukuaji Jumuishi wa Uchumi*

14. *Katika kuimarisha ukuaji jumuishi wa uchumi, katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2025-2030), CCM itaielekeza Serikali kuweka sera madhubuti za uchumi jumla, kibajeti, na kiutawala ili kuhakikisha Pato Halisi la Taifa linakua na pato la mtu mmoja moja linaongezeka kwa kutekeleza yafuatayo: -*

    i. Kuchochea shughuli za kiuchumi na kijamii ili kukuza uchumi kwa wastani usiopungua asilimia 7.0 kwa mwaka ili kuendelea kuongeza fursa za ajira na kipato;

    ii. Kutekeleza mikakati itakayoimarisha utulivu wa thamani ya sarafu yetu pamoja na utulivu wa uchumi kwa kuwa na mfumuko wa bei kwa kiwango kisichozidi tarakimu moja;

    iii. Kuhakikisha deni la Taifa linaendelea kuwa himilivu na mikopo inatumika kutekeleza miradi ya maendeleo yenye tija na inayochochea maendeleo ya kiuchumi. Mikopo yote itakayochukuliwa na Serikali itakuwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo inayochochea ukuaji wa uchumi na kuboresha ustawi wa wananchi. Hakuna mikopo itakayochukuliwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ya Serikali;

    iv. Kuimarisha akiba ya fedha za kigeni kwa kuchukua hatua zifuatazo:-

        a. Kuongeza akiba ya dhahabu kufikia angalau tani sita;

        b. kuongeza mauzo ya bidhaa nje ya nchi hususan bidhaa zilizoongezewa thamani;

        c. Kudhibiti matumizi ya fedha za kigeni katika matumizi ya kawaida; na

        d. Kuepuka kuagiza bidhaa kutoka nje ya nchi hususan zile ambazo zinaweza kuzalishwa nchini.

    v. Kuimarisha ukusanyaji wa kodi kufikia asilimia 15.6 ya Pato la Taifa ili kuongeza wigo wa upatikanaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya ujenzi na utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kugharimia huduma za kijamii na kiuchumi;

vi. Kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji hususan kwa wajasiriamali wanaofanya biashara ndogo na za kati;

vii. Kuimarisha matumizi ya sayansi na teknolojia na kupanua wigo wa matumizi ya TEHAMA katika kuchochea maendeleo ya sekta za kiuchumi na kijamii nchini;

viii. Kuimarisha huduma jumuishi za kifedha ili kuwezesha wananchi kutumia huduma hizo katika kuchochea ukuaji wa shughuli za kiuchumi na ustawi wa Taifa; na

ix. Kupunguza riba za mikopo na riba katika Taasisi za Fedha na Mifuko ya Uwezeshaji ili kutoa fursa kwa wananchi, hususan wenye vipato vya chini na kati ikiwa ni pamoja na vijana, wanawake na watu wenye ulemavu kupata mikopo ya muda mfupi na mrefu kwa riba ndogo.

### *2.1.2 Kuimarisha Sekta Binafsi*

15. ***CCM inatambua kuwa sekta binafsi ndio mhimili wa ujenzi wa uchumi imara. Hivyo, Serikali za CCM zitaendelea kuweka mazingira wezeshi ya kukuza sekta binafsi nchini. Katika kutekeleza lengo hilo CCM itaielekeza Serikali kuchukua hatua zifuatazo: -***

i. Kutunga na kutekeleza sera ya maendeleo ya sekta binafsi nchini;

ii. Kuendelea kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji kwa kuhuisha na kutekeleza kikamilifu Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara (MKUMBI); na

iii. Kuanzisha Mfuko Maalumu wa kuwezesha upatikanaji wa mitaji kwa wafanyabiashara wa Kitanzania, hususan wajasiriamali wanaofanya biashara ndogo ndogo na za kati, na kuwezesha uendelezaji wa kampuni changa.

### *2.1.3 Kuimarisha na Kukuza Sekta za Kimageuzi za Uzalishaji*

16. CCM inatambua umuhimu na mchango wa sekta za uzalishaji katika kukuza ajira, kuongeza mauzo nje ya nchi na kukuza akiba ya fedha za kigeni. Sekta hizi ni pamoja na kilimo, mifugo, viwanda, madini, nishati, ardhi, utalii, na uchumi wa buluu. Kutokana na umuhimu wake, CCM itaendelea kuweka kipaumbele kwa sekta za uzalishaji ili kuhakikisha zinaimarisha mchango wake katika ukuaji wa uchumi na ustawi wa wananchi. ***Katika kuendelea kuimarisha na kukuza sekta za kimageuzi zinazoweza kuchochea uzalishaji CCM itasimamia utekelezaji wa sera katika maeneo yafuatayo:***

#### 2.1.3.1 Kuongeza tija katika kilimo

17. Kwa kutambua nafasi ya kilimo katika usalama wa nchi, ujenzi wa uchumi na kukuza kipato cha wananchi, CCM itaendelea kusimamia mapinduzi katika sekta ya kilimo ili kukifanya kuwa cha kisasa na chenye tija. Lengo ni kuhakikisha nchi inajitosheleza kwa chakula, kuongeza kipato cha wakulima, kukuza Pato la Taifa, kuwa kichocheo cha kukua kwa viwanda, na kuongeza ajira. ***Katika miaka mitano ijayo, CCM inaweka shabaha ya kuona kuwa mchango wa sekta ya kilimo katika Pato la Taifa unaongezeka kutoka asilimia 4.6 mwaka 2025 hadi asilimia 10 ifikapo mwaka 2030 kwa kuchukua hatua zifuatazo:***

i. Kuimarisha upatikanaji wa mbegu bora na kwa bei nafuu;

ii. Kuendelea kutoa ruzuku ya pembejeo mbalimbali kwa wakulima ili kupunguza gharama za uzalishaji na kuongeza tija;

iii. Kuboresha na kuongeza miundombinu ya umwagiliaji itakayoongeza eneo la kilimo cha umwagiliaji kutoka hekta 983,466.06 mwaka 2024 hadi kufikia hekta 5,000,000 mwaka 2030 ili kupunguza utegemezi wa mvua kwenye kilimo;

iv. Kuimarisha upatikanaji wa zana za kisasa kwa kuanzisha vituo vya kukodisha zana za kilimo, ikiwamo kununua na kusambaza matrekta 10,000;

v. Kupitia upya mifumo ya uuzaji wa mazao ya kilimo, mifugo, na misitu kwa lengo la kunufaisha wakulima, kurahisisha na kuwezesha mazingira ya kufanya biashara vijijini;

vi. Kuwapatia wakulima teknolojia za kisasa za uhifadhi wa chakula, na kuanzisha na kuendeleza kilimo cha mazao yanayohimili ukame na mabadiliko ya tabianchi ili kuimarisha uhifadhi na usalama wa chakula;

vii. Kuimarisha mazingira wezeshi na kuweka mfumo utakaowezesha mauzo ya mazao ya wakulima kwa bei ya sokoni na kwa utaratibu wa kulinda bei za mazao hayo kwa wakulima ili kumnufaisha zaidi mkulima;

viii. Kuanzisha na kuendeleza mashamba makubwa ya pamoja ya kilimo cha kisasa cha biashara kwa mazao ya kimkakati na yenye mahitaji makubwa ili kuongeza kipato kwa Watanzania na nchi kwa ujumla;

ix. Kuhamasisha na kuendeleza kilimo hai ili kuongeza uzalishaji na kipato kwa wakulima; na

x. Kuanzisha mfuko wa dhamana kupitia Mfuko wa Pembejeo za Kilimo, Benki ya Maendeleo ya Kilimo na Benki ya Ushirika ili kuwawezesha wakulima na wananchi wengine wanaojishughulisha na uongezaji wa thamani kwa mazao ya kilimo, mifugo na samaki kukopa katika taasisi za fedha kwa riba ndogo.

xi. Kuimarisha vyama vya ushirika kimuundo, kimenimejenti na kirasilimali kama vyombo muhimu vya sauti vya wakulima, wafugaji na wavuvi

#### 2.1.3.2 Kuimarisha Ufugaji wa Kisasa

18. Chama kinatambua kuwa mifugo ni miongoni mwa sekta muhimu katika ukuaji wa uchumi na uzalishaji wa ajira kwa vijana na kuongeza kipato kwa wafugaji. Katika kipindi cha utekelezaji wa Ilani hii, Chama kitaendelea kutoa kipaumbele kwa sekta hiyo ili kuiimarisha na hivyo kuleta mabadiliko makubwa kwa kuhamasisha na kuwezesha uwekezaji katika ufugaji wa kisasa na wa kibiashara pamoja na kuchakata bidhaa za mifugo ili kuongeza thamani ya mazao hayo. ***Lengo ni kuongeza mchango wa sekta ya mifugo katika Uchumi wa Taifa angalau ufikie asilimia 5 kwa mwaka ifikapo 2030 kwa kuchukua hatua zifuatazo: -***

i. Kutenga, kupima na kumilikisha kwa wafugaji maeneo ya shughuli za ufugaji kutoka hekta 3,466,111.43 hadi hekta 6,000,000 pamoja na kuyaboresha maeneo hayo kwa kuyapatia huduma muhimu zikiwamo maji, majosho, malisho na huduma za ugani;

ii. Kupitia upya mfumo wa umiliki na uendeshaji wa ranchi za umma ili kushirikisha sekta binafsi kwa lengo la kuzifanya zijiendeshe kisasa, kibiashara na kupata tija,;

iii. Kuimarisha huduma za ugani, kinga na tiba ya mifugo ili kuwezesha wafugaji kukabiliana na magonjwa na vifo vya mifugo na hivyo kuongeza uzalishaji na kipato;

iv. Kukarabati na kuongeza mabwawa/ malambo ya maji ya mifugo kutoka 1,397 hadi 1,842, na visima virefu kutoka 124 hadi 225;

v. Kuongeza mauzo ya mazao ya mifugo nje ya nchi kutoka tani 14,000 mwaka 2025 hadi tani 50,000 mwaka 2030;

vi. Kurahisisha upatikanaji wa mitaji, mbegu na maeneo ya malisho ili kuwawezesha wananchi kushiriki kikamilifu katika shughuli za ufugaji;

vii. Kuhamasisha na kuwezesha ujenzi wa machinjio ya kisasa pamoja na masoko ya mifugo nchini kwa ajili ya kuongeza thamani na biashara ya mifugo na mazao yake; na

viii. Kuimarisha utoaji wa elimu ya ufugaji wa kisasa inayozingatia tija ya uzalishaji.

### 2.1.3.3 Kuimarisha Ujenzi wa Uchumi wa Viwanda na Kukuza Biashara

19. Sekta ya viwanda ni muhimu katika kukuza uchumi wa nchi kwa kuzalisha bidhaa ili kujitosheleza na mahitaji na kupunguza kiwango cha uagizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi. Vilevile, sekta hii ni muhimu katika kukuza ajira na kuongeza thamani ya malighafi na bidhaa hususan zinazozalishwa ndani ya nchi na hivyo kuongeza mapato na fedha za kigeni. Kwa kutambua umuhimu huo, kipaumbele kitawekwa katika kuweka mazingira wezeshi kwa sekta binafsi ili kuwekeza katika uzalishaji viwandani na hivyo kuongeza mchango wa sekta hiyo katika uchumi. ***Katika kuimarisha sekta ya uzalishaji viwandani, CCM itahakikisha Serikali inatunga na kutekeleza mikakati ya kuhakikisha sekta hii inakua kwa angalau wastani wa asilimia 9 kwa mwaka kwa kuchukua hatua zifuatazo:***

i. Kutunga na kutekeleza sera na sheria itakayozuia kusafirisha nje ya nchi bidhaa zitokanazo na rasilimali za asili bila kuongezewa thamani nchini;

ii. Kubuni na kutekeleza mkakati wa kuanzisha na kuendeleza viwanda vya kimkakati ikiwamo dawa, chuma, mbolea, ngano, sukari, mafuta ya kula, na mavazi kwa lengo la kujitosheleza kwa mahitaji ya msingi;

iii. Kuweka mazingira maalumu ya kuvutia ujenzi wa viwanda vidogo vijijini kwa lengo la kufanya ongezeko la awali la thamani *(primary processing)* katika sekta za kimkakati zikiwamo kilimo, mifugo, uvuvi, na misitu ili kuongeza fursa za ajira na kupunguza upotevu wa mazao;

iv. Kuimarisha miundombinu ya masoko ikijumuisha vituo vya ukusanyaji na uongezaji thamani;

v. Kuanzisha na kuendeleza kongani za viwanda na Maeneo Maalumu ya Kiuchumi (SEZs), pamoja na maeneo huru ya biashara; na

vi. Kuweka mazingira malum ya kuvutia uwekezaji katika ujenzi wa viwanda vya uzalishaji wa bidhaa mahususi kwa mahitaji ya nchi ikiwamo:

a. Kiwanda cha kuzalisha chakula cha mifugo;

b. Kiwanda cha kuzalisha mbolea kwa kutumia gesi; na

c. Kiwanda cha kuchakata samaki.

#### 2.1.3.4 Kuendelea Kuikuza Sekta ya Madini Kama Hazina ya Taifa

20. CCM inatambua kuwa sekta ya madini ina nafasi ya kipekee katika kuchangia ukuaji wa Pato la Taifa, upatikanaji wa fedha za kigeni, na ukuaji wa uchumi kwa ujumla. Katika kuhakikisha sekta hiyo inaongeza mchango katika ukuaji wa uchumi, kipaumbele kitawekwa katika kuongeza thamani ya madini nchini kabla ya kusafirishwa nje, kuwezesha uchimbaji wa madini wenye tija, uendelezaji wa wachimbaji wadogo ili kuwawezesha kunufaika na ushiriki wao katika shughuli za madini, na kuimarisha usimamizi wa mapato yatokanayo na biashara ya madini. ***Lengo ni kuona sekta ya madini inakua kwa wastani wa angalau asilimia 7 kwa mwaka. Ili kufikia azma hiyo Chama kitaielekeza Serikali kutekeleza yafuatayo:***

i. Kutenga maeneo maalumu ya wachimbaji wadogo wa madini, kuwapatia leseni na kuwaendeleza;

ii. Kufanya utafiti zaidi wa maeneo yenye madini na kuongeza eneo lililopimwa na kufanyiwa utafiti kutoka asilimia 16 ya sasa hadi kufikia asilimia angalau 50 ifikapo mwaka 2030 ili kuhamasisha uwekezaji hususan wa madini muhimu na ya kimkakati;

iii. Kutokana na umuhimu na nafasi yake katika kukuza uchumi wa nchi na wananchi kwa ujumla, Serikali itaweka mazingira maalumu ya kisera na kisheria yatakayohakikisha kuwa madini adimu na ya kimkakati *(strategic mineral resources and rare earth elements)* yanachimbwa na Watanzania na/au Watanzania kwa ubia na wawekezaji kutoka nje. Aidha, Serikali itaweka sera, sheria na kanuni zitakazohakikisha kuwa madini haya hayasafirishwi nje bila kuongezewa thamani nchini.

iv. Kupunguza utoroshaji wa madini nchini kwa asilimia 75 kwa kuanzisha na kuimarisha vituo vya ukaguzi na usafirishaji wa madini katika mikoa yenye madini kama Geita, Mwanza, Shinyanga, Morogoro na Manyara;

v. Kuweka utaratibu wa kisera na kisheria kuhakikisha kuwa madini yote yanayozalishwa nchini yanaongezewa thamani kabla ya kusafirishwa nje ya nchi;

vi. Kutenga maeneo maalumu ya wachimbaji wadogo wa madini, kuwapatia leseni na kuwaendeleza; na

vii. Kuifanya Tanzania kuwa kituo cha uuzaji wa madini katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati pamoja na kuimarisha masoko ya madini na vito ikiwamo Tanzanite kwa kujenga jengo la Tanzanite Exchange Centre (TEC) katika eneo la Mirerani, Wilaya ya Simanjiro.

#### 2.1.3.5 Kuendelea Kuimarisha Upatikanaji wa Umeme

21. CCM inatambua kuwa umeme ni kichocheo muhimu cha ukuaji wa shughuli za maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Aidha, upatikanaji wa umeme wa uhakika kwa wananchi una mchango na nafasi ya pekee ya kupunguza umaskini. Kwa kuzingatia haya, katika kipindi cha mwaka 2025 - 2030, CCM itaendelea kuisimamia Serikali kuongeza kasi ya uzalishaji wa umeme na kuimarisha usambazaji wake. ***Lengo ni kuona kuwa kila kaya inakuwa na huduma ya umeme***

***na kwamba panakuwa na umeme wa kutosha kwa ajili ya shughuli za uzalishaji. Katika kufikia azma hiyo, Serikali itaelekezwa kutekeleza yafuatayo:***

i. Kuongeza matumizi ya uhakika ya umeme kwa mtu kutoka 103 kWh hadi kufikia 300 kWh ifikapo mwaka 2030 kwa kuchukua hatua zifuatazo:

   a. Kuimarisha uzalishaji wa umeme kutoka Megawati 3,077.96 mwaka 2024 hadi kufikia Megawati 8,000 ifikapo mwaka 2030;

   b. Kuimarisha mifumo ya usafirishaji wa umeme kutoka kilomita 7,745.4 mwaka 2024 hadi kufikia kilomita 13,366.85 mwaka 2030 ili kupunguza upotevu wa umeme wakati wa usafirishaji kutoka asilimia 16 mwaka 2024 hadi kufikia asilimia 10 mwaka 2030, pamoja na kuhakikisha upatikanaji wa umeme wa uhakika katika meneo ya kimkakati ikiwamo mashamba na viwanda;

   c. Kukamilisha usambazaji wa umeme nchini, ikiwa ni pamoja na kupeleka umeme katika vitongoji 31,532 vilivyosalia, sawa na asilimia 49 ya vitongoji vya Tanzania Bara pamoja na kuunganisha umeme katika kaya na taasisi; na

   d. Kuimarisha uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme kwenye maeneo yaliyo mbali na gridi ya Taifa kwa kushirikisha sekta binafsi.

ii. Kuwezesha upatikanaji wa umeme wa uhakika kwa ajili ya uendeshaji wa treni ya kisasa ya umeme (SGR) kwa kujenga njia za Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 220 kutoka Makutopora hadi Tabora (SGR Lot III); Tabora hadi Isaka (SGR Lot IV), Mwanza hadi Isaka (SGR Lot V) na Tabora hadi Kigoma (SGR Lot VI);

iii. Kuhamasisha tafiti, bunifu na uwekezaji katika teknolojia zinazohusu uzalishaji wa nishati mbadala ikiwamo jua, upepo, na mawimbi ya bahari;

iv. Kuweka mfumo mpya wa kisera, kisheria na kikanuni utakaotoa fursa kwa sekta binasi kushiriki katika uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa huduma ya umeme.

v. Kuimarisha matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa kuhakikisha asilimia isiyopungua 50 ya Watanzania wanatumia nishati safi ifikapo mwaka 2030 kwa kuchukua hatua zifuatazo:

   a. Kuhamasisha matumizi na uwekezaji wa nishati safi ya kupikia kwa kuweka vivutio ili kuimarisha matumizi ya nishati hiyo;

   b. Kupunguza gharama za nishati safi, vifaa na majiko sanifu ya kupikia pamoja na kutoa elimu ili kuwezesha wananchi hususan wa kipato cha chini kutumia nishati safi; na

   c. Kuongeza wigo wa tafiti na ubunifu wa teknolojia zinazohusu nishati safi ya kupikia ili kusaidia katika upatikanaji wa vifaa na malighafi kwa gharama nafuu na hivyo kuongeza wigo wa matumizi ya nishati safi.

### 2.1.3.6 Kuimarisha Matumizi Endelevu ya Ardhi

22. CCM inatambua kuwa ardhi ni rasilimali muhimu inayotumika kwa ajili ya shughuli mbalimbali ikiwamo kilimo, viwanda, uchimbaji wa madini, na utunzaji wa mazingira kwa maendeleo. Aidha, CCM inatambua kuwa ardhi ni rasilimali ya kwanza ambayo kila raia anaweza kumiliki. ***Hivyo, CCM itaendelea kuisimamia Serikali kutunga sera na sheria zitakazohakikisha umiliki sawa na matumizi endelevu ya ardhi. Katika kutekeleza azma hii, Chama kitaielekeza Serikali kutekeleza masuala yafuatayo:-***

    i. Kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji na miji kwa kusajili na kumilikisha hatimiliki;
    ii. Kuanzisha benki ya ardhi iliyopangwa na kupimwa kwa ajili ya matumizi mbalimbali ya maendeleo na hifadhi;
    iii. Kulinda maeneo ya ardhi ya kilimo kwa wakulima na malisho ya mifugo kwa wafugaji kwa kuimarisha sera na sheria;
    iv. Kuimarisha upatikanaji, utunzaji wa kumbukumbu na utoaji wa huduma na taarifa sahihi za ardhi kwa wakati katika ngazi zote nchini; na
    v. Kusimamia na kuratibu uandaaji na ukamilishaji wa Mipango Kabambe ya miji mbalimbali nchini ili kuwezesha upangaji, upimaji na umilikishaji ardhi kufanyika kwa gharama nafuu. Vilevile, kusimamia na kuratibu ukuaji na uendelezaji wa Miji katika mikoa yote pamoja na kuimarisha ufuatiliaji na tathmini ya mipango hiyo

### 2.1.3.7 Kuimarisha Sekta ya Utalii

23. Sekta ya utalii ni muhimu katika kuchochea ukuaji wa uchumi na maendeleo ya Taifa kwa ujumla. Katika kipindi cha utekelezaji wa Ilani hii, Chama cha Mapinduzi kitaielekeza Serikali kuongeza wigo wa mazao ya utalii na kuendelea kuitangaza hazina ya utalii tuliyo nayo kwa mbinu za kisasa ili kuongeza idadi ya watalii. ***Lengo ni kuongeza mchango wa sekta ya utalii katika Pato la Taifa kutoka asilimia 17 mwaka 2025 hadi asilimia asilimia 20 mwaka 2030. Katika kufikia azma hiyo Chama kitaielekeza Serikali kutekeleza yafuatayo:*** -

    i. Kuimarisha mikakati ya kutangaza na kuvutia watalii wa ndani na nje ya nchi kwa kuanzisha kampeni maalumu ya kufikisha idadi ya watalii milioni nane (8,000,000) kwa mwaka ifikapo mwaka 2030;
    ii. Kukuza na kuongeza idadi ya watalii wa mikutano na maonesho kwa kujenga vituo vya kisasa vya mikutano na maonesho katika majiji makubwa ya Dar es Salaam, Dodoma, Arusha na Mwanza;
    iii. Kuhamasisha uwekezaji katika ujenzi wa hoteli, hosteli za vijana na nyumba za kulala wageni ili kuongeza uwezo wa nchi kupokea watalii;
    iv. Kuongeza ajira kwenye sekta ya utalii kutoka ajira 1.5 milioni mwaka 2024 hadi ajira milioni tatu ifikapo mwaka 2030 kwa kuongeza uwekezaji katika maeneo ya utalii na ujuzi katika fani za utalii ikiwamo uongozaji wa watalii, huduma kwa wateja, na usimamizi wa hoteli;

v. Kuimarisha miundombinu ya utalii itakayowezesha kufungua vivutio vya utalii na kuvifanya kufikika kwa urahisi na usalama;

vi. Kubuni na kutekeleza mikakati ya kuongeza na kukuza wigo wa vivutio ya utalii ikiwamo: -

a. Kutumia utajiri wa historia na makumbusho tuliyonayo;

b. Kuboresha michezo, burudani, mazingira, utamaduni, malikale, uwindaji, kumbi za mikutano, fukwe, meli, matukio, jiolojia, ikolojia;

c. Kuendeleza utalii wa miji *(city tourism)*; na

### 2.1.3.8 Kuimarisha Mchango wa Uchumi wa Buluu katika Uchumi wa Taifa

24. CCM inatambua fursa za kiuchumi zilizopo katika rasilimali za maji, zikiwamo bahari, mito, mabwawa, na maziwa. Hata hivyo, fursa ya uchumi wa buluu haijatumika kikamilifu katika kuchangia katika maendeleo ya uchumi wa nchi. ***Katika kukuza sekta ya uchumi wa buluu, CCM itaielekeza Serikali kuchukua hatua zifuatazo: -***

i. Kuongeza fursa za masoko ya bidhaa za uvuvi na mwani ili kuwawezesha wavuvi na wakulima kuwa na uhakika wa masoko

ii. Kuwezesha upatikanaji wa mitaji/ mikopo na vifaa kwa wavuvi na wakuzaji viumbe maji, vyama vya ushirika na wawekezaji kwa kushirikisha taasisi za kifedha ili kuwawezesha kushiriki kikamilifu katika uvuvi na ukuzaji viumbe maji kwa njia ya kisasa na kibiashara;

iii. Kujenga bandari ya uvuvi Bagamoyo na kukamilisha ujenzi wa Bandari ya Uvuvi Kilwa itakayochangia kuongeza Pato la Taifa, matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi, na ajira;

iv. Kujenga mabwawa ya ufugaji wa samaki na vizimba vya kufugia samaki baharini na kuanzisha vituo vipya vya ukuzaji viumbe maji katika Ziwa Tanganyika, Ziwa Nyasa na maeneo mengine ya nchi ili kuhamasisha uwekezaji katika ukuzaji wa viumbe maji kibiashara;

v. Kuimarisha miundombinu ya uvuvi kwa kukarabati na kujenga mialo na masoko ya samaki ili kuongeza thamani na ubora wa samaki na kupunguza upotevu wa mazao ya uvuvi;

vi. Kuimarisha usimamizi wa uvuvi nchini ikiwamo kukamilisha uanzishwaji wa Mamlaka ya Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi ili kuongeza ufanisi wa uendelezaji wa rasilimali za uvuvi;

vii. Kununua meli za uvuvi zitakazowezesha kuvua eneo la bahari kuu ili kuongeza upatikanaji wa mazao yatokanayo na uvuvi kwa ajili ya matumizi ya ndani ya nchi pamoja na kuongeza mauzo ya nje ya nchi;

viii. Kuwajengea wavuvi wazalendo uwezo wa kufanya uvuvi wa kisasa kwa kuwapatia mafunzo na nyenzo;

ix. Kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika sekta ya uvuvi ikiwamo uzalishaji wa vifaranga bora ili kupunguza gharama za uzalishaji; na

x. Kuendeleza mpango wa ujenzi wa mashamba darasa ya ukuzaji viumbe maji katika Halmashauri za Wilaya ili kusogeza huduma za ugani na utoaji wa mafunzo kwa vitendo kwa wananchi katika maeneo hayo; na

xi. Kuanzisha programu maalumu ya kupandikiza rejesha na kujazilia samaki walio katika hatari ya kutoweka kwa lengo la kuendeleza zao la samaki kama nyenzo ya uchumi na lishe.

### 2.1.3.9 Kuimarisha Utafutaji wa Mafuta na Matumizi ya Gesi Asilia

25. CCM inatambua kuwa nchi yetu ina fursa kubwa ya kunufaika na rasilimali za mafuta na gesi asilia. Ili kutumia fursa hizo ni muhimu kuwa na mikakati thabiti ikiwamo kuimarisha tafiti na utafutaji wa mafuta pamoja na kuimarisha miundombinu itakayowezesha kuongeza usambazaji wa huduma ya gesi asilia kwa wananchi wengi na kwa gharama nafuu. ***Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Chama kitaielekeza Serikali kuimarisha sekta ndogo ya mafuta na gesi asilia ili kuimarisha mchango wake katika uchumi pamoja na kunufaisha wananchi kwa kutekeleza mikakati ifuatayo:***

i. Kuimarisha ushiriki wa wazawa na sekta binafsi katika shughuli za mafuta na gesi asilia;

ii. Kuanza utekelezaji wa Mradi wa kuchakata na kusindika Gesi Asilia kuwa Kimiminika (Liquefied Natural Gas – LNG). Katika utekelezaji wa mradi huu, CCM itahakikisha kuwa mikataba ya ujenzi na uuzaji wa gesi inazingatia maslahi mapana ya nchi. Aidha, CCM itahakikisha kuwa Serikali inaweka Sheria na Kanuni zitakazohakikisha ushiriki wa Watanzania katika hatua zote za ujenzi wa mradi.

iii. Kuendelea na ujenzi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (East African Crude Oil Pipeline - EACOP) pamoja na kutekeleza miradi na programu za kupeleka mafuta na gesi asilia nje za nchi;

iv. Kuimarisha shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi asilia pamoja na uzalishaji, usambazaji na matumizi ya gesi asilia katika viwanda, taasisi, majumbani na kwenye magari;

v. Kuhakikisha kuna upatikanaji wa mafuta ya kutosha na ya akiba nchini ikiwamo kujenga miundombinu ya hifadhi ya mafuta;

vi. Kujenga miundombinu ya vituo vya magari ya gesi na umeme; na

vii. Kuimarisha na kuongeza upatikanaji na matumizi ya gesi (CNG) kwa ajili ya uzalishaji wa mbolea pamoja na uendeshaji wa magari na mitambo hadi kufikia angalau asilimia 20 ya magari yote.

### 2.1.3.10 Uhifadhi ya Mazingira na Ustahimilivu Mabadiliko ya Tabianchi

26. CCM inatambua umuhimu wa uhifadhi wa mazingira katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwa maendeleo endelevu. Katika kipindi cha mwaka 2025 - 2030 Chama kitaendelea kuisimamia Serikali kutekeleza sera, sheria, mikakati, miongozo na miradi mbalimbali ya hifadhi ya mazingira kwa ajili ya kupunguza athari zinazosababishwa na uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi. ***Chama kitaielekeza serikali kuchukua hatua mahsusi katika kuhifadhi mazingira na kuimarisha mikakati ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kama ifuatavyo: -***

i. Kutekeleza mpango wa matumizi ya maeneo ya maji bahari na maji baridi kwa kushirikiana na wananchi na wadau;

ii. Kuwajengea wananchi uelewa kuhusu mfumo bora wa biashara ya Kaboni ili kulinda maslahi ya wananchi na Taifa;

iii. Kuimarisha uwezo wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ili kupunguza athari kwa Taifa;

iv. Kuhamasisha upandaji, utunzaji na ukuzaji miti milioni 1.5 kila mwaka katika kila halmashauri ili kudhibiti hali ya jangwa na ukame;

v. Kutekeleza programu mbalimbali za ufugaji nyuki kwa lengo la kuongeza kiwango na uzalishaji wa asali na mazao mengine ya nyuki;

vi. Kuanzisha vituo vitatu vya kuhifadhia asali katika kanda tatu kwa lengo la kuongeza thamani na kuongeza mauzo ya asali bora katika masoko ya kitaifa na kimataifa;

vii. Kuimarisha mifumo ya tahadhari ya mapema kwa kujenga mifumo ya kidijitali itakayowezesha wananchi na serikali kupata taarifa za haraka kuhusu majanga kama vile mafuriko, ukame, moto au matetemeko ya ardhi ili kuchukua tahadhari za mapema; na

viii. Kufufua ujenzi wa Bwawa la Kidete katika Mto Mkondoa kwa lengo la kuzuia mafuriko, kulinda miundombinu ya reli ya SGR na MGR na kuendeleza kilimo cha umwagiliaji.

## 2.2 Kuongeza Fursa za Ajira kwa Vijana, Kuongeza Kipato kwa Wananchi na Kupunguza Umaskini

27. CCM inatambua kuwa nyenzo kubwa ya kuwawezesha wananchi kuongeza kipato na kuondokana na umaskini ni kuongeza fursa za ajira kwa kuongeza shughuli za kiuchumi. Hivyo, Chama kitaendelea kuisimamia Serikali kuhakikisha kuwa inakuza na kuwezesha shughuli za kiuchumi zinazoanzishwa na kuendeshwa na Watanzania ili kuwapa fursa ya kuendelea kushiriki katika shughuli za kiuchumi.

28. Ili kujenga mazingira ya kuongeza kipato na kupunguza umaskini, CCM itaisimamia Serikali kuweka mazingira sahihi ya kuzalisha fursa za ajira kwa vijana na uwezeshaji wa wananchi kiuchumi, hususan kwa makundi maalumu ya vijana, wanawake, watu wenye ulemavu, na wazee.

29. Kwa ujumla, hatua za kukuza na kuimarisha sekta za kimageuzi zilizoainishwa hapo juu zinalenga kuchochea upatikanaji wa ajira. Lengo la CCM katika miaka mitano ijayo ni kuzalisha ajira zenye tija zisizopungua milioni nane (8,000,000) katika sekta rasmi na isiyo rasmi. Aidha, CCM inalenga kuona kuwa nusu ya ajira hizo zinazalishwa katika sekta rasmi.

30. *Katika kuendelea kupanua fursa za ajira kwa vijana na kuwawezesha wananchi kiuchumi, CCM itaielekeza na kuisimmamia serikali kuchukua hatua za ziada zifuatazo:-*

    i. Kwa kutambua nafasi ya uzalishaji viwandani katika kuchochea na kukuza fursa za ajira, katika kipindi cha miaka mitano ijayo, CCM itaielekeza na kuisimamia serikali kuanzisha na kutekeleza

programu maalumu ya ujenzi wa miundombinu ya kongani (industrial sheds) za viwanda vidogo na vya kati vya kuongeza thamani ya mazao kwa kila mkoa na kila wilaya. Serikali itaelekezwa kujenga angalau kongani moja ya viwanda kila mkoa ikilenga kuongeza thamani ya mazao ya kilimo, uvuvi, ufugaji, misitu, madini na bidhaa za ujenzi kwa kuzingatia fursa za kijiografia katika mkoa na wilaya husika. Katika kutekeleza hili, na katika kuwapunguzia wananchi gharama, serikali itagharimia ujenzi wa kongani hizo pamoja na miundombinu muhimu kama vile barabara, maji, na umeme. Kazi ya mwekezaji (mzawa) itakuwa ni kununua na kuweka mashine husika. Aidha, CCM itaisimamia serikali kuweka mazingira rafiki ya kikodi kwa ajili ya viwanda hivi.

ii. Kuanzisha mikakati na programu maalumu kwa kushirikiana na sekta binafsi kuwawezesha wabunifu wanaoanzisha kampuni changa ikiwa ni pamoja na kuwapatia mitaji ya kuanzia, ujuzi, fursa za masoko na kuendeleza bunifu hizo;

iii. Kuwa na dirisha maalumu kwa ajili ya mitaji ya kuanzisha kampuni changa kupitia Mfuko Maalumu wa Kuwezesha Upatikanaji wa Mtaji kwa wafanyabiashara wa Kitanzania;

iv. Kuanzisha utaratibu maalumu kwa wanafunzi wa elimu ya juu kutumia muda wao wa ziada kufanya kazi katika taasisi mbalimbali ndani na nje ya vyuo;

v. Kuanzisha maeneo maalumu ya uendelezaji wa bunifu na teknolojia zinazoibuliwa ili kuzalisha ajira nyingi hususan kwa kundi la vijana;

vi. Kuweka mazingira wezeshi ya kisera na kimkakati kwa kuhamasisha uanzishwaji na kuimarisha makampuni ya vijana na Vyama vya Ushirika (SACCOS) vyenye kujiendesha kibiashara katika Halmashauri zote nchini ili yaweze kupata mikopo, mitaji na nyenzo kwa lengo la kuwezesha wananchi wengi zaidi wakiwemo wanaohitimu elimu ya juu na vyuo vya ufundi kujiajiri na kutoa ajira kwa wengine; na

vii. Kuanzisha programu maalumu ya hamasa na mafunzo kwa Watanzania ili kutumia fursa za ajira nje ya nchi.

viii. Kupitia upya mifuko ya uwezeshaji wananchi kiuchumi ili kuwa na mfumo mmoja imara na uwezo wa kuhudumia makundi mbalimbali ya wananchi;

ix. Kuimarisha utekelezaji wa Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini (TASAF) ili kuibua na kutekeleza miradi ya kuzalisha ajira, kukuza uchumi wa kaya na kuendeleza rasilimali watu; na

x. Kuweka mazingira wezeshi ili kuchochea uanzishwaji na usajili wa makampuni ya kibiashara kama sehemu ya kurasimisha sekta isiyo rasmi.

xi. Kuanzisha vituo vya mafunzo stadi kwa ajili ya kuandaaa vijana kushindana kupata fursa za ajira nje ya nchi *(Skills Development Centre for Overseas Employment)*

## 2.3 Kuboresha Maisha ya Watu na Ustawi wa Jamii

31. CCM inatambua kuwa mafanikio ya juhudi za maendeleo hudhihirika kupitia kuboreka kwa hali za maisha ya watu. Aidha, CCM inaamini kuwa kielelezo cha ubora wa maisha ya watu ni upatikanaji wa huduma bora za jamii kwa wote. Huduma hizi ni pamoja na elimu, afya, maji, umeme, hifadhi ya jamii, na makazi bora.
32. Katika miaka mitano ijayo, CCM itaendelea kuzisimamia Serikali kuendelea kuwekeza katika kupanua huduma bora za jamii na kuweka mifumo thabiti ya ugharimiaji wa huduma hizo. Lengo ni kuhakikisha wananchi wote wanapata huduma bora za jamii na kwa gharama nafuu.

### *2.3.1 Kuinua Ubora wa Elimu Katika Ngazi Zote*

33. CCM inaamini kuwa rasilimali watu ndio rasilimali kuu katika kuleta maendeleo. Ili kutumia rasilimali hiyo kikamilifu, Taifa halina budi kuinoa ili kuimarisha mchango wake katika kuchochea maendeleo. Nyenzo muhimu ya kuinoa rasilimaliwatu ni elimu. Hivyo, CCM itaendelea kuwekeza katika kupanua fursa na kuboresha elimu na mafunzo katika ngazi zote. *Lengo ni kuhakikisha kuwa mfumo wa elimu unazalisha wahitimu wenye maarifa na ujuzi stahiki na uwezo wa kushindana kimataifa. Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, CCM itaisimamia Serikali kutekeleza yafuatayo ili kuimarisha sekta ya elimu: -*

    i. Kuendelea kuimarisha usajili katika elimu ya awali na msingi ili kuhakikisha watoto wote wenye umri wa kwenda shule wanajiunga na kubaki shule. Aidha, Serikali ya CCM itaendelea kutoa elimu ya msingi na sekondari bila ada. Lengo ni kuona kuwa angalau asilimia 80 ya watoto wanaomaliza elimu ya msingi wanaendelea na elimu ya sekondari ifikapo mwaka 2030.

    ii. Kuboresha maslahi ya walimu na wanataaluma

    iii. Kusimamia utekelezaji wa sera mpya ya elimu na mafunzo na mitaala yake inayolenga kuwajengea wahitimu umahiri na hivyo kuwawezesha kuhimili ushindani katika soko la ajira;

    iv. Katika kuchochea na kuimarisha ari ya kujifunza kusiko na ukomo, Serikali itajenga maktaba ya Taifa Dodoma na kuhuisha maktaba katika ngazi za mikoa na wilaya;

    v. Kupitia upya mfumo wa ugharimiaji wa elimu ya juu nchini kwa lengo la kuboresha utaratibu wa ugharimiaji na kuelekeza sehemu kubwa ya bajeti ya elimu ya juu kugharimia programu na shughuli za kitaaluma;

    vi. Kuhakikisha kuna kuwa na miundombinu bora na ya kutosha ya kufundishia na kujifunzia ili kukidhi mahitaji ya sera mpya ya elimu na mitaala yake;

    vii. Kuimarisha elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi kwa kuhakikisha kila wilaya ina chuo cha ufundi stadi;

    viii. Kuimarisha vyuo vya mafunzo ya kati ili kuzalisha wataalamu wa kada ya kati kwa ajili ya sekta za uzalishaji na huduma;

    ix. Kuimarisha elimu ya maadili na uzalendo katika mfumo rasmi na mfumo usio rasmi wa elimu; na

    x. Kuimarisha mazingira ya kufundishia na kujifunzia, pamoja na uhuru wa kitaaluma katika taasisi za elimu ya juu ili ziweze kushindana kimataifa.

### 2.3.2 *Kuendelea kuimarisha Huduma Bora za Afya*

34. Chama kinatambua kuwa huduma bora za afya ni haki ya msingi ya kila Mtanzania kama mtaji wake wa kwanza wa kujiendeleza. Aidha, huduma bora za afya ni muhimu katika kuhakikisha wananchi wanakuwa na afya bora ili kuwawezesha kushiriki katika shughuli za maendeleo na kuboresha maisha yao. Katika kuendelea kuimarisha huduma za afya nchini, katika kipindi cha utekelezaji wa Ilani hii, Chama kitaielekeza Serikali kutekeleza yafuatayo: -

   i. Kuimarisha programu na mikakati ya kuzuia magonjwa mbalimbali ya kuambukiza na yasiyo ya kuambukiza;

   ii. Pamoja na kwamba Tanzania imepigahatuakubwakatikakudhibiti ugonjwa wa malaria, ugonjwa huu bado ni changamoto kubwa kwa uhai na afya za Watanzania. Asilimia 8 ya Watanzania wanaambukizwa vimelea vya malaria kila mwaka wengi wao wakiwa vijijini (10%) ukilinganisha na asilimia moja mijini. Aidha asilimia 93 ya Watanzania wanaishi katika maeneo yenye vimelea vya malaria, huku Tanzania ikichangia asilimia 4.4 ya vifo vyote vitokanavyo na malaria duniani. Kwa kuzingatia hali hii, CCM inaweka lengo la kuangamiza maambukizi ya vimelea vya malaria kwa Serikali kuchukua hatua zifuatazo:-

      a. Kuanzisha programu maalumu ya kuangamiza mazalia ya vimelea vya mbu kote nchini;

      b. Kuimarisha upatikanaji wa dawa za kuangamiza mazalia ya vimelea vya mbu kwa kuimarisha kiwanda cha kuzalisha dawa hizo cha Kibaha;

      c. Kuhakikisha kuwa halmashauri zote nchini zinatenga bajeti maalumu kwa ajili ya kuangamiza mazalia ya vimelea vya mbu.

   iii. Kuanza kutekeleza programu na sheria ya Bima ya Afya kwa Wote (Universal Health Insurance);

   iv. Kuimarisha upatikanaji wa bidhaa za Afya nchini kwa kuweka mazingira wezeshi kwa Sekta Binafsi kuanzisha viwanda vya bidhaa za Afya nchini; Kuimarisha MSD kuendelea na ununuzi na uzalishaji wa Bidhaa za Afya; na kugharimia ununuzi wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi kulingana na mahitaji;

   v. Kuendelea kupanua na kuimarisha miundombinu na upatikanaji wa vifaa vya kutolea huduma za afya katika ngazi zote, ikiwamo zahati, vituo vya afya, na hospitali;

   vi. Kuimarisha matumizi ya mfumo ya dijitali na akili unde katika kutoa huduma za afya nchini;

   vii. Kuendelea kuongeza wataalamu katika sekta ya afya, pamoja na kuimarisha mafunzo katka sekta ya afya;

   viii. Kuimarisha mifumo ya kutolea huduma za afya ya akili, msaada wa kisaikolojia na kijamii kwa makundi yenye uhitaji;

   ix. Kuimarisha sekta ya tiba asili ikiwamo kilimo cha mimea dawa;

   x. Kuendelea kuimarisha huduma za afya kwa akina mama wajawazito na watoto ili kudhibiti na kumaliza vifo vya akina mama wakati wa uzazi na watoto; na

xi. Kwa kutambua umuhimu wa lishe katika kujenga na kulinda afya za wananchi, CCM itahimiza na kusimamia upatikanaji wa lishe bora kwa wote kwa kuchukua hatua zifuatazo:

   a. Kuboresha huduma za lishe kwa kuimarisha uwekaji wa virutubisho katika vyakula vinavyozalishwa hapa nchini;

   b. Kuongeza huduma za lishe kwa makundi yanayoathirika kwa wingi ikiwa ni pamoja na watoto chini ya miaka mitano, wajawazito na vijana wa rika balehe;

   c. Kuhakikisha upatikanaji wa lishe bora katika shule za msingi na sekondari;

   d. Kuanzisha programu maalumu ya kutoa elimu ya umma kuhusu lishe bora; na

   e. Kuimarisha mfumo wa kitaasisi wa kusimamia tafiti na huduma za lishe nchini.

### *2.3.3 Kuimarisha Upatikanaji wa Maji Kwa Wananchi Wote*

35. CCM inatambua umuhimu wa maji katika maisha ya kila siku ya wananchi, matumizi ya viwandani pamoja na kuimarisha hali ya usafi wa mazingira. Aidha, CCM inatambua kazi kubwa ambayo Serikali imefanya katika miaka mitano iliyopita katika kuimarisha upatikanaji wa huduma ya maji kwa wananchi, hususan vijijini. Ili kuendelea kuimarisha upatikanaji wa huduma ya maji kwa wananchi wote, katika miaka mitano ijayo, Serikali ya CCM itachukua hatua zifuatazo:

   i. Kuimarisha ulinzi na uendelezaji wa vyanzo na raslimali za maji;

   ii. Kuongeza idadi ya kaya vijijini na mijini zilizofikiwa na huduma ya maji safi na salama kwa asilimia isiyopupungua 90;

   iii. Kujenga miradi ya maji na mitambo ya kutibu maji kwa ajili ya matumizi ya binadamu ili kuimarisha usalama wa maji;

   iv. Kuanzisha na kutekeleza Gridi ya Taifa ya Maji itakayotumia vyanzo vikubwa vya maji kwa ajili ya matumizi ya nyumbani, uchumi na mazingira, ikiwamo Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika, na Ziwa Nyasa. Katika miaka mitano ijayo, Serikali ya CCM itajenga mradi mkubwa wa maji kutoka Ziwa Victoria kwenda Dodoma kupitia Singida. Mradi huu utakuwa mabomba mawili, bomba moja la maji ya kunywa na bomba jingine kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji na mifugo.

   v. Kuimarisha mifumo ya uondoaji wa majitaka nchini ili kuongeza upatikanaji wa huduma hiyo kutoka asilimia 13 hadi angalau asilimia 40;

   vi. Kuongeza kasi ya uvunaji wa maji ya mvua kwa kujenga mabwawa ya ukubwa wa kati na mabwawa ya kimkakati kwa lengo la kuimarisha uwezo wa kuhifadhi maji ya mvua kwa ajili ya matumizi ya binadamu, kilimo, mifugo na uvuvi; na

   vii. Kukamilisha ujenzi wa mabwawa ya kimkakati ikiwa ni pamoja na Bwawa la Kidunda na Farkwa ili kuongeza usalama wa maji nchini.

### *2.3.4 Kuimarisha Familia na Ustawi wa Makundi Maalumu*

36. CCM inatambua kuwa familia ndiyo msingi wa Taifa. Aidha, CCM inatambua kuwa baadhi ya makundi ya watu yanahitaji uangalizi wa kipekee ili kupata fursa sawa katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Makundi hayo ni pamoja na watoto, wazee, wanawake na Watu Wenye Ulemavu. Kutokana na umuhimu huo, Chama kitaielekeza Serikali kutekeleza yafuatayo: -
    i. Kutekeleza mikakati ya kudhibiti ukatili wa kijinsia dhidi ya watoto, wasichana, wanawake, wazee na watu wenye ulemavu katika kaya, vituo vya malezi, taasisi za elimu, maeneo ya umma na binafsi;
    ii. Kuimarisha familia kama msingi wa jamii bora na imara yenye kuzingatia maadili mema ya Kitanzania;
    iii. Kuhakikisha masuala ya jinsia yanazingatiwa wakati wa maandalizi na utekelezaji wa sera, mipango, programu na miradi mbalimbali ya maendeleo;
    iv. Kuimarisha malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto pamoja na kuhakikisha mifumo ya malezi inazingatia uwajibikaji na utunzaji wa familia katika jamii;
    v. Kuimarisha huduma za ustawi kwa wazee ikiwamo huduma za afya, matunzo, na ushirikishwaji katika maamuzi na shughuli mbalimbali za maendeleo.
    vi. Kuhamasisha jamii ili kutambua na kutekeleza wajibu wa watoto kwa wazazi na wazazi kwa watoto; na
    vii. Kuwatambua na kutoa huduma kwa watu wenye ulemavu kwa kujenga miundombinu rafiki na kuhakikisha maandalizi na utekelezaji wa mipango, programu na miradi ya maendeleo yanazingatia mahitaji ya kundi hilo.

### *2.3.5 Kuimarisha Hifadhi ya Jamii kwa Wote*

37. CCM inatambua umuhimu wa hifadhi ya jamii katika kuweka kinga ya kiuchumi na kijamii kwa wananchi ili kutoa usalama wa kiuchumi na kusaidia katika kupunguza umasikini, kuleta utulivu na ustawi wa jamii. Katika kipindi cha utekelezaji wa Ilani hii, Chama kitaielekeza Serikali kuendelea kutekeleza yafuatayo: -
    i. Kuimarisha mifumo ya hifadhi ya jamii ili iwafikie wananchi wengi zaidi pamoja na kuhamasisha wananchi kwenye sekta rasmi na isiyo rasmi kujiunga na mifumo ya hifadhi ya jamii ili Watanzania walio wengi waweze kufaidika na huduma zitokanazo na mifumo ya hifadhi ya jamii ikiwamo afya na mafao mengine;
    ii. Kulipa mafao kwa wakati na kuboresha huduma kwa wastaafu ikiwamo mifumo ya uhakiki na upatikanaji wa taarifa na malipo ya mafao kwa wastaafu;
    iii. Kuimarisha usimamizi wa mifuko ya hifadhi ya jamii hususan katika uwekezaji ili kuendelea kuwa himilivu na hivyo kuwa na uwezo wa kulipa mafao kwa wakati;
    iv. Kuimarisha Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) ili kufikia wananchi wengi zaidi wa kipato cha chini;

v. Kuendelea kuboresha mafao kwa wastaafu; na

vi. Kuanzisha mafao mahsusi kwa mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi kwa wakulima, wafugaji na wavuvi wote watakaokuwa wanachama wa mpango wa hifadhi ya jamii.

### *2.3.6 Kuboresha Makazi ya Wananchi na Kuendeleza Miji*

38. CCM inatambua kuwa makazi bora ni haki ya msingi kwa kila Mtanzania na ni kichocheo muhimu cha maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Hivi sasa nchini Tanzania kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022, Tanzania ina uhaba wa nyumba 3,800,000 na uhaba huo unaongezeka kwa nyumba 300,000 kila mwaka. Wakati uhaba huo ukiongezeka, idadi ya watu itaongezeka kutoka watu milioni 61 (kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022) hadi kufikia watu milioni 78 ifikapo 2030.

39. Ili kukabiliana na uhaba wa makazi bora unaochochewa na kuongezeka kwa idadi kubwa ya watu, katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2025 – 2030), CCM itaielekeza Serikali kuchukua hatua mahsusi za kuboresha upatikanaji wa nyumba bora, salama na za gharama nafuu kwa wananchi wa kada zote – mijini na vijijini kwa kuchukua hatua zifuatazo:

i. Kutunga na kutekeleza sera ya nyumba na makazi itakayokuwa dira ya maendeleo ya sekta ya nyumba na makazi nchini;

ii. Kutunga na kutekeleza sheria, kanuni na mikakati itakayosaidia kupunguza gharama za ujenzi ili wananchi wa kipato cha chini waweze kujenga nyumba za kisasa kwa gharama nafuu. Lengo ni kuhakikisha kuwa ifikapo mwaka 2030 Serikali inajenga na/au kuwezesha ujenzi wa nyumba bora na za bei nafuu zisizopungua 50,000;

iii. Serikali itahakikisha kuwa maeneo yaliyopimwa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za makazi na biashara yanakuwa na huduma muhimu za barabara, maji, umeme na mawasiliano;

iv. Kuanzisha kanzidata ya kitaifa ya nyumba kwa lengo la kuimarisha usimamizi wa sekta ya nyumba na kuboresha mahusiano kati ya wamiliki na wapangaji wa nyumba;

v. Kuanzisha mfumo wa kitaasisi katika kuratibu biashara katika sekta ya miliki;

vi. Kuandaa mwongozo wa kitaifa utakaoelekeza mipango na ujenzi wa nyumba vijijini na mijini kwa kuzingatia mazingira na rasilimali zilizopo;

vii. Kuanzisha na kutekeleza programu maalumu ya ujenzi wa nyumba kwa makundi maalumu ya watumishi wa sekta za kitaalamu na vyombo vya ulinzi na usalama, wakiwemo walimu, polisi, madaktari, wauguzi, watumishi wa mahakama ili kuwawezesha kumiliki nyumba kabla ya kustaafu kupitia miradi ya nyumba za gharama nafuu; na

viii. Kuendelea kuyaboresha makazi holela yaliyopo katikati ya miji kwa kuanzisha programu ya kuhuisha na kujenga upya na kuwamilikisha wakazi husika.

## 2.4 Kuimarisha Miundombinu ya Usafiri na Usafirishaji

40. CCM inatambua nafasi ya miundombinu imara, ya uhakika, ya kisasa, na iliyo salama katika kuchochea maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Kimsingi, miundombinu ya usafiri na usafirishaji sio tu kwamba ni muhimili wa ukuaji wa uchumi, bali pia ni kielelezo bayana cha maendeleo mijini na vijijini. Ni kwa sababu hii Serikali ya CCM imeendelea kuwekeza katika kupanua miundombinu ya usafiri na usafirishaji. Lengo la CCM ni kutumia jiografia ya Tanzania katika kuifanya nchi yetu kuwa kitovu cha usafirishaji barani Afrika. ***Katika kutekeleza hili, katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2025 – 2030), Serikali ya CCM itaendelea kuimarisha na kuunganisha miundombinu ya usafiri ikiwamo bandari, reli, viwanja vya ndege, barabara na madaraja ili kurahisisha huduma za usafiri na usafirishaji ndani na nje ya nchi. Aidha, jitihada hizo zitaenda sambamba na uboreshaji wa mifumo ya uagizaji na utoaji wa mizigo nchini. Maeneo mahsusi yatakayopewa kipaumbele katika kuimarisha miundombinu ya usafiri na usafirishaji katika miaka mitano ijayo ni kama yafuatayo:***

### *2.4.1 Kuendelea kupanua na kuimarisha ujenzi wa barabara na madaraja*

41. Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, kipaumbele cha ujenzi wa barabara na madaraja kitawekwa katika barabara na madaraja yanayoelekea katika maeneo yanayochochea shughuli za kiuchumi na huduma za jamii. Kwa kuzingatia muktadha huu, maelekezo ya CCM katika miaka mitano ijayo ni kama yafuatayo:

i. Kukamilisha kwa kiwango cha lami ujenzi na ukarabati wa barabara zinazounganisha makao makuu ya mikoa yote nchini na zile zinazounganisha Tanzania na nchi jirani;

ii. Kufanya upanuzi na ukarabati mkubwa katika barabara zifuatazo:

   a. Dar es salaam – Kibiti-Lindi-Mingoyo (km 161);

   b. Dar es salaam – Morogoro – Dodoma – Singida - Shinyanga – Mwanza (km 477);

   c. TANZAM (Tumbatu Jct – Mangae/Melela – Mikumi – Iyovi (km 158.45);

   d. Dar es salaam – Chalinze – Segera – Arusha (km 646).

iii. Kuunganisha kwa kiwango cha lami barabara za makao makuu ya mikoa na wilaya;

iv. Kuhakikisha barabara zinazokwenda kwenye makazi ya watu, shughuli za biashara na maeneo ya uzalishaji katika miji na majiji zinakarabatiwa na kujengwa kwa kiwango cha lami;

v. Kuhakikisha kuwa barabara za vijijini zinakarabatiwa na kujengwa, ili ziweze kupitika katika kipindi chote cha mwaka;

vi. Kuendelea kuwekeza katika ujenzi wa miundombinu ya barabara na madaraja ili kurahisisha usafiri na usafirishaji, na kuunganisha maeneo ya uzalishaji na masoko;

vii. Kuhakikisha kuwa barabara zote vijijini zinakarabatiwa na kujengwa na kuwa zinapitika katika kipindi chote cha mwaka;

viii. Kuendelea na utatuzi wa msongamano wa magari mijini kwa:

a. Kuanza ujenzi wa barabara za juu (flyovers) katika makutano ya barabara katika maeneo ya Morocco, Mwenge, Magomeni na Tabata Jijini Dar es Salaam;

b. Kutekeleza miradi ya kupunguza msongamano katika miji na majiji mengine ikiwamo Mwanza, Dodoma, Arusha, Mbeya, Babati, Singida, Songea na Iringa; na

c. Kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya mabasi yaendayo haraka (BRT) Awamu ya IV - VI katika barabara za Ali Hassan Mwinyi – Morocco - Mwenge - Tegeta na Mandela kuanzia makutano ya Ubungo na Bandari, makutano ya Mandela/ Tabata – Tabata Segerea na Tabata – Kigogo; na

d. Kuboresha mfumo wa upatikanaji na uendeshaji wa mabasi yaendayo haraka (BRT) kwa kuishirikisha sekta binafsi.

ix. Kujenga Daraja la Kilambo kwenye mpaka wa mkubwa kati ya Tanzania na Msumbiji ili kuchochea na kuongeza biashara kati ya Tanzania na Msumbiji; na

x. Kuimarisha ulinzi na usalama barabarani kwa kutumia njia za kisasa, ikiwamo kufunga kamera barabarani

### *2.4.2 Kuendelea na ujenzi wa miradi ya reli*

42. Ujenzi wa miradi ya reli utapewa kipaumbele kwa reli ambazo zinafungua nchi kwa ajili ya biashara ili kutumia vizuri fursa ya kijiografia ambayo Tanzania inayo. Maelekezo ya CCM ni kutekeleza miradi ifuatayo katika kipindi cha miaka mitano ijayo.

i. Kukamilisha ujenzi wa reli ya SGR kwa kipande cha Mwanza - Isaka (km 341), Makutupora – Tabora (km 368), Tabora - Isaka (Km 165), Tabora-Kigoma (506), Uvinza- Musongati (km 156.6);

ii. Kuimarisha uendeshaji wa reli ya kati na TAZARA kwa kuendelea na ununuzi wa vifaa vya uendeshaji wa reli ikiwa ni pamoja na vichwa vya treni, mabehewa, mitambo na mashine kwa ajili ya matengenezo ya njia;

iii. Kuanza ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) kutoka Bandari ya Mtwara hadi Mbamba Bay na tawi lake kutoka Songea hadi Ludewa ili kuunganisha na mradi wa makaa ya mawe (Liganga) na madini ya chuma (Mchuchuma);

iv. Kujenga kipande reli ya kisasa (SGR) kutoka Itigi hadi Singida;

v. Kuanza ujenzi wa reli ya kisasa itakayounganisha Bandari ya Tanga kuelekea Arusha hadi Musoma (km 1,108) na itakayoungana na reli ya kisasa (SGR) ya kutoka Dar es salaam hadi Kigoma;

vi. Kujenga kituo cha reli na mtandao wake ndani ya Bandari ya Dar es Salaam;

vii. Kujenga reli na kuweka usafiri wa treni za mijini (Metro) katika majiji ya Dar es Salaam na Dodoma ili kupunguza msongamano na kurahisisha usafiri; na

viii. Kukamilisha miundombinu ya usafirishaji wa shehena za mizigo kupitia SGR pamoja na kuhamasisha matumizi yake.

### *2.4.3 Kuimarisha Bandari*

43. Tanzania ni lango la usafirishaji wa bidhaa kwa nchi saba ambazo hazikupitiwa na ushoroba wa Bahari ya Hindi. Hii ni fursa ambayo nchi inapaswa kuendelea kuitumia katika kukuza uchumi na kuimarisha mahusiano na kujipambanua kidiplomasia katika ukanda wa Afrika na duniani. Hivyo, basi maelekezo ya CCM ni kuhakikisha kuwa Serikali inaendelea kuimarisha bandari zetu kwa kutekeleza yafuatayo:
    i. Kujenga bandari mpya ya Bagamoyo;
    ii. Kujenga miundombinu ya kupokelea na kuhifadhi mafuta bandarini yenye mita za mraba 420,000 na ujenzi wa gati la kuhudumia meli za mafuta lenye uwezo wa kufunga mpaka meli nne (4) kwa wakati mmoja;
    iii. Kuboresha bandari za Dar es Salaam, Mtwara, Tanga, Kigoma, Kalema, Musoma na bandari kavu katika eneo la Kurasini - Dar es Salaam, Kwala - Pwani na Ihumwa – Dodoma;
    iv. Kujenga miundombinu ya bandari itakayounganisha Mkoa wa Kusini Unguja (Zanzibar) na Bagamoyo (Tanzania Bara);
    v. Kuendelea kuhamasisha sekta binafsi kushiriki katika uendelezaji na uendeshaji wa bandari nchini.

### *2.4.4 Vivuko na Meli*

44. Kama ilivyo kwa barabara na reli, meli ni nyenzo muhimu sana katika kuchochea ukuaji wa uchumi, kuifungua nchi na kuimarisha huduma za usafiri kwa wananchi. Katika miaka mitano ijayo, CCM itaendelea kuisimamia serikali kuendelea kuiamarisha vivuko na meli kwa kutekeleza yafuatayo:
    i. Kukarabati meli zilizopo katika maziwa makuu na kujenga meli mpya za mizigo na abiria katika Ziwa Tanganyika, Ziwa Victoria, na Bahari ya Hindi;
    ii. Kujenga meli ya mizigo kutoka Mtwara kwenda visiwa vya Comoro, nchi ambayo inaitegemea Tanzania kwa bidhaa nyingi muhimu, ikiwamo chakula
    iii. Kujenga kiwanda cha ujenzi wa meli chenye uwezo wa kuhimili meli zenye uzito wa tani 5,000 katika Ziwa Tanganyika;
    iv. Kujenga vivuko vipya na kukarabati vilivyopo ili kuimarisha usalama na ubora wa huduma ya usafirishaji; na
    v. Kujenga na kukarabati miundombinu kwenye vituo vyote vya vivuko ambavyo havina miundombinu hiyo.

### *2.4.5 Kuendelea kuimarisha usafiri wa anga*

45. Katika miaka mitano iliyopita, kuanza kuimarika kwa usafiri wa anga umechochea sana shughuli za utalii na huduma ya usafiri kwa wananchi kwa ujumla. Ni lengo la CCM kuona kuwa usafiri wa anga nchini unaendelea kuimarika kwa kutekeleza yafuatayo:
    i. Kuendelea kuimarisha Shirika la Ndege Tanzania kwa kuongeza idadi ya ndege za abiria na mizigo, na kuboresha uendeshaji wake
    ii. Kukamilisha ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato Dodoma;
    iii. Kukamilisha ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Mwanza na kukipandisha hadhi kuwa cha Kimataifa;
    iv. Kukamilisha ukarabati na upanuzi wa viwanja vya ndege vya Tanga, Lake Manyara, Lindi na Iringa;

v. Kuboresha na kupanua jengo la pili la abiria katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere;

vi. Kujenga viwanja vipya vya ndege vifuatavyo:

a. Omukajunguti (Kagera);

b. Mugumu (Serengeti - Mara); na

c. Mikumi (Morogoro).

d. Singi

vi. Kujenga hoteli katika viwanja vikubwa vya ndege (Dar es Salaam na Kilimanjaro).

## 2.5 Kukuza Matumizi ya Sayansi na Teknolojia Katika Shughuli za Kiuchumi na Kijamii

46. Sayansi, teknolojia na ubunifu ni vichocheo muhimu vinavyoharakisha kasi ya ukuaji wa uchumi ambao ni jumuishi, shirikishi na endelevu. Kutokana na umuhimu huo, mikakati madhubuti itakayowezesha nchi yetu kunufaika na maendeleo ya sayansi, teknolojia na ubunifu pasipo kusababisha athari hasi katika mazingira, rasilimali za asili na maadili ya Mtanzania haina budi kubuniwa na kutekelezwa kikamilifu. Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, CCM itasimamia uimarishaji wa matumizi ya sayansi na teknolojia katika kuchochea maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa kuchukua hatua zifuatazo: -

i. Kuweka mfumo wa kuwatambua na kuwawezesha Watanzania wenye vipaji na ambao wapo nje ya mfumo rasmi ili kupata mafunzo na ujuzi katika viwanda atamizi na taasisi nyingine ndani na nje ya nchi kwa lengo la kuboresha bunifu zao;

ii. Kukuza na kuendeleza wabunifu ili kulea vijana wenye vipaji vya kipekee katika uhandisi na teknolojia ili kuzalisha kundi la wanasayansi wenye umahiri wa juu zaidi wa kufanya tafiti na bunifu za viwango vya juu katika maeneo ya kimkakati kwa kuongeza na kuimarisha vituo atamizi ikiwamo katika vyuo vya ufundi, taasisi za elimu ya kati na juu;

iii. Kuwekeza katika miundombinu ya kisasa ya utafiti na ubunifu ili kuongeza mchango wa sayansi, teknolojia, ugunduzi na ubunifu katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika ngazi mbalimbali za taasisi za elimu. Ili kufikia azma hii Serikali itaongeza bajeti ya utafiti na maendeleo (R & D) ili kufikia walau asilimia 1 ya Pato la Taifa;

iv. Kuweka mazingira wezeshi kwa wataalamu wabobezi kutoka nje ya nchi kuja kufanya kazi nchini ili kuhawilisha maarifa na teknolojia kwa ajili ya maendeleo ya Taifa;

v. Kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika shughuli za kiuchumi na kijamii;

vi. Kushirikiana na sekta binafsi kuanzisha maeneo maalumu kwa ajili ya kujenga vituo vya ubunifu;

vii. Kuandaa na kutekeleza mkakati maalumu wa kutumia teknolojia zinazoibukia ikiwamo akili unde, matumizi ya roboti, satalaiti, mnyororo wa taarifa ili kuimarisha ufanisi na tija katika uzalishaji na utoaji wa huduma;

viii. Kuanzisha huduma za mawasiliano ya intaneti yenye kasi katika maeneo ya umma ikiwamo maeneo ya hospitali, taasisi za elimu na vituo vya usafiri hadi kufikia asilimia 80;

ix. Kuunda na kurusha satalaiti za kimkakati katika mzunguko wa anga la juu kwa ajili ya matumizi mbalimbali ikiwamo mawasiliano, ufuatiliaji wa hali ya hewa, na uchunguzi wa sayari;

x. Kuanzisha Kituo cha Taifa cha Usalama Mtandao kwa ajili ya ulinzi wa miundombinu ya TEHAMA na kuimarisha matumizi salama ya teknolojia ya kidijitali;

xi. Kuimarisha upatikanaji wa huduma za Serikali kwa njia ya dijitalii. Lengo la CCM ni kuona kuwa angalau asilimia 50 ya huduma zote za Serikali zinapatikana dijitali kwa lengo la kuongeza ufanisi katika kipindi cha utekelezaji wa Ilani hii; na

xii. Kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha Biashara Mtandaoni kwa ukanda wa Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika kupitia Shirika la Posta Tanzania.

## 2.6 Kudumisha Demokrasia na Utawala Bora

47. CCM inaamini kuwa misingi imara ya utawala bora, demokrasia, haki za binadamu na utawala wa sheria ni muhimu katika kuhakikisha Taifa linaendelea kuwa na amani na utulivu. Katika kipindi cha utekelezaji wa Ilani hii, Chama kitaielekeza Serikali kuendelea kuimarisha demokrasia na utawala wa sheria kwa kutekeleza yafuatayo: -

i. Kuimarisha misingi ya demokrasia kwa kuboresha mazingira wezeshi ya wananchi kushiriki katika shughuli mbalimbali za kijamii, kiuchumi na kisiasa kwa kuzingatia maadili na sheria za nchi;

ii. Kuhuisha na kukamilisha mchakato wa katiba mpya;

iii. Kuimarisha mapambano dhidi ya rushwa na ufisadi kwa kuzuia na kudhibiti vitendo vya rushwa na kuchukua hatua kali za kisheria na kinidhamu dhidi ya viongozi na watumishi wa umma wanaojihusisha na vitendo hivyo;

iv. Kuendelea kuimarisha taasisi za utawala bora, maadili, na uwajibikaji kama vile Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi katika Utumishi wa Umma, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Tanzania (TAKUKURU), na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ili ziweze kutimiza wajibu wao ipasavyo;

v. Kuendelea kuimarisha Serikali za Mitaa kama nyenzo ya demokrasia na maendeleo ya wananchi;

vi. Kuendelea kuimarisha uhuru wa asasi za kiraia na vyombo vya habari kama taasisi muhimu katika kuimarisha uwajibikaji na sauti ya wananchi; na

vii. Katika kuimarisha taasisi za kitaaluma katika kuishauri Serikali na wadau wengine wa maendeleo, itatungwa sheria ya kuundwa kwa bodi za kitaaluma na Baraza Jumuishi la kitaaluma ambazo zitakuwa na jukumu la kuishauri serikali katika masuala ya kitaaluma na kitaalamu.

48. Katika kuimarisha mnyororo wa Haki Jinai, na kwa kuzingatia mapendekezo ya Tume ya Rais ya Haki Jinai, CCM itaielekeza Serikali kuchukua hatua zifuatazo:

i. Kuhuisha mfumo wa nyumba kumi kisheria;

ii. Kuimarisha matumizi ya mitandao katika malipo na uhamishaji fedha kimtandao na udhibiti matumizi ya fedha taslim;

iii. Kuimarisha matumizi ya kamera za ulinzi (CCTV) na TEHAMA katika kubaini na kuzuia uhalifu na wahalifu;

iv. Kuanzisha mamlaka mpya na huru ya upelelezi inayojitegemea itakayojulikana kama Ofisi ya Taifa ya Upelelezi (National Bureau of Investigation) itakayokuwa na jukumu la kupeleleza makosa yote ya jinai; na

v. Kuboresha mishahara na maslahi ya askari wa Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza, na uhamiaji ikiwamo kupitia upya umri wa kustaafu na mafao ya pensheni.

49. CCM inatambua umuhimu kuimarisha Utumishi wa Umma kama mhimili muhimu wa kutekeleza misingi ya demokrasia na utawala bora. Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Chama kitaielekeza Serikali kuendelea kuimarisha mazingira ya kazi, mifumo ya utendaji kazi na uwajibikaji wa Watumishi wa Umma ili kuongeza ufanisi. Katika kufikia azma hiyo, Serikali itaelekezwa kutekeleza yafuatayo: -

i. Kufanya ukaguzi na tathmini pana ya Watumishi wa Umma (human resource audit) kwa lengo la kubaini mahitaji ya wakati ya raslimali watu katika utumishi wa umma;

ii. Kuboresha mishahara na maslahi ya watumishi wa umma;

iii. Kuimarisha mifumo ya kuongeza ufanisi na uwajibikaji kwa Watumishi wa umma;

iv. Kuendelea kuimarisha maadili ya viongozi na Watumishi wa Umma;

v. Kuendelea kujenga Utumishi wa Umma wenye sifa stahiki, uadilifu, uzalendo wa kitaifa, moyo wa kujituma, weledi, uwajibikaji, na kufanya kazi kwa bidii na kwa masilahi ya Taifa; na

vi. Kuweka mazingira ya ustawi wa Vyama vya Wafanyakazi.

## 2.7 Kudumisha Muungano, Amani, Utulivu, Usalama na Diplomasia ya Kimataifa

50. CCM ni chama kilichoanzishwa na kujengwa katika misingi ya kudumisha umoja, mshikamano, na amani kama nguzo muhimu za maendeleo. Aidha, CCM inaamini katika umoja wa Afrika, na kwamba Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ni kielelezo thabiti cha umoja huo. Hivyo, basi CCM itaendelea kuuenzi na kuulinda muungano huo kama msingi wa kuwa na Taifa imara la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika kuendelea kuimarisha Muungano na kulinda amani, utulivu na usalama nchini, CCM itaelekeza Serikali kutunga na kutekeleza sera zenye kulenga yafuatayo:

vii. Kuimarisha ulinzi na usalama wa ndani ya nchi hususan maeneo ya kimkakati kama vile bandari, viwanja vya ndege, na mipakani ili kudumisha amani, utulivu na usalama wa raia na mali zao;

viii. Kuimarisha vyombo vya ulinzi na usalama kwa kuboresha mazingira ya kazi ikiwamo makazi, vifaa, zana, mafunzo yanayoendana na teknolojia na mifumo ya intelijensia ya kisasa ili kutekeleza majukumu yao ipasavyo;

ix. Kuimarisha mikakati ya kupambana na uhalifu wa mtandao na biashara haramu ikiwamo dawa za kulevya, silaha na usafirishaji wa binadamu;

x. Kuhamasisha na kutoa elimu kwa wananchi kuhusu masuala ya ulinzi, usalama, uzalendo wa kitaifa na umuhimu wa kushiriki katika ulinzi wa Taifa ikiwa ni pamoja na kujiunga na Jeshi la Akiba na vikundi vya ulinzi shirikishi ili kuimarisha ulinzi na usalama wa nchi yetu;

xi. Kuimarisha ushirikiano na jumuiya za kikanda, kimataifa, na nchi nyingine katika nyanja za ulinzi na usalama;

xii. Kuimarisha kambi za Jeshi la Kujenga Taifa (Tanzania Bara) na Jeshi la Kujenga Uchumi (Zanzibar) ili kuwezesha wahitimu wa Kidato cha Sita na vijana wanaojitolea kwa hiyari kupata fursa ya mafunzo yanayolenga kujenga uzalendo kwa Taifa, moyo wa kujitolea na stadi za kazi;

xiii. Kuimarisha mifumo ya utambuzi wa raia na wageni ili kuimarisha udhibiti wa mienendo ya watu katika uingiaji, ukaaji na utokaji wao nchini na kuimarisha usalama ikiwa ni pamoja na kuhakikisha mifumo hiyo inasomana;

xiv. Kuimarisha usalama mijini kwa kuwekeza katika teknolojia ya ufuatiliaji kama kamera za CCTV katika majiji, pamoja na kuongeza vituo vya polisi na huduma za dharura;

xv. Kuendelea kuimarisha ushirikiano katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kati ya Serikali ya Muungano wa Tanzania (SMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ)

51. Katika kuhakikisha Tanzania inaendelea kuwa na sauti katika Jumuiya ya Kimataifa na kutoa mchango wake kikamilifu katika ujenzi wa dunia bora na yenye amani na utulivu, CCM itasimamia Serikali kuimarisha diplomasia ya kimataifa kwa kuchukua hatua zifuatazo:

i. Kuhakikisha nchi inashiriki kikamilifu katika juhudi za kujenga na kuimarisha utangamano wa Afrika Mashariki, Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika, Umoja wa Afrika na Jumuiya nyingine za Kimataifa ili kuimarisha mifumo ya haki kwa kutetea haki za binadamu na kuhakikisha kuwa haki na usawa vinazingatiwa katika kila ngazi ya utawala

ii. Kukuza diplomasia ya uchumi katika medani ya uhusiano wa uwili, kikanda na kimataifa ili kuongeza upatikanaji wa masoko ya bidhaa na huduma pamoja na kuboresha biashara za nje;

iii. Kuimarisha usimamizi na uratibu wa mikataba, itifaki, na makubaliano yaliyofikiwa baina ya Tanzania na mataifa mengine, pamoja na jumuiya za kikanda na kimataifa ili kuhakikisha nchi inafaidika ipasavyo na fursa zinazotokana na makubaliano hayo;

iv. Kuweka mazingira wezeshi na rafiki ya Watanzania waishio nje ya nchi (diaspora) kushiriki katika maendeleo ya kijamii, kiuchumi na kiutamaduni;

v. Kuimarisha balozi zetu kwa kufungua Balozi na Konseli Kuu kulingana na mahitaji na vipaumbele vya nchi pamoja na kuendeleza ujenzi na ukarabati wa majengo ya ofisi, makazi na vitega uchumi ili ziwe viungo muhimu vya kulinda maslahi ya kiuchumi ya nchi yetu kutoka katika nchi hizo;

vi. Kuhamasisha matumizi ya Kiswahili kama lugha ya diplomasia katika Jumuiya za Kikanda na Kimataifa ili kuongeza utambulisho wa Taifa na kuimarisha nafasi ya Tanzania katika majukwaa hayo;

vii. Kuendesha kampeni za kuimarisha taswira ya Tanzania kimataifa kwa kutumia mitandao ya dijitali na vyombo vya habari vya kimataifa ili kuonesha mafanikio na fursa zilizopo nchini;

viii. Kuhakikisha nchi yetu inaendelea kuwa nchi isiyofungamana na upande wowote ili kuweza kutetea maslahi ya nchi yetu kwa kuzingatia misingi ya Taifa letu;

ix. Kuwawezesha Watanzania wengi hususan vijana kupata fursa za masomo nje ya nchi, katika vituo atamizi na vituo mahiri vya kiteknolojia katika katika mataifa mbalimbali rafiki; na

x. Kuendelea kushiriki kikamilifu katika shughuli za kulinda amani kupitia misheni za kimataifa ikiwamo za Umoja wa Afrika na Umoja wa Mataifa ili kuleta utulivu katika nchi jirani na rafiki zinazokumbwa na migogoro.

## 2.8 Kudumisha Utamaduni wa Taifa na Kukuza Sanaa na Michezo

52. Utamaduni, sanaa na michezo ni sekta muhimu katika kuchochea ukuaji wa uchumi endelevu kwa kuzalisha fursa za ajira, kuchochea mauzo ya bidhaa za kitamaduni ndani na nje ya nchi, kuvutia uwekezaji, kukuza utalii na kuitangaza nchi kimataifa. Vilevile, sekta ya utamaduni, sanaa na michezo ina mchango mkubwa katika kukuza utalii nchini kupitia sherehe na makongamano mbalimbali ya kitamaduni, sanaa, na mashindano ya michezo ambayo huvutia watalii wa ndani na nje ya nchi, hivyo kuongeza mapato kupitia huduma za kitalii, usafiri, na malazi.

53. Aidha, utamaduni, sanaa na michezo ni sekta zinazoboresha afya za wananchi, kuchochea ubunifu na uvumbuzi, na kuimarisha amani na umoja wa kitaifa. Vilevile, mauzo ya bidhaa na huduma za kiutamaduni huwezesha nchi kuingiza fedha za kigeni na hivyo kukuza uchumi na kuboresha maisha ya watu. Kutokana na mchango wa sekta hizi katika maendeleo ya Taifa letu, CCM itaendelea kuielekeza Serikali kuweka mazingira rafiki kwa ajili ya kuvutia uwekezaji zaidi katika masuala ya utamaduni, sanaa na michezo.

54. ***Katika kuibua na kuendeleza utamaduni wa Taifa, Serikali ya CCM itachukua hatua zifuatazo:***

i. Kuongeza jitihada za kuitangaza Lugha ya Kiswahili kimataifa kama alama kuu ya utamaduni wa Taifa, pamoja na kutoa kipaumbele katika kutenga rasilimali fedha kwa ajili hiyo;

ii. Kufanya tafiti mbalimbali zinazolenga kuziibua na kuziendeleza mila, desturi na utamaduni chanya wa Kitanzania na kurithisha kwa vizazi vijavyo;

iii. Kulinda, kuhifadhi na kuimarisha miundombinu ya urithi wa ukombozi wa Afrika kwa ajili ya kuimarisha historia ya ukombozi na utalii. Katika kutekeleza hili, pamoja na hatua zingine, Serikali itajenga Jumba la Sanaa la Kitaifa Dodoma (National Arts Gallery);

iv. Kuendelea kuwaenzi mashujaa wa harakati za ukombozi wa Afrika kwa kuhifadhi kumbukumbu zao ili kuimarisha uzalendo kwa jamii hasa vijana;

v. Kukuza utalii wa kitamaduni kwa kuonyesha utamaduni wa Mtanzania kwa wageni kupitia matamasha, makumbusho, na safari za kitamaduni ndani na nje ya nchi.

55. ***Katika kukuza na kuendeleza sanaa nchini, Serikali ya CCM itachukua hatua zifuatazo:-***

i. Kutenga maeneo kwa ajili ya shughuli za utamaduni na sanaa na kujenga vituo vya utamaduni na sanaa katika ngazi ya mikoa kupitia Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa;

ii. Kujenga maktaba ya kisasa ya kitaifa ya muziki na filamu (National Music and Film Dijital Library);

iii. Kuimarisha mafunzo ya kitaalamu kwa wasanii na walimu wa sanaa ili kuongeza ujuzi na kuwafikia vijana wengi zaidi katika kupata mafunzo ya sanaa;

iv. Kukuza masoko ya bidhaa za sanaa ndani na nje ya nchi kwa kuhamasisha ushiriki wa wasanii katika maonesho na matamasha ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa;

v. Kuunganisha vyuo vya sanaa na wasanii walio kwenye jamii ili kuendeleza vipaji na kuhamasisha ukuaji wa sanaa nchini;

vi. Kuimarisha mifumo ya kutambua na kuwaendeleza vijana wenye vipaji vya sanaa pamoja na kuwaingiza kwenye mfumo rasmi;

vii. Kuweka mfumo imara wa kulinda hakimiliki za wasanii kwa kuimarisha sheria za hakimiliki ili kuhakikisha Taifa na wasanii wananufaika na kazi za sanaa;

viii. Kujenga studio ya uzalishaji wa filamu yenye teknolojia na vifaa vya kisasa vya uzalishaji wa filamu; na

ix. Kujenga kituo kikubwa cha burudani kwa ajili ya maonesho ya kazi za Sanaa na burudani nyingine kitaifa na kimataifa;

56. ***Katika kukuza na kuendeleza michezo nchini, Serikali ya CCM itachukua hatua zifuatazo: -***

i. Kuweka utaratibu endelevu katika ngazi zote za utawala kwa wananchi kushiriki katika michezo kwa lengo la kulinda na kuimarisha afya;

ii. Kuanzisha shule za akademia za michezo kwa lengo la kuandaa wanamichezo wa leo na baadaye;

iii. Kuendelea kuimarisha michezo katika ngazi zote za elimu ikiwamo shule za msingi, sekondari, na vyuo ili kuibua vipaji vya michezo kuanzia ngazi za chini;

iv. Kutenga, kulinda na kuendeleza angalau kiwanja kimoja cha michezo chenye hadhi ya kitaifa kwa kila mkoa;

v. Kuimarisha na kuendeleza miundombinu ya michezo itakayokidhi viwango vya ubora kitaifa na kimataifa ikiwamo kuwekeza katika ujenzi wa viwanja vya michezo vya kisasa na vituo vya mazoezi pamoja na ukarabati wa miundombinu iliyopo ili kuimarisha mazingira ya mazoezi kwa wananchi;

vi. Kuanzisha vituo vya umahiri vya kukuza vipaji vya vijana na watoto kupitia akademia za michezo katika kila halmashauri ili kuandaa kizazi kipya cha wanamichezo bora;

vii. Kuhakikisha shule maalumu zilizotengwa kwa ajili ya kukuza na kuendeleza vipaji kwa wanamichezo zinajengewa miundombinu muhimu na kupatiwa wataalamu mahiri ili kuendeleza vipaji;

viii. Kukamilisha maandalizi ya nchi kuwa mwenyeji wa Mashindano ya Mpira wa Miguu Barani Afrika (AFCON-2027) kwa kujenga na kuimarisha miundombinu ya michezo, kuhamasisha ushiriki wa wananchi, na kuandaa miundombinu muhimu wezeshi ikiwamo hoteli, migahawa na usafiri; na

ix. Kuendeleza michezo ya watu wenye ulemavu kwa kujenga miundombinu rafiki kwa matumizi ya kundi hilo.

## 2.9 Kuongeza Kasi ya Maendeleo Vijijini

57. Chama Cha Mapinduzi kinatambua kuwa wananchi wengi bado wanaishi vijijini na kwamba kasi ya maendeleo vijijini inahitaji kuongezeka na kupewa msukumo mpya. Aidha, CCM inatambua umuhimu wa kuimarisha maendeleo vijijini na kufanya vijiji vikue kiuchumi na katika huduma za jamii ili kupunguza wimbi la vijana kuhamia mijini kwa kukuza ajira. Hivyo, katika kipindi cha utekelezaji wa Ilani hii, Serikali ya CCM itaongeza kasi ya maendeleo vijijini kwa kuchukua hatua mahsusi zifuatazo:

    i. Kuendelea kuwekeza katika ujenzi wa miundombinu ya barabara na madaraja vijijini ili kurahisisha usafiri na usafirishaji, na kuunganisha maeneo ya uzalishaji na masoko. CCM itaisimamia Serikali kuhakikisha kuwa barabara zote za vijijini zinapitika katika kipindi chote cha mwaka;

    ii. Kuanza programu maalumu ya ujenzi wa nyumba bora vijijini kama ilivyoelezwa katika sehemu ya 2.3 ya Ilani hii;

    iii. Kuimarisha huduma ya mawasiliano ili kuongeza kasi na kupanua wigo wa matumizi ya teknolojia ya habari kwa wananchi wa vijijini ili kunufaika na fursa zitokanazo na shughuli za uzalishaji kiuchumi na kijamii. Serikali ya CCM itaweka sera za kikodi za kuvutia wawekezaji kuimarisha huduma ya mawasiliano vijijini;

    iv. Kuongeza kasi ya kusogeza huduma za msingi ikiwamo maji, afya, elimu na umeme vijijini;

    v. Kukuza stadi za maisha na ujuzi miongoni mwa vijana kwa kujenga na kuweka mazingira wezeshi ya ujenzi wa vyuo vya mafunzo ya amali ili kukuza ajira katika kila wilaya;

    vi. Kupitia upya mifumo ya uuzaji wa mazao ya kilimo, mifugo, na misitu kwa lengo la kunufaisha wakulima, kurahisisha na kuwezesha mazingira ya kufanya biashara vijijini;

    vii. Kuweka mazingira maalumu ya kuvutia ujenzi wa viwanda vidogo vidogo vijijini kwa lengo la kufanya uchakataji wa malighafi katika sekta za kimkakati zikiwamo kilimo, mifugo, uvuvi, na misitu ili kuongeza fursa za ajira na kupunguza upotevu wa mazao baada ya mavuno;

    viii. Kuimarisha usalama wa chakula kwa kuboresha uhifadhi wa mazao, kuwapatia wakulima teknolojia za kisasa za uhifadhi wa chakula, na kuanzisha na kuendeleza kilimo cha mazao yanayohimili ukame na mabadiliko ya tabianchi;

    ix. Kuimarisha miundombinu ya masoko ikijumuisha vituo vya ukusanyaji na uongezaji thamani;

    x. Kuweka mfumo mpya wa upatikanaji wa fedha vijijini kwa kutekeleza mpango maalumu wa kurahisisha utoaji wa huduma na kutoa mikopo yenye riba ndogo itakayowawezesha wananchi kuwekeza katika kilimo cha kisasa na shughuli za ujasiriamali; na

    xi. Kupanga matumizi bora ya ardhi, kupima na kumilikisha ardhi kwa wananchi ili kuwawezesha kupata mikopo na motisha ya kuwekeza zaidi katika kilimo, ufugaji, na shughuli nyingine za kiuchumi.

SURA

# 03.

# *Mazingatio* Maalumu ya *Ilani* kuhusu *Zanzibar*



# Ujumbe wa Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi

*Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Zanzibar na Mgombea wa Urais wa Zanzibar, 2025*

## *Ndugu Wananchi Wenzangu,*

Kwa heshima na taadhima, ninatumia fursa hii kuwashukuru kwa dhati kwa kunichagua kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi wa Awamu ya Nane katika Uchaguzi Mkuu uliofanyika Oktoba, 2020. Aidha, ninapenda kuwashukuru kwa kuendelea kudumisha amani, umoja na mshikamano wa kitaifa ambao umechangia kupata mafanikio makubwa katika kipindi cha miaka mitano (2020 – 2025) ya utekelezaji wa Ilani ya CCM, hususan katika ukuaji wa uchumi, kuimarika kwa huduma za jamii ikiwamo sekta za elimu, afya, maji na ujenzi wa miundombinu. Hali hii imewasukuma wanachama wa CCM kupitia Mkutano Maalumu wa CCM uliofanyika tarehe 18 na 19 Januari, 2025 kupendekeza jina langu kuwa Mgombea wa Urais wa Zanzibar, kupitia Chama Cha Mapinduzi.

CCM imeendelea kuhakikisha kuwa Ilani za Uchaguzi Mkuu zinaweka mazingatio maalumu kwa Zanzibar, kwa lengo la kudumisha Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar, na kuimarisha Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ikiwa ni sehemu ya tunu ya kitaifa. Katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2025 – 2030), CCM itaendelea kuweka mazingira bora na kuwa kinara wa maendeleo kwa kuweka vipaumbele muhimu vya kuinua uchumi na kuboresha ustawi wa wananchi. Miongoni mwa vipaumbele hivyo ni: kuimarisha mshikamano wa Wazanzibari kwa kudumisha amani na maridhiano; kujenga uchumi imara unaonufaisha kila mwananchi; na kuimarisha upatikanaji wa ajira hususan kwa vijana kwa kuzalisha angalau ajira 350,000 katika sekta rasmi na isiyo rasmi ifikapo mwaka 2030.

***Ndugu Wananchi wenzagu,*** CCM itaweka vipaumbele vya kuimarisha uchumi endelevu, huduma za afya, elimu na maji, miundombinu ya usafiri na usafirishaji na nishati, kuanzisha hifadhi ya Taifa ya chakula na kuongeza uzalishaji wa ndani. CCM itaweka msisitizo maalumu kuwainua wananchi kiuchumi kwa kutoa mikopo nafuu na kushajiisha matumizi ya teknolojia na mafunzo ya umahiri katika uzalishaji sambamba na kusimamia upatikanaji wa masoko. Katika kuimarisha haiba ya miji, CCM itaendelea kuanzisha makaazi bora na kusimamia maendeleo ya miji kwa kutumia teknolojia za kisasa za ujenzi unaozingatia mipango miji na usafi wa mazingira. Aidha, CCM itajikita katika kuanzisha hifadhi ya mafuta ya petroli na dizeli ili kuhakikisha upatikanaji endelevu wa nishati hiyo na kupunguza athari za mabadiliko ya bei. CCM itaimarisha ushirikiano na sekta binafsi ili kukuza sekta za uchumi wa buluu, viwanda, kilimo na huduma, kwa lengo la kuongeza Pato la Taifa na ustawi wa wananchi.

Ninakishukuru kwa dhati chama changu, CCM, kwa kututeua; mimi kuwa Mgombea wa Kiti cha Urais wa Zanzibar, na Dkt. Samia Suluhu Hassan kuwa Mgombea wa Kiti cha Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na kuridhia Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi kuwa Mgombea Mwenza. Ninaamini kwa pamoja tutaendeleza mafanikio tuliyoyapata na kufanya mengi mapya katika kufikia malengo tuliyojiwekea ya kuboresha maisha ya Watanzania.

***Ndugu Wananchi wenzangu,*** Ninaomba kura zenu za NDIYO kwangu binafsi Mgombea wa Urais wa Zanzibar, Dkt. Samia Suluhu Hassan, Mgombea Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wagombea wote wa CCM katika nafasi za Ubunge, Ujumbe wa Baraza la Wawakilishi na Udiwani. °

Kwa heshima kubwa, naahidi kwamba, nitaongeza kasi ya maendeleo kwa kuimarisha vyanzo vya mapato, kukuza uchumi wa Zanzibar, na kuhakikisha wananchi wote wananufaika na huduma bora za jamii.

***Kazi na Utu, Tunasonga Mbele!***

***Mungu Ibariki Afrika; Mungu Ibariki Tanzania***

***Kidumu Chama cha Mapinduzi***

**Dkt. Hussein Ali Mwinyi**

**Makamu Mwenyekiti wa CCM Zanzibar na Mgombea Urais wa Zanzibar Mwaka 2025**

## 3.0 Ahadi na Maelekezo ya CCM kwa Upande wa Mapinduzi ya Zanzibar (2025 – 2030)

58. Ilani ya CCM imeendelea kuwa na eneo mahsusi kuhusu Zanzibar kwa madhumuni ya kuendeleza Sera zinazoendana na upekee huo. CCM inahakikisha kwamba, Tanzania Bara na Zanzibar zinaendelea kulinda Uhuru wake, kudumisha Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar, na kuimarisha Muungano ili kuendelea kujenga Taifa linalojitegemea kiuchumi na kisiasa, lenye ustawi wa watu wake na linaloenzi na kuthamini mila nzuri, desturi na utamaduni. Kwa mwaka 2025 – 2030, CCM itaendelea kustawisha maisha ya wananchi katika sekta zote za kijamii na kiuchumi kwa kutekeleza vipaumbele vifuatavyo:

   i. Kuendelea kuwaunganisha Wazanzibari kudumisha umoja, amani, utulivu, ushirikiano, maridhiano na uvumilivu;

   ii. Kuendelea kuwashirikisha wananchi katika kujenga uchumi imara ambao utazingatia usawa na kunufaisha maeneo yote ya Zanzibar;

   iii. Kuimarisha upatikanaji wa ajira kwa vijana kwa kuzalisha angalau ajira 350,000 kwenye sekta rasmi na isiyo rasmi;

   iv. Kufanya mageuzi katika sekta ya kilimo kwa kuongeza uzalishaji wa ndani na kuhakikisha uhakika wa chakula kwa kuanzisha Hifadhi ya Taifa ya Chakula.;

   v. Kuendelea kuimarisha miundombinu wezeshi ya kiuchumi ikiwamo barabara, bandari na viwanja vya ndege ili kuweza kuunganisha huduma muhimu za kiuchumi;

   vi. Kuimarisha mifumo na mifuko ya uwezeshaji wa wananchi kiuchumi ikiwamo kuendelea kutoa mikopo, ya fedha na vifaa vya uzalishaji bila ya riba;

   vii. Kuendelea kuwekeza katika miundombinu na huduma za jamii kwa kushirikiana na sekta binafsi na kushajiisha matumizi ya teknolojia za kisasa na ubunifu ili kuleta ufanisi katika kutoa huduma bora kwa wananchi.

   viii. Kuanzisha makaazi bora na upendezeshaji wa miji kwa kuzingatia teknolojia mpya ya ujenzi, mipango miji na mipango ya usafi wa mazingira pamoja na udhibiti wa taka;

   ix. Kuanzisha hifadhi ya kitaifa ya nishati ya mafuta (petrol na dizeli) kwa lengo la kuhakikisha upatikanaji endelevu wa mafuta na kupunguza athari za mabadiliko ya bei;

   x. Kuendelea kuimarisha vivutio maalumuu ili kushajiisha wawekezaji kuleta mitaji, teknolojia na ujuzi hasa katika sekta ya uchumi wa buluu, viwanda, nishati, kilimo, utalii, miundombinu na utoaji wa huduma;

   xi. Kuweka mazingira wezeshi kwa wafanyabiashara wakubwa, wa kati na wadogo kuchangia zaidi katika uchumi, Pato la Taifa na fursa za ajira;

   xii. Kuendelea kuimarisha upatikanaji wa huduma za jamii ikiwamo maji, nishati, elimu na afya; na

   xiii. Kuendelea kufanya mapitio pamoja na kuzifuta sera, sheria, kanuni na miongozo inayokwamisha ustawi wa wananchi.

## 3.1 Kuchochea Mapinduzi ya Uchumi wa Kisasa na Endelevu

59. CCM inatambua kwamba ukuaji wa uchumi ni chachu katika kuleta maendeleo endelevu na ustawi wa wananchi. Ukuaji wa uchumi unafungamana na uimara wa sekta za uzalishaji, kuwapo kwa fursa za uwekezaji na upatikanaji wa mitaji, na ushirikishwaji wa sekta binafsi. Kwa kuzingatia umuhimu huo, CCM itaielekeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutekeleza mambo yafuatayo:

### *3.1.1 Kuendelea Kuimarisha Hali ya Uchumi*

60. Hatua za kuimarisha hali za uchumi zinalenga katika kuwajengea mazingira wezeshi wananchi wanaoishi katika kipato cha chini na kukuza uwezo wao katika kujikimu na kumudu huduma za msingi. Katika kufikia haya hatua zifuatazo zitachukuliwa: -
    i. Kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei kuwa chini ya asilimia 5 kwa mwaka;
    ii. Kuongeza ukuaji wa Pato la Taifa kutoka asilimia saba (7) na kufikia asilimia kumi (10) kwa mwaka;
    iii. Kuzalisha fursa mpya za ajira laki tatu na nusu (350,000) kwa vijana; na
    iv. Kuongeza kipato cha Mzanzibari kutoka Dola za Kimarekani 1,241 (sawa na Shilingi 3,219,898.6) mwaka 2023 kufikia Dola za Kimarekani 1880 (sawa na shilingi 4,877848) kwa mwaka.

### *3.1.2 Kuimarisha Usimamizi wa Sera za Uchumi, Fedha na Mapato*

61. CCM inatambua umuhimu wa kuwapo kwa sekta madhubuti ya fedha katika kuiwezesha Serikali kutekeleza mipango ya maendeleo na kufikia malengo yaliyowekwa. Muelekeo wa Ilani ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025 ni kuimarisha mifumo ya kifedha na upatikanaji wa mitaji ili kuimarisha uwekezaji na kuongeza ukusanyaji wa mapato ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Katika kufikia hayo CCM itailekeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutekeleza yafuatayo: -
    i. Kufanya mapitio ya Sera na Sheria zinazosimamia fedha ili kuboresha huduma za fedha;
    ii. Kuimarisha ushirikiano na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika usimamizi wa sera za fedha na kodi kwa kuzingatia mazingira maalumu ya Zanzibar.
    iii. Kuendelea kuimarisha huduma za kifedha na bima kwa mfumo wa uchumi wa Kiislamu;
    iv. Kuimarisha na kusimamia upatikanaji wa mikopo ya masharti nafuu kwa wajasiriamali na vikundi vya kijamii;
    v. Kuongeza usalama wa taasisi za kifedha katika kutoa huduma kwa wananchi;
    vi. Kuboresha upatikanaji wa huduma za kibenki kwa wananchi wa mijini na vijijini;
    vii. Kuimarisha matumizi ya mifumo ya dijitali katika utoaji wa huduma za kifedha pamoja na ulipaji na hivyo kupunguza matumizi ya fedha taslimu;

viii. Kuimarisha ukusanyaji, udhibiti na kubuni nyanzo vipya vya mapato; na

ix. Kuendeleza mchakato wa uanzishaji wa Soko la Hisa na Mitaji Zanzibar.

### 3.1.3 Kuimarisha Sekta Binafsi

62. Sekta binafsi ni muhimili muhimu kwa ukuaji wa uchumi na ustawi wa jamii. Hivyo, CCM inalenga kuleta maendeleo ya nchi na wananchi kwa ujumla kwa kuimarisha mazingira ya biashara, kuhamasisha uwekezaji, na kuimarisha ushirikiano na sekta binafsi kwa lengo la kukuza uchumi shirikishi. Katika kufikia lengo hilo, CCM itaielekeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutekeleza yafuatayo: -

i. Kuweka mazingira rafiki kwa sekta binafsi kwa kupunguza urasimu, kuimarisha utawala bora, na kutoa vivutio vya uwekezaji. Hii itajumuisha mabadiliko ya sera za kodi, udhibiti wa masoko, na kupunguza gharama za kufanya biashara;

ii. Kuimarisha ushirikiano kupitia ubia wa sekta ya umma na binafsi (PPP) na njia nyingine kama ubia na ukodishaji wa miradi ya kimkakati kama vile miundombinu, nishati mbadala, na huduma za kijamii. Ubia wa sekta ya umma na binafsi utasaidia kupunguza mzigo wa kifedha kwa serikali huku ukiongeza ufanisi wa utekelezaji wa miradi;

iii. Kutoa fursa kwa wajasiriamali kupitia mafunzo, mikopo nafuu, na kuimarisha miundombinu ya masoko. Sekta binafsi itahamasishwa kusaidia biashara ndogo na za kati (MSMEs) zinazochangia sehemu kubwa ya ajira na maendeleo ya kiuchumi;

iv. Kuhamasisha uwekezaji katika ubunifu na teknolojia za kisasa ili kuendeleza sekta za kilimo, viwanda, na huduma. Sekta binafsi itachukua nafasi muhimu katika kuboresha uzalishaji, kuongeza thamani ya bidhaa za ndani, na kuimarisha ushindani wa kimataifa;

v. Kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika sekta muhimu kama vile kilimo, utalii, nishati, afya, na elimu. Maeneo haya ni muhimu kwa ukuaji wa uchumi shirikishi na ustawi wa jamii;

vi. Kuimarisha ushirikiano baina ya sekta binafsi moja na nyingine;

vii. Kuwezesha ushiriki wa wananchi katika miradi yote mikubwa nchini; na

viii. Kuweka mazingira ya kubuni fursa za ajira hususan kwa vijana na wanawake kupitia miradi ya maendeleo, ujasiriamali, na uwekezaji katika viwanda vinavyoongeza thamani.

### 3.1.4 Kuimarisha na Kukuza Maendeleo ya Sekta za Uzalishaji

63. Sekta za uzalishaji zina mchango mkubwa katika kuongeza uzalishaji, ajira, na Pato la Taifa. Katika kipindi cha 2025 - 2030 CCM itaielekeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutekeleza yafuatayo:

#### 3.1.4.1 Kilimo

64. Kilimo ni miongoni mwa sekta muhimu kwa maendeleo na ustawi wa uchumi, upatikanaji wa chakula, na kipato kwa wananchi wengi wa Zanzibar hasa wa wanaoishi vijijini. Kutokana na umuhimu huo, CCM itaielekeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuongeza uzalishaji na huduma katika sekta ya kilimo kwa kutekeleza yafuatayo:

i. Kuleta mageuzi katika sekta ya kilimo kwa kuzingatia matumizi ya teknolojia za kuongeza uzalishaji na tija, kuimarisha miundombinu ya uzalishaji, upatikanaji wa mikopo nafuu na masoko kwa bidhaa za kilimo;

ii. Kuanzisha Hifadhi ya Taifa ya Chakula kwa kukarabati maghala manne (4) na ujenzi wa vihenge maeneo ya Dunga Unguja na Chamanangwe Pemba vyenye uwezo wa kuhifadhi tani 60,000 sambamba na kuweka mfumo wa uendeshaji na usimamizi wa hifadhi hizo;

iii. Kuandaa programu maalumuu ya kuongeza uzalishaji wa mazao ya karafuu, matunda, mboga na viungo kwa kuwahusisha vijana na kuweka vivutio kwa wasafirishaji wa bidhaa hizo nje ya nchi;

iv. Kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara kwa kuimarisha tafiti, upatikanaji wa pembejeo na huduma za ugani;

v. Kulinda na kuhifadhi maeneo ya kilimo kwa kutumia utaratibu maalumu wa kisera na kisheria;

vi. Kuandaa mifumo ya kudhibiti usalama wa chakula katika mnyororo wa chakula kwa lengo la kulinda afya za walaji;

vii. Kuimarisha mfumo wa utambuzi na udhibiti wa maradhi na wadudu waharibifu wa mazao na mimea;

viii. Kuimarisha huduma za ugani kwa kutumia mbinu za kisasa ikiwamo matumizi ya TEHAMA na kuanzisha vituo vya wakulima (farmer service centres);

ix. Kuanzisha mfumo wa upatikanaji wa huduma na pembejeo muhimu za uzalishaji ikiwa ni pamoja na mbolea, viatilifu, mbegu na miche bora, huduma za ugani na zana za kilimo kwa kushirikiana na sekta binafsi;

x. Kuandaa mpango wa kuwawezesha vijana kupata mikopo nafuu ya zana za kilimo na teknolojia za uzalishaji;

xi. Kuweka mkazo katika kuongeza uzalishaji wa mazao kwa eneo (tija) ili kukabiliana na changamoto ya udogo wa ardhi ya kilimo uliopo na kupunguza utegemezi wa chakula kutoka nje ya nchi;

xii. Kuimarisha upatikanaji wa masoko ya bidhaa za kilimo ndani na nje ya nchi ikiwamo soko la utalii;

xiii. Kujenga vyumba vya baridi kwa ajili ya kuhifadhia bidhaa za kilimo na mifugo;

xiv. Kuimarisha Chuo cha Kilimo na Mifugo kwa kuongeza fani za kilimo na mifugo; na

xv. Kushajiisha uwekezaji katika kuongeza thamani ya bidhaa za kilimo zinazozalishwa Zanzibar.

### 3.1.4.2 Mifugo

65. Mifugo ni miongoni mwa sekta muhimu za kiuchumi kwa wananchi hasa wa vijijini, na ni chanzo cha kujipatia kipato na chakula. Kutokana na umuhimu huo, CCM katika kipindi cha 2025 – 2030 itaielekeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutekeleza yafuatayo:

i. Kuleta mageuzi katika sekta ya mifugo kwa kuzingatia matumizi ya teknolojia za kuongeza uzalishaji na tija, kuimarisha miundombinu ya uzalishaji, upatikanaji wa mikopo nafuu na masoko kwa bidhaa za mifugo;

ii. Kuongeza uzalishaji wa kuku, mayai, mbuzi na kulinda masoko ya bidhaa hizo kwa kudhibiti uingizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi;

iii. Kushirikisha sekta binafsi na wawekezaji kwa kuweka vivutio katika kuanzisha viwanda viwili kwa ajili ya uzalishaji wa vifaranga na viwili kwa uzalishaji wa vyakula vya mifugo;

iv. Kuandaa programu za matumizi ya teknolojia za kisasa katika upatikanaji na uzambazaji wa mbegu bora za mifugo;

v. Kujenga vituo vya kisasa vya matibabu ya mifugo na ushauri wa kitaalamu katika kila wilaya;

vi. Kuanzisha vituo vipya vya kisasa vya kukusanyia maziwa ili kuweka mazingira mazuri ya soko kwa maziwa yanayozalishwa Zanzibar;

vii. Kuwawezesha vijana kushiriki katika ufugaji kwa kuwapatia taaluma, mikopo na masoko; na

viii. Kujenga machinjio ya kisasa ili kulinda ubora na usalama wa bidhaa za mifugo.

### 3.1.4.3 Misitu na Maliasili

66. Misitu na Maliasili ni rasilimali muhimu kwa maendeleo ya Zanzibar, CCM itaendelea na jitihada za kulinda na kusimamia maliasili na misitu ili kuhakikisha matumizi endelevu ya maliasili kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho pamoja na kuongeza ajira na kipato kwa wananchi. CCM itaielekeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutekeleza yafuatayo:

i. Kuyawezesha makundi ya vijana kwa kuwapatia mitaji na taaluma na kuwawezesha kuzalisha na kusarifu asali kibiashara;

ii. Kuongeza ushiriki wa jamii katika udhibiti na matumizi endelevu ya rasilimali za misitu kwa kuongeza misitu mipya ya hifadhi;

iii. Kuongeza vivutio katika maeneo ya uhifadhi, sambamba na kuboresha miundombinu ya huduma;

iv. Kutekeleza mpango wa kurithisha Zanzibar ya Kijani kwa kupanda miti ya aina mbali ikiwamo ya matunda, bustani, miti ya vivuli, mikoko na mingineyo;

v. Kupandisha hadhi Misitu itakayokidhi vigezo kutoka misitu ya Hifadhi za jamii na kuwa msitu wa Hifadhi ili kuimarisha utalii wa kimaumbile;

vi. Kuandaa programu za kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia itakayozingatia utoaji wa ruzuku katika bei na vifaa vya nishati safi pamoja na kujenga uelewa kwa wananchi juu ya matumizi ya nishati safi na usalama wake; na

vii. Kuandaa utaratibu wa kisheria wa kudhibiti matumizi ya nishati ya kuni/mkaa kwenye maeneo yenye matumizi makubwa kama vile makambi, dakhalia na bekari za mikate.

### 3.1.4.4 Ushirika

67. Vyama vya ushirika ikijumuisha vyama vya uzashalishaji na SACCOS ni chachu kubwa ya kuwaweka wananchi pamoja na kufanya shughuli za kiuchumi zenye kuwaongezea kipato na kuinua hali zao za maisha. CCM inatambua mchango mkubwa wa ushirika katika kuleta maendeleo ya nchi na wanachi kwa ujumla. Kwa mwaka 2025 - 2030 CCM itaielekeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutekeleza yafuatayo: -

i. Kuanzisha mifumo ya kielekroniki kurahisisha usajili, usimamizi na ukaguzi wa vyama vya ushirika;

ii. Kuhamasisha mfumo wa ushirika kujiendesha kibiashara;

iii. Kuviwezesha vyama vya ushirika kupata masoko ya uhakika;

iv. Kuhamasisha vyama vya ushirika kununua hisa katika benki ya ushirika Tanzania; na

v. Kuweka vivutio maalumu kwa lengo la kuongeza ushiriki wa Vijana na makundi mengine katika Sekta ya Ushirika.

### 3.1.4.5 Nishati

68. Upatikanaji nishati ya umeme, mafuta na gesi wenye kukidhi mahitaji ni muhimu katika kuchochea uzalishaji, upatikanaji endelevu wa huduma na ukuaji wa uchumi. Ili kuhakikisha kunakuwa na upatikanaji endelevu wa nishati, CCM itaielekeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutekeleza yafuatayo: -

i. Kuendeleza ushirikiano na sekta binafsi Kuhakikisha upatikanaji wa mafuta unaozingatia uhimilivu wa bei na uwezo wa wananchi;

ii. Kujenga miundombinu ya uhifadhi wa mafuta na gesi asilia;

iii. Kujenga miundombinu ya kisasa ya uzalishaji na usafirishaji wa nishati ya umeme;

iv. Kuwekeza katika uzalishaji wa nishati ya umeme kutokana na vyanzo vipya ikiwamo jua, upepo, mawimbi ya bahari ili kupunguza utegemezi wa chanzo kimoja;

v. Kujenga vituo maalumu vya gesi na umeme kushajiisha matumizi ya magari maalumu yanayotumia nishati hiyo;

vi. Kuendelea kufanya mageuzi ya kimuundo na utendaji katika Shirika la Umeme la Zanzibar,

vii. Kushajiisha matumizi ya nishati safi na salama kwa matumizi ya nyumbani na sehemu za huduma za kijamii ili kukabiliana na mabadiliko ya tabia ya nchi;na

viii. Kuongeza matumizi ya nishati mbadala katika sekta za kilimo, huduma za maji, elimu na Afya.

### 3.1.4.6 Madini

69. CCM inatambua kuwa sekta ya madini inaweza kuchangia fursa za ajira, pato na uchumi wa Zanzibar. Ili kufikia azma hiyo Chama kitaielekeza Serikali ya Mapinduzi Zanziba kutekeleza yafuatayo:

i. Kuanzisha utaratibu wa kisera, kisheria na miongozo ya utafutaji na uendelezaji wa madini kupitia Sekta ya Madini Zanzibar;

ii. Kuanzisha programu ya kushajiisha na ufadhili wa taaluma ya madini kwa vijana wanaojiunga na vyuo vya elimu ya juu; na

iii. Kufanya utafiti wa maeneo yenye madini pamoja na kuchora ramani ya jiolojia ya Zanzibar;

iv. Kuweka mazingira maalumu ya kuvutia sekta binafsi kuwekeza hususan katika utafiti, uchimbaji wa madini ya kimkakati; na

v. Kuimarisha udhibiti wa utoroshaji wa madini kwa kuanzisha vituo vya ukaguzi vya usafirishaji wa madini katika maeneo ya bandari na viwanja vya ndege.

### 3.1.4.7 Biashara

70. Sekta ya biashara ni muhimu katika maendeleo ya uchumi na ustawi wa wananchi kwa kuchangia katika mzunguko wa fedha, ajira, na upatikanaji wa bidhaa na huduma. Kutokana na umuhimu huo, CCM itaielekeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutekeleza yafuatayo:

i. Kuimarisha urari wa biashara kwa Uchumi wa Zanzibar kutoka -22 mwaka 2024; hadi kufikia -11.9 mwaka 2030;

ii. Kuongeza thamani ya ufanyaji biashara kutoka shilingi bilioni 1,825.5 kwa mwaka 2024 hadi kufikia shilingi bilioni 2.708.0 mwaka 2030;

iii. Kuanzisha mazingira wezeshi ikiwamo uanzishaji wa kampuni changa (startups), mitaji kupitia Mfuko Maalumu wa Kuwezesha Upatikanaji wa Mtaji kwa wafanyabiashara wa Kitanzania;

iv. Kujenga Kituo cha Kimataifa cha Biashara, eneo la Dimani;

v. Kurasimisha na kukuza tasnia ya hakimiliki za kibiashara

vi. Kuendelea kusimamia mageuzi ya urahisishaji wa kufanya biashara Zanzibar ikiwamo kuijengea uwezo Mamlaka ya Usimamizi wa Leseni;

vii. Kuendelea na program ya mapitio ya ada na tozo zilizo kero kwa wananchi na wafanyabiashara kwa lengo la kuzifuta;

viii. Kujenga Maabara za Kisasa ya Upimaji (Testing House) katika eneo la Chamanangwe Pemba na Dunga kwa Unguja kwa lengo la kudhibiti ubora wa bidhaa zinazoagizwa na kuzalishwa;

ix. Kuendelea kununua karafuu kupitia Shirika la Biashara la Taifa la Zanzibar (ZSTC) kutoka kwa wakulima kwa bei ya asilimia 80 ya thamani katika Soko la Dunia.

x. Kufungua fursa za masoko ya ndani na nje kwa bidhaa zinazozalishwa na wajasiamali wa ndani;

xi. Kuanza kusarifu mwani katika Kiwanda cha Mwani kilichopo Chamanangwe – Mkoa wa Kaskazini Pemba;

xii. Kuanzisha na kuimarisha mifumo ya kidijitali ya usajili na utunzaji wa taarifa za usajili ili huduma zote za usajili kwa Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali Zanzibar ziwe zinafanyika mtandaoni;

xiii. Kudhibiti uingizaji wa bidhaa bandia kwa kuimarisha usimamizi kwenye milango ya uingizaji wa bidhaa nchini

xiv. Kujenga maabara kwa ajili ya upimaji wa mita za maji pamoja na za umeme;

xv. Kuhakikisha kuwa leseni vibali na ruhusa za kufanya biashara zinatolewa kupitia mifumo ya kielektroniki ili kuongeza Pato la Taifa na kupunguza mianya ya upotevu wa mapato;

xvi. Kujenga eneo kwa ajili ya uhakiki wa magari ya kusafirishia mafuta;

xvii. Kuongeza uwezo wa maabara za vifungashio, vimelea, nguo na ngozi, umeme na ujenzi kuzipatia vyeti vya umahiri (accrediation) kwa lengo la kuwezesha bidhaa hizo kimataifa.

xviii. Kuendelea kushirikiana na taasisi husika katika kurahisisha biashara baina ya Tanzania Bara na Zanzibar; na

xix. Kuendelea kupitia mifumo ya kodi na bei kwa bidhaa muhimu zinazoagizwa na kuzalishwa ndani ili kupunguza utitiri wa kodi za bidhaa.

### 3.1.4.8 Viwanda

71. Viwanda ni sekta muhimu katika kukuza uchumi, kuongeza uzalishaji wa bidhaa na kuleta ajira kwa wananchi. Ili kuhakikisha Zanzibar inafaidika na sekta hii, CCM itaielekeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutekeleza yafuatayo:

i. Kuandaa programu maalumuu ya kukuza viwanda vya usindikaji wa bidhaa zinazotokana na mazao yenye thamani (high value crops) ikijumuisha viungo, mafuta ya mimea na mwani;

ii. Kuongeza mchango wa sekta ya viwanda katika Pato la Taifa kutoka asilimia 20.8 hadi asilimia 25;

iii. Kuweka mkakati wa kuanzisha viwanda vipya kupunguza uingizaji wa bidhaa kutoka nje kwa bidhaa maalumu (import substitituion strategy) na kukidhi asilimia 60 ya mahitaji ya ndani;

iv. Kuandaa mfuko maalumuu wa kukuza viwanda vidogo na kuweka vivutio vya kodi, kwa lengo la kuchochea uzalishaji wa bidhaa kwa matumizi ya ndani na nje ya nchi;

v. Kuimarisha mfuko wa maendeleo ya viwanda kusaidia viwanda vya kimkakati;

vi. Kuendeleza maeneo maalumuu ya uwekezaji wa viwanda (EPZ) ikijumuisha maeneo ya Chamanangwe Pemba na Dunga Unguja kwa kuweka miundombinu muhimu ya uzalishaji;

vii. Kuendeleza maeneo maalumuu ya viwanda (industrial parks) na kuwawezesha wazalishaji wadogo kuyatumia maeneo hayo;

viii. Kuwawezesha wawekezaji wa ndani katika kuzalisha vifungashio bora vya bidhaa kwa lengo la kukidhi mahitaji ya soko Zanzibar; na

ix. Kuiwezesha Taasisi ya Viwango kuwa na maabara ya kisasa ili kuwasaidia wazalishaji wa ndani.

#### 3.1.4.9 Ardhi

72. Ardhi ni rasilimali muhimu inayotumika kwa ajili ya shughuli mbalimbali za maendeleo ikiwamo kilimo, viwanda, utunzaji wa mazingira na uwekezaji. CCM itaendelea kuzisimamia sera na sheria zitakazohakikisha matumizi endelevu ya ardhi ili kuleta maendeleo kwa wananchi. Katika kipindi cha 2025 - 2030 CCM itaielekeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutekeleza masuala yafuatayo:

i. Kuendelea kufanya mapitio ya sera, mipango na sheria za ardhi ili kuendana na mabadiliko ya kijamii, kiuchumi, na kimazingira, pamoja na utekelezaji wa mkakati wa usimamizi wa ardhi;

ii. Kupima na kuyatangaza (gazette) maeneo ya kudumu ya ardhi kwa matumizi ya kilimo; matumizi ya viwanda na uwekezaji; maeneo ya ardhi yaliyo wazi; maeneo yaliyotengwa kwa matumizi maalumuu; maeneo ya burudani na maeneo kwa matumizi ya jamii;

iii. Kuendelea na zoezi la utambuzi na usajili wa ardhi katika maeneo ya Unguja na Pemba;

iv. Kuweka mpango maalumu wa upangaji na upimaji wa visiwa vidogo vidogo kulingana na matumizi ya wananchi na uwekezaji wa visiwa hivyo;

v. Kuendelea kupima na kuyapangia matumizi maeneo yote ya ardhi ya akiba (land bank) ili kuongeza thamani ya maeneo hayo;

vi. Kuanza mpango wa kufukia bahari kwa lengo la kupata ardhi kwa ajili ya matumizi ya maendeleo; na

vii. Kuanzisha na kuimarisha mifumo ya dijitali ya usajili wa ardhi.

### *3.1.5 Uchumi wa Buluu*

73. Kwa kuzingatia jiografia ya Zanzibar, Uchumi wa Buluu unaendelea kuwa ni kichocheo muhimu kwa maendeleo na uchumi. Uchumi wa Buluu unajumuisha maeneo ya utalii, uvuvi, mafuta na gesi asilia, miundombinu, usafiri wa baharini na usimamizi wa bahari. Ili kuhakikisha Uchumi wa Buluu unaendelea kuchangia ukuaji wa uchumi na maendeleo, CCM itaielekeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutekeleza yafuatayo: -

#### 3.1.5.1 Utalii

74. Sekta ya utalii ni mhimili muhimu kwa maendeleo na ina mchango mkubwa katika uchumi na maisha ya Wazanzibari. Ili kukuza sekta hii kwa kuboresha miundombinu na kuongeza wigo wa huduma na vivutio vya utalii kwa kuzingatia upekee wa utamaduni na jiografia ya Zanzibar, CCM itaielekeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutekeleza yafuatayo: -

    i. Kuimarisha utalii wa mikutano ya kitaifa, kikanda na kimataifa, matamasha, matibabu, maonesho na michezo;

    ii. Kuongeza idadi ya watalii wa kimataifa wanaotembelea Zanzibar kutoka 800,000 na kufikia watalii 1,500,000 sambamba na kuongeza wastani wa matumizi ya siku kwa mtalii kutoka Dola za Kimarekani 418 mwaka 2024 hadi Dola 506 kwa siku;

    iii. Kuongeza vyumba vyenye hadhi ya juu kutoka 7,626 hadi kufikia 10,000 ili kuwavutia watalii wenye hadhi kubwa;

    iv. Kuimarisha viwango vya huduma za utalii ikiwamo malazi na huduma nyinginezo kwa kuzingatia uwezo wa makundi mbalimbali ya watalii;

    v. Kuongeza idadi ya watalii wanaotembelea kisiwa cha Pemba kutoka 200,000 hadi watalii 300,000 kwa mwaka;

    vi. Kuweka viwango vya utalii endelevu katika eneo la malazi (accommodation) kwa asilimia 30 kufikia mwaka 2030 kwa kuzingatia viwango vya kimataifa;

    vii. Kuibua na kuimarisha utunzaji wa vivutio vya utalii vya kimaumbile, mashamba ya viungo na katika maeneo ya Hifadhi za Misitu kwa kushirikiana na wanajamii;

    viii. Kuendeleza matumizi ya utamaduni wa Mzanzibari katika utalii;

    ix. Kutenga eneo maalumu kwa ajili ya uuzaji wa bidhaa zinazozalishwa nchini; na

    x. Kuongeza ujuzi na umahiri katika utoaji wa huduma mbalimbali katika Sekta ya utalii.

#### 3.1.5.2 Uvuvi

75. Uvuvi utaendelea kuwa sekta ya kipaumbele katika kuongeza ajira, na mchango wake katika uchumi. CCM itaielekeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutekeleza yafuatayo:

    i. Kujenga bandari mbili kubwa za uvuvi katika eneo la Ngalawa kwa Unguja na Shumba Mjini kwa Pemba;

    ii. Kuimarisha miundombinu ya uvuvi kwa kujenga madiko na masoko makubwa mawili, Mkoani na Fungurefu na masoko madogo matano (5);

    iii. Kununua meli kubwa moja ya uvuvi wa bahari kuu;

    iv. Kujenga viwanda vya kuchakata samaki katika eneo la Shumbamjini Pemba;

v. Kuwashajiisha wawekezaji binafsi kuwekeza katika uvuvi wa bahari kuu pamoja na kuimarisha miundombinu wezeshi;

vi. Kuongeza uzalishaji wa samaki kutoka tani 80,085 mwaka 2023 na kufikia wastani wa tani 160,000 kwa mwaka 2030;

vii. Kuanzisha mamlaka kwa ajili ya kusimamia ubora na viwango vya mazao ya baharini yanayosafirishwa katika soko la kimataifa;

viii. Kuanzisha chuo cha uvuvi;

ix. Kuanzisha mamlaka maalumu itakayosimamia rasilimali za uvuvi na uhifadhi wa bahari;

x. Kujenga jengo la kitega uchumi kwa ajili ya uuzaji wa bidhaa zinazotokana na bahari katika eneo la Malindi;

xi. Kujenga mabwawa ya ufugaji wa samaki, vizimba vya kufugia samaki baharini na vitotoleshi;

xii. Kuwakuza wafugaji wa mazao ya baharini (wafugaji wa samaki, matango bahari na kaa) na kuwawezesha kufuga kibiashara; na

xiii. Kuanzisha mfumo wa ufuatiliaji na udhibiti wa uvuvi usio rasmi.

#### 3.1.5.3 Kilimo cha Mwani

76. Kilimo cha mwani ni chanzo muhimu cha uchumi kwa wananchi wanaoishi ukanda wa bahari hasa wanawake. Ili kuongeza uzalishaji na kipato cha wananchi sambamba na mchango wake katika Pato la Taifa, CCM itaielekeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutekeleza yafuatayo:

i. Kuongeza uzalishaji wa zao la mwani mkavu kutoka tani 19,715 mwaka 2024 hadi tani 40,000 kufikia mwaka 2030;

ii. Kujenga miundombinu ya kuimarisha uhifadhi na usarifu wa mwani ikiwa ni pamoja na bohari nne za kuhifadhi mwani na viwanda vitano (5) vya usarifu wa mwani;

iii. Kuendeleza tafiti zinazolenga kuhakikisha upatikanaji wa mbegu bora na kuongeza uzalishaji wa mwani wenye tija;

iv. Kuanzisha vituo saidizi vya kusarifu mwani kwa ajili ya kuongeza ubora na thamani ya bidhaa zinazozalishwa kutokana na mwani ikiwamo sabuni na dawa;

v. Kuimarisha upatikanaji wa mbegu bora za mwani kwa kuanzisha vitalu maalumu katika maeneo ya Unguja na Pemba;

vi. Kutafuta fursa za masoko ya mwani na bidhaa zake kwa wakulima na wajasiriamali;

vii. Kuwekeza katika kuongeza matumizi ya teknolojia za kisasa za usarifu wa mwani kwa uzalishaji wa dawa, virutubisho, chakula, bidhaa za urembo na nyenginezo; na.

viii. Kushajiisha matumizi ya zao la mwani ndani na nje ya nchi ili kuongeza na kupanua soko la zao hilo nchini.

#### 3.1.5.4 Mafuta na Gesi Asilia

77. CCM inaendelea kuisimamia Serikali katika kuimarisha sekta ya mafuta na gesi kwa lengo la kuendeleza jitihada za kuongeza vyanzo vya ukuaji wa uchumi wa Zanzibar. Ili kuhakikisha sekta hii inachangia maendeleo ya uchumi na ajira kwa Wazanzibari, CCM itaielekeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kufanya yafuatayo: -

i. Kuendeleza utafiti na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia katika maeneo ya Zanzibar;

ii. Kutangaza na kugawa vitalu vipya vya uwekezaji wa mafuta na gesi asilia; na

iii. Kujenga kituo cha kudumu cha kuhifadhi taarifa na sampuli za mafuta na gesi asilia.

### 3.1.5.5 Bandari

78. Kutokana na Jiografia ya Zanzibar, bandari ni sekta muhimu kwa maendeleo ya uchumi. Ili kuimarisha miundombinu na huduma za bandari na kuifanya Zanzibar kuwa kituo mahiri cha kanda, katika usafiri wa baharini, CCM itaielekeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kufanya yafuatayo: -

i. Kuendelea na ujenzi wa bandari jumuishi katika maeneo ya Mangapwani inayojumuisha bandari ya mizigo, uhifadhi wa makontena na mizigo, maegesho ya meli, maeneo maalumuu ya kuhifadhi mafuta na gesi pamoja na eneo la utawala na usimamizi wa bandari;

ii. Kujenga bandari za kisasa za abiria maeneo ya Mpigaduri na Kizimkazi kwa Unguja na bandari za Shumba na Wete kwa Pemba;

iii. Kuimarisha Bandari ya Malindi ili kutumika kwa ajili ya kutoa huduma za utalii;

iv. Kujenga chelezo cha meli (dry dock) katika bandari jumuishi ya Mangapwani;

v. Kuweka miundombinu ya mafuta kwa vyombo vya usafiri wa baharini katika bandari ya Malindi, Mpigaduri, Mkokotoni kwa Unguja na bandari ya Mkoani, Wete na Shumbamjini kwa upande wa Pemba;

vi. Kujenga bandari ya kipekee na ya kisasa katika ukanda wa Afrika ya Mashariki ambayo itaunganisha usafiri wa aina tatu (Triport) ikiwamo usafiri wa baharini (ferry and water tax), usafiri wa anga kupitia ndege zenye uwezo wa kutua baharini (sea plane) na kituo kikuu cha usafiri wa umma kupitia vyombo vya usafiri ardhini;

vii. Kujenga eneo la biashara na maonesho, maduka, na ujenzi wa hoteli ya kisasa yenye hadhi ya nyota tano (5) na maegesho ya vyombo vya baharini (Marina) katika bandari ya Mpigaduri;

viii. Kuendeleza awamu ya pili ya ujenzi wa Bandari ya Fumba kwa kutanua eneo la kuweka makontena na ujenzi wa maghala ya kuhifadhia mizigo, maegesho ya magari kwa takribani hekta 6 – 8 na ujenzi wa gati yenye urefu wa mita 225 na upana wa mita 25 utakaowezesha meli kubwa za kimataifa kufunga gati;

ix. Kugeuza bandari ya Malindi kuwa bandari ya kuhudumia meli za kitalii (Cruise Ship Terminal) itayoendana na mandhari na matakwa ya hifadhi ya Mji Mkongwe;

x. Kufanya ukarabati wa Bandari ya Mkoani na kuibadilisha matumizi yake kutoka bandari ya abiria kuwa bandari ya mizigo na makontena;

xi. Kuifanyia ukarabati mkubwa bandari ya Wesha itakayoendelea kutoa huduma za mafuta na gesi pamoja na kurekebisha eneo maalumu la bandari kwa ajili ya majahazi;

xii. Kuweka miundo mbinu pamoja na gati ya ushushaji na upakiaji wa mafuta na gesi (Conventional Buoy Mooring) katika bandari ya Mangapwani;

xiii. Kufanya mageuzi ya kitaasisi kwa kuleta ufanisi wa usimamizi na uendeshaji wa Bandari; na

xiv. Kuendeleza ujenzi wa Bandari kavu kwa kushirikiana na Sekta Binafsi.

### 3.1.5.6 Usafiri wa Baharini

79. CCM inalenga kuifanya Zanzibar kuwa kitovu cha usafiri wa baharini katika ukanda wa Afrika Mashariki kwa kuboresha miundombinu ya bandari na usafiri wa baharini. Mkazo utaelekezwa katika kuimarisha na kupanua wigo wa huduma za usafiri wa baharini ili kukuza biashara, kuongeza mapato, na kurahisisha usafiri wa abiria na mizigo kati ya visiwa vya Zanzibar na nchi jirani. CCM itaielekeza Serikali kutekeleza yafuatayo: -
    i. Kuongeza usajili wa vyombo vya abiria na mizigo vya ndani na meli za kimataifa. Usajili wa vyombo vya ndani vya abiria na mizigo kutoka 81 (abiria 13 na mizigo 68) mwaka 2024 hadi kufikia 200 mwaka 2030;
    ii. Kuongeza usajili vya vyombo vidogovodogo kutoka 2,556 vilivyopo sasa hadi kufikia 4,000 kufikia mwaka 2030;
    iii. Kuongeza usajili wa meli za kimataifa kutoka meli 973 za sasa hadi kufikia meli 2,500 ifikapo mwaka 2030;
    iv. Kuongeza idadi ya Mabaharia kutoka 4,466 waliopo sasa hadi kufikia Mabaharia 6,000 kufikia mwaka 2030;
    v. Kuongeza mchango wa Mamlaka ya Usafiri Baharini kwa Serikali kuu kutoka shilingi Bilioni 2.225 mwaka 2024/2025 hadi kufikia Bilioni 5 kufikia mwaka 2030;
    vi. Kuanzisha usafiri wa teksi za baharini kwa ajili ya kutoa huduma za usafiri kwa wananchi na watalii; na
    vii. Kujenga Chuo cha Mabaharia na huduma za meli Zanzibar.

### 3.1.5.7 Usimamizi wa Bahari

80. Usimamizi wa bahari ni muhimu kwa kuweka mazingira bora ya bahari na rasilimali endelevu kwa maendeleo na tija itokanayo na uchumi wa buluu. Ili kutilia mkazo utunzaji wa mazingira na rasilimali za bahari, CCM itaielekeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kufanya yafuatayo: -
    i. Kuweka Miongozo na Mipango endelevu ya Matumizi ya Bahari;
    ii. Kuendelea kuimarisha uhifadhi shirikishi wa maeneo tengefu ya bahari kwa kuwashirikisha wananchi na kulinda mazingira ya baharini dhidi ya uchafuzi wa mazingira unaotokana na shughuli za meli; na kuzijengea uwezo jumuiya za uhifadhi wa bahari Zanzibar; na
    iii. Kuimarisha ulinzi na usalama wa watumiaji wa bahari na mali zao.

## *3.1.6 Uhifadhi na Urithi wa Kale*

81. CCM inalenga kuimarisha sekta ya uhifadhi wa urithi wa mambo ya kale ili kutunza historia na tamaduni kwa ajili ya vizazi vya sasa na vijavyo, kuvutia watalii na kuleta maendeleo ya kiuchumi. Ili kufikia malengo hayo, CCM itaielekeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutekeleza yafuatayo: -
    i. Kuandaa mpango maalumu wa uhifadhi na kuendeleza urithi wa asili, majengo ya kihistoria na tamaduni za Zanzibar, ikiwamo sanaa, utamaduni wa Kiislamu, na tamaduni za jadi;
    ii. Kusimamia na kutekeleza uendelezaji wa viwango vya kimataifa vya uhifadhi wa urithi wa kihistoria na kuhakikisha maeneo haya yanaendelezwa kwa mujibu wa sera za uhifadhi wa urithi;

iii. Kuhifadhi asilimia 15 ya mali za urithi wa kihistoria;

iv. Kuhakikisha majengo na maeneo ya urithi yanafanyiwa ukarabati na utunzaji endelevu;

v. Kuanzisha mamlaka ya usimamizi na kuendeleza uhifadhi wa maeneo ya kihistoria na urithi;

vi. Kuendelea kushirikiana na sekta binafsi katika kuendeleza na kutunza maeneo ya kihistoria ikiwamo uwekezaji ili kuongeza Pato la Taifa;

vii. Kukarabati majengo yote ya kihistori Unguja na Pemba; na

viii. Kuimarisha vivutio asilia na vya kitamaduni.

### *3.1.7 Hifadhi ya Mazingira, Mabadiliko ya Tabianchi na Kukabiliana na Majanga*

82. CCM imedhamiria kuendelea kutekeleza maeneo maalumu ambayo yatasaidia kuimarisha ustawi wa jamii. Ili kufikia malengo hayo, CCM itaisimamia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutekeleza yafuatayo:

#### 3.1.7.1 Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi

83. CCM inatambua umuhimu wa uhifadhi wa mazingira katika kuweka uendelevu wa rasilimali na mabadiliko ya tabianchi kwa maendeleo endelevu. Ili kupunguza athari zinazosababishwa na uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi, CCM itaielekeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutekeleza yafuatayo:

i. Kuendelea kuimarisha maeneo yaliyochimbwa maliasili zisizorejesheka kwa kupanda miti na kuweka matumizi mbadala katika maeneo 11 (8 Unguja na 3 kwa Pemba) yaliochimbwa rasilimali zisizorejesheka;

ii. Kuanzisha programu za usimamizi na uendeshaji wa biashara ya hewa ya ukaa (carbon credit);

iii. Kuendelea kuimarisha maeneo yaliyoathirika na maji ya bahari kwa Unguja na Pemba;

iv. Kuongeza eneo la bahari lililohifadhiwa kutoka asilimia 10.4 hadi asilimia 16;

v. Kufanya tafiti na kuibua maeneo yaliyoathiriwa na mabadiliko ya tabianchi;

vi. Kuimarisha ulinzi wa Bahari dhidi ya matumizi yasiyosahihi na usalama wa nchi kwa kufunga rada tano (5) pamoja na vifaa vya uangalizi; na

vii. Kufanya tafiti na kuibua malighafi mbadala za ujenzi ili kupunguza utegemezi wa maliasili zisizorejesheka.

#### 3.1.7.2 Usafi wa Mazingira

i. Kuboresha sera na sheria zinazosimamia huduma za usafi wa mazingira na utunzaji wa maji machafu;

ii. Kuanzisha programu ya kukuza mandhari ya mijini na vijijini ikiwamo uwekaji wa maeneo ya bustani;

iii. Kuboresha huduma za usafi katika masoko, fukwe, vituo vya mabasi, na maeneo ya mikusanyiko ya watu;

iv. Kujenga mifumo bora ya ukusanyaji, utenganishaji, na urejelezaji wa taka ili kupunguza uchafuzi wa mazingira na kukuza matumizi ya rasilimali uendelevu;

v. Kushajiisha uwekezaji katika utaratibu wa ushirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ikiwa ni pamoja na teknolojia mpya za usimamizi wa taka; na

vi. Kuanzisha vituo vya kisasa vya kuchakata taka na kutengeneza mbolea au nishati mbadala.

#### 3.1.7.3 Kukabiliana na Majanga

84. Kuongezeka kwa shughuli za kibinaadamu na mabadiliko ya tabianchi kumeongeza changamoto za majanga asilia (ya kimaumbile). Kwa kutambua umuhimu wa kukabiliana na majanga hayo katika mipango ya maendeleo ya nchi, CCM itaielekeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutekeleza yafuatayo: -
    i. Kuimarisha uwezo wa taasisi za serikali na jamii kushughulikia majanga kwa haraka na ufanisi, ikiwamo usambazaji wa rasilimali muhimu, uratibu wa vikosi vya dharura, na utoaji wa misaada kwa waathirika;
    ii. Kujenga na kuimarisha miundombinu ya uokoaji visiwani, ikiwa ni pamoja na mafunzo kwa vikosi vya uokoaji, ununuzi wa vifaa vya kisasa, na ushirikiano wa taasisi mbalimbali katika kukabiliana na majanga makubwa kama moto, mafuriko, na ajali;
    iii. Kuandaa utaratibu wa kuvuna maji ya mvua na kuweka matumizi bora ya maji hayo katika shughuli za kilimo na kijamii;
    iv. Kuanzisha na kuboresha mifumo ya tahadhari ya mapema inayotegemea teknolojia za kisasa kwa ajili ya kufuatilia, kutabiri, na kutoa taarifa kwa wananchi kuhusu majanga yanayoweza kutokea ili kupunguza madhara;
    v. Kuufanyia mapitio Mpango wa Kujiandaa na Kukabiliana na Maafa (Zanzibar Emergency preparedness and Recovery Plan) na kutoa mafunzo kwa wadau juu ya utekelezaji wa Mpango huo;
    vi. Kuwashajiisha wananchi kujiunga na bima mbalimbali za maafa;
    vii. Kuimarisha Mfuko wa Dharura kwa kutenga bajeti maalumu ya kukabiliana na majanga; na
    viii. Kuimarisha na kuendeleza Mradi wa Zanzibar Salama kwa maeneo ambayo hayajafikiwa.

## 3.2 Kuongeza Fursa za Ajira, Kipato na Kupunguza Umaskini

### *3.2.1 Kuongeza Fursa za Ajira kwa Vijana*

85. CCM inatambua kuwapo kwa uhitaji wa ajira kwa wananchi hasa vijana. Ili kuongeza fursa za ajira kwa vijana, CCM itaelekeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutekeleza yafuatayo: -
    i. Kuendeleza programu za kukuza ujuzi na kujenga umahiri wa kazi kwa vijana zikiwamo uanagenzi, mafunzo kazini na ulezi wa kitaaluma kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kujiajiri na kuajirika katika sekta za umma na binafsi;
    ii. Kuendeleza utaratibu wa kulinda fursa za ajira kwa vijana wazawa kupitia sera na sheria;
    iii. Kuendelea kuratibu programu za kazi zinazingatia sheria, miongozo, kanuni na taratibu za usalama na afya kazini;
    iv. Kuandaa programu maalumuu za kuwavutia wawekezaji na Sekta binafsi kwa lengo la kuajiri vijana;
    v. Kutoa mafunzo mahsusi ikiwamo ujuzi kwa fani adimu (rare skills) ambazo vijana wa wameshindwa kupata fursa za ajira kutokana na kukosa ujuzi unaohitajika;

vi. Kuendelea kusimamia utekelezaji wa viwango vya kazi ili kulinda maslahi ya wafanyakazi ikiwamo mikataba, mishahara, saa za kazi na stahiki zao;

vii. Kuendeleza ushirikiano na Wizara ya Mambo ya Nje kutafuta fursa za ajira nje ya nchi kupitia mikataba ya ajira baina ya Tanzania na nchi nyengine;

viii. Kuandaa mpango maalumu wa kuwaibua vijana wajasiriamali mabingwa na kuwawezesha kukuza miradi yao ili waweze kuajiri vijana wengine pamoja na kutoa mafunzo na usimamizi kwa wajasiriamali wapya;

ix. Kuimarisha usimamizi wa usuluhishishaji na utatuzi wa migogoro ya kazi kwa lengo la kukuza mahusiano mema ya kazi baina ya waajiri na waajiriwa;

x. Kuanzisha mikakati na programu maalumu kwa kushirikiana na sekta binafsi kuwawezesha wabunifu wanaoanzisha kampuni changa ikiwa ni pamoja na kuwapatia mitaji ya kuanzia, ujuzi, fursa za masoko na kuendeleza bunifu hizo;

xi. Kuandaa mfumo wa kieletroniki wa utafutaji na uwekaji wa taarifa za fursa za ajira; na

xii. Kuanzisha ajira mpya 350,000 kwa wananchi wa Zanzibar hasa vijana katika sekta rasmi na zisizo rasmi Unguja na Pemba;

xiii. Kuandaa utaratibu wa kurithisha ujuzi (skills transfer) kutoka kwa wafanyakazi wa kigeni kwenda kwa wafanyakazi wa ndani kwa kada zinazohitajika;

xiv. Kuanzisha kampuni za Serikali katika sekta za uzalishaji na huduma zenye fursa za masoko na ajira;

xv. Kuandelea kusimamia utaratibu maalumu wa kudhibiti wageni kufanya kazi zinazopaswa kufanywa na wazawa; na

xvi. Kushajiisha Vyuo Vya Elimu ya Juu na Mafunzo ya Amali kutoa taaluma na mafunzo ili vijana kutumia fursa za ajira zitokanazo na majukwaa ya kidijitali, uchumi wa kijani (green jobs) na uchumi wa buluu.

### *3.2.2 Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi*

86. CCM imeendelea kutilia mkazo umuhimu wa maendeleo ya wananchi kupitia uwezeshaji wa wananchi kiuchumi. Chama kimeendelea kuchukua hatua mbalimbali kuwawezesha wananchi kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi. Ili kufikia lengo hilo CCM itaielekeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutekeleza yafuatayo: -

i. Kutoa mikopo ya jumla ya shilingi bilioni 100 kwa wananchi pamoja na kutoa mafunzo ya usimamizi wa fedha kwa wajasiliamali wazalishaji na wafanyabiashara sambamba na kuwapatia mafunzo ya uzalishaji na kuwaungnisha na masoko;

ii. Kutoa mikopo kwa mgawanyo ufuatao; asilimia 40 kwa vijana, asilimia 40 kwa wanawake na asilimia 20 kwa watu wenye ulemavu kwa kiwango kinachofikia shilingi bilioni 2.5 ifikapo mwaka 2030;

iii. Kuimarisha kongani za uzalishaji ili kurahisisha upatikanaji wa huduma za masoko, taaluma na ubunifu;

iv. Kuwatambua wajasiliamali wenye mafanikio na kutumia maeneo yao kama vituo vya mafunzo ya vitendo yasiyopungua miezi sita (6) na kuwatumia kama walezi wa wajasiliamali wadogo;

v. Kutoa mikopo kwa wajasiliamali wakubwa hamsini (50) na kuwawezesha kuwaajiri vijana wasiopungua hamsini (50) kila mmoja;

vi. Kuandaa muongozo wa kukuza wajasiliamali ambao utaainisha miradi yenye tija kwa kila sekta;

vii. Kuwajengea uwezo wajasiriamali na wazalishaji kwa kuwaunganisha na taasisi za viwango ili kuzalisha bidhaa zenye ubora zinazokubalika kitaifa na kimataifa;

viii. Kuanzisha Vituo vya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi katika Mikoa mitano (5) na wilaya kumi na moja(11) za Zanzibar;

ix. Kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji na tathmini ya mifuko ya uwezeshaji wananchi kiuchumi ili kuboresha urejeshaji na tija ya mikopo;

x. Kutoa huduma ya uzalishaji kwa wazalishaji mia tatu (300) katika vituo vya uzalishaji.

### *3.2.3 Maendeleo ya Sayansi na Teknolojia*

87. CCM inalenga kukuza sekta za ubunifu kwa kuendeleza ubunifu wa dijitali katika maeneo mbalimbali ikiwamo utengenezaji wa filamu, sanaa na ufundi, muziki, uchoraji, mitindo, na tasnia ya burudani kwa ujumla. Ili kufikia malengo hayo, CCM itaielekeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutekeleza yafuatayo: -

#### 3.2.3.1 Kuimarisha Sekta ya Ubunifu na Kuongeza Thamani ya Bidhaa za Utamaduni

i. Kuanzisha na kuendesha programu maalumuu za mafunzo juu ya matumizi ya dijitali katika sanaa za uchoraji, mitindo, na utengenezaji wa bidhaa za kitamaduni;

ii. Kusaidia wasanii na wajasiriamali wa kitamaduni kuingia katika soko la kimataifa kupitia majukwaa ya kidijitali ili kuwawezesha vijana kujiajiri na kuchangia uchumi wa Zanzibar;

iii. Kuongeza matumizi ya maudhui yanayotengenezwa Zanzibar katika jumla ya maudhui yanayotumiwa na watumiaji;

iv. Kuanzisha vituo vya kukuza ubunifu vya kisekta kwa ajili ya kuendeleza vipaji na ubunifu kwa vijana;

v. Kuendeleza tasnia ya ubunifu ili kuchangia ukuaji wa uchumi wa Zanzibar kupitia bidhaa za kitamaduni; na

vi. Kuanzisha maeneo maalumu *(technology parks)* ya uendelezaji wa bunifu na teknolojia zinazoibuliwa ili kuzalisha ajira nyingi hususan kwa kundi la vijana.

#### 3.2.3.2 Kuimarisha Mazingira ya Uchumi wa Dijitali na Kuongeza Upatikanaji wa Teknolojia Mpya

i. Kuimarisha uwekezaji katika miundombinu ya TEHAMA na kujenga vituo vya teknolojia vilivyokidhi viwango vya kimataifa;

ii. Kuwekeza katika Mfumo wa Mkonga wa Taifa na kuhamasisha uwekezaji wa sekta binafsi katika miundombinu ya kidijitali;

iii. Kuanzisha majukwaa ya mtandaoni na mifumo ya biashara mtandao inayosaidia masoko ya ndani, ya kanda, na kimataifa;

iv. Kuongeza kiwango cha maudhui ya kidijitali yanayotengenezwa Zanzibar na kusafirishwa nje;

v. Kuongeza idadi ya vituo vya teknolojia vyenye vyeti vya kimataifa ili kuwezesha ubunifu na uchumi wa kidijitali; na

vi. Kuimarisha mafunzo na matumizi ya teknolojia mpya katika kutatua changamoto zinazoikabili jamii yetu.

#### 3.2.3.3 Kuwezesha Elimu ya Dijitali na TEHAMA kwa Umma

i. Kuongeza mafunzo ya teknolojia ya habari na mawasiliano kwa wanafunzi katika ngazi zote za elimu ili kujenga uwezo wa teknolojia miongoni mwa vijana;

ii. Kuimarisha mafunzo ya TEHAMA, ikiwa ni pamoja na uundaji wa programu, katika skuli za msingi, sekondari, na vyuo vikuu ili kuwajengea wanafunzi ujuzi wa kuunda programu mbalimbali; na

iii. Kuimarisha mafunzo ya ujasiriamali wa kidijitali ili kukuza ujasiriamali na ubunifu.

### *3.2.4 Uchumi wa Dijitali na Uvumbuzi*

88. Uchumi wa dijitali ni sekta yenye thamani kubwa na nyenzo muhimu kwa ustawi wa sekta nyingine. Kwa azma ya kukuza uchumi wa kidijitali na uvumbuzi, kwa kuimarisha mchango wake na sekta nyingine ikiwamo utalii, CCM itaielekeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutekeleza yafuatayo: -

i. Kuimarisha upatikanaji na matumizi ya teknolojia za kidijitali katika uendeshaji wa shughuli za Serikali ili kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma;

ii. Kukuza ubunifu unaohusishwa na utalii, ikijumuisha sanaa na ufundi, muziki, na bidhaa za kitamaduni ambazo zinaweza kuvutia watalii;

iii. Kuweka sera na sheria ya matumizi ya teknolojia ya akili unde;

iv. Kuanzisha programu maalumu za mafunzo na uwekezaji kwa vijana ili kuongeza thamani ya bidhaa na huduma zinazovutia watalii; na

v. Kuongeza matumizi ya maudhui ya dijitali na bidhaa za kitamaduni zinazotumiwa na watalii.

### *3.2.5 Utafiti na Ubunifu*

89. CCM inatambua kuwa mipango ya maendeleo na utekelezaji wake inahitaji misingi madhubuti ya maarifa yanayotokana na utafiti na ubunifu. Kwa muktadha huo, CCM inalenga kukuza mbinu za utafiti na ubunifu kwa lengo la kuleta athari chanya kwa jamii na kuimarisha uchumi wa Zanzibar. Katika kufikia malengo haya, CCM itailekeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutekeleza yafuatayo: -

#### 3.2.5.2 Kuimarisha Utafiti

i. Kuratibu taasisi za utafiti kwa lengo la kuzisajili na kuzitangaza kazi zao za kitaaluma na kuwezesha matumizi ya matokeo ya tafiti hizo;

ii. Kuendelea kushirikiana na taasisi za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika utekelezaji wa sera, mipango na mikakati ya kitaifa, kikanda na kimataifa katika masuala ya utafiti na ubunifu;

iii. Kushajiisha vyuo na taasisi kupanua wigo wa utafiti na ubunifu ili kuimarisha matumizi yake;

iv. Kuhamasisha kizazi cha wanataaluma wachanga na chipukizi kufanya utafiti na ubunifu unalenga kutatua changamoto za kijamii na kiuchumi ndani na nje ya nchi na kutoa fursa za ajira;

v. Kuendelea kutenga bajeti maalumu katika utafiti na ubunifu kwa sekta za vipaumbele;

vi. Kubuni na kuimarisha ajenda za kitaifa za utafiti zitakazohusisha mipango endelevu ya uwekezaji na upangaji wa vipaumbele;

vii. Kuweka mipango ya muda mrefu inayohakikisha taasisi za utafiti zinawezeshwa kifedha na kiutawala kwa ajili ya kufanya tafiti zinazoleta matokeo yenye athari chanya;

viii. Kutumia matokeo ya tafiti katika mipango na shughuli za serikali kwa kuimarisha upatikanaji wa taarifa zinazohitajika katika kufanya maamuzi ya msingi;

ix. Kuweka mfumo wa kuhakikisha kuwa tafiti zinazofanywa zinaleta matokeo chanya yanayoweza kutumika katika sekta mbalimbali, zikiwamo sekta za umma na binafsi, na kuweka mfumo wa ushirikiano na uratibu kati ya sekta hizo;

x. Kuandaa mfumo wa ufuatiliaji na tathmini utakaowezesha kupima matokeo ya utekelezaji wa tafiti zilizofanywa;

xi. Kuhakikisha vyuo vya elimu ya ufundi, kati na juu vinaanzisha vituo atamizi;

xii. Kuongeza na kuimarisha vituo atamizi kwa ajili ya kukuza na kuendeleza wabunifu ili kulea na kuwezesha vijana na wataalamu kuendeleza ujuzi wao na kuanzisha kampuni ndogo zinazotokana na ubunifu na hivyo kuchochea, kuzalisha ajira na kuongeza uzalishaji; na

xiii. Kuimarisha na kuanzisha vituo vya umahiri katika maeneo ya kimkakati yenye mchango mkubwa katika kustawisha uchumi wa viwanda na kuboresha maisha ya Wazanzibari.

## 3.3 Huduma za Habari na Mawasiliano

90. CCM inatambua umuhimu wa sekta ya habari na mawasiliano katika maendeleo. Chama kinalenga kuimarisha huduma za habari na mawasiliano. Ili kufikia malengo hayo, Chama kitaielekeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutekeleza yafuatayo: -

### *3.3.1 Habari*

i. Kuimarisha ubora wa upatikanaji wa habari kupitia redio, televisheni, magazeti na mitandao ya kijamii katika maeneo yote ya nchi;

ii. Kuongeza idadi ya wananchi wanaotumia mifumo ya dijitali katika shughuli za maendeleo;

iii. Kuendelea kuwekeza katika kuimarisha miundombinu ya utangazaji kwa Shirika la Utangazaji la Zanzibar (ZBC) ikiwa ni pamoja na kuliunganisha na taasisi nyengine za serikali zinazotoa huduma za tasnia ya utangazaji;

iv. Kuboresha mazingira ya ufanyaji kazi wa vyombo vya habari ili kuiwezesha sekta ya habari kutoa mchango wake kikamilifu katika shughuli za maendeleo;

v. Kukamilisha miundombinu (majengo na mitambo) ya kiwanda cha uchapishaji wa magazeti ya Serikali ili kuongeza tija na ufanisi katika utoaji wa huduma;

vi. Kuendelea kufanya mageuzi ya kisera na kisheria katika Idara ya Habari Maelezo ili kusimamia masuala ya habari na kuwajengea uwezo wanahabari waweze kutimiza utendaji wa majukumu yao kwa uadilifu;

vii. Kuendelea kuimarisha uwezo wa Wakala wa Uchapaji wa Serikali kwa kuwapatia wataalamu na vifaa vya kisasa vya uchapaji na kuimarisha huduma za bohari kuu ya Wakala

viii. Kuanza ujenzi wa ofisi na kuweka vifaa vya kisasa katika Tume ya Utangazaji ili kuhakikisha kuwa maudhui yanayotolewa na vyombo vya habari (redio, televisheni, na televisheni mtandao) yanazingatia mila, silka na utamaduni wa Mzanzibari; na

ix. Kuboresha uwekezaji wa miundombinu mipya na vifaa vya kisasa katika sekta ya habari.

### *3.3.2 Mawasiliano*

i. Kuanzisha mji maizi/ mji wa kidijitali *(Smart City)* katika maeneo ya uwekezaji wa TEHAMA, Fumba;

ii. Kuboresha mawasiliano ya simu hasa katika maeneo ya visiwa vidogo vidogo;

iii. Kuiunganisha Zanzibar na mkonga wa kimataifa *(International Gateway)* kwa lengo la kuongeza ufanisi katika upatikanaji wa huduma za mtandao;

iv. Kuimarisha mfumo wa Serikali mtandao *(e-Governance)* katika utendaji wa Serikali ili kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma kwa jamii;

v. Kuanzisha mfumo wa dijitali wa tahadhari za mapema wa kukabiliana na majanga katika vituo vya dharura vya kukabiliana na majanga mbalimbali kama vile moto, mafuriko na magonjwa;

vi. Kuweka majina ya mitaa na barabara kwenye mfumo wa anuani za makaazi kwa wananchi wote wa Zanzibar ili kuzitumia katika shughuli tofauti za kijamii na kiuchumi hivyo kuimarisha huduma za mawasiliano

## 3.4 Kuboresha Maisha ya Watu na Ustawi wa Jamii

91. CCM inatambua kwamba upatikanaji wa huduma za jamii kwa wakati ni msingi wa maendeleo na kigezo muhimu cha utawala bora na uongozi wenye kujali wananchi wake. Kwa kuzingatia umuhimu huo Chama kitaielekeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutekeleza mambo yafuatayo: -

### *3.4.1 Elimu*

#### 3.4.1.1 Elimu na Mafunzo ya Amali

92. Katika miaka mitano ijayo, Chama cha Mapinduzi kinaweka kipaumbele katika kuboresha na kuimarisha sekta ya elimu na mafunzo ya amali kwa lengo la kujenga uwezo wa kitaaluma, ufundi, na ujuzi kwa wananchi wa Zanzibar. Ili kufikia malengo hayo, CCM itaielekeza Serikali kutekeleza yafuatayo: -

#### 3.4.1.2 Elimu ya Maandalizi na Msingi

i. Kuongeza kiwango cha uandikishaji katika ngazi ya elimu ya maandalizi na msingi kutoka asilimia 67.9 kwa maandalizi na 86.7 kwa msingi mwaka 2024 na kufikia asilimia 100 mwaka 2030;

ii. Kujenga skuli mbili za kisasa za maandalizi kwa kila Wilaya;

iii. Kujenga madarasa mapya 1,000 kwa elimu ya msingi yanayojumuisha skuli 10 za ghorofa;

iv. Kuimarisha programu ya lishe kwa kuongeza idadi ya skuli zinazonufaika na programu hiyo kutoka skuli 50 mwaka 2024 hadi kufikia skuli 100 mwaka 2030;

v. Kujenga vyoo 500 na sehemu za kunawia mikono kwa skuli za maandalizi na msingi; na

vi. Kuziunganisha skuli 50 za Msingi na mkonga wa Taifa ili kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika kujifunzia na kufundishia

#### 3.4.1.3 Elimu ya Sekondari

i. Kuongeza kiwango cha uandikishaji katika ngazi ya elimu ya sekondari kutoka asilimia 63.7 mwaka 2024 na kufikia asilimia 90 mwaka 2030;

ii. Kujenga skuli tatu za wanawake za Mkoa ili kuimarisha upatikanaji wa fursa za elimu ya Sekondari kwa wanafunzi wa kike;

iii. Kujenga madarasa mapya 1,000 kwa elimu ya Sekondari yanayojumusiha skuli 10 za ghorofa;

iv. Kujenga skuli tatu za ufundi ili kuwajengea vijana ujuzi unaoendana na mahitaji ya soko la ajira;

v. Kuimarisha utoaji wa mafunzo ya amali katika ngazi ya sekondari kwa kuongeza idadi ya wanafunzi wanaosoma mkondo wa amali kutoka wanafunzi 400 mwaka 2024 hadi kufikia 10,000 mwaka 2030;

vi. Kuziunganisha skuli 50 za sekondari na Mkonga wa Taifa ili kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika kufundishia na kujifunzia;

vii. Kujenga karakana tatu katika kila Wilaya ili kuwezesha utoaji wa mafunzo ya amali na ufundi kwa wanafunzi wa Sekondari;

viii. Kujenga dakhalia moja katika kila Wilaya ili kuongeza idadi ya wanafunzi wanaonufaika na huduma hiyo kutoka wanafunzi 6,212 mwaka 2024 hadi kufikia wanafunzi 10,000 mwaka 2030; na

ix. Kuimarisha ufaulu wa wanafunzi wa Kidato cha Nne kutoka asilimia 82.0 mwaka 2024 na kufikia asilimia 90.0 mwaka 2030 na ufaulu wa wanafunzi wa kidato cha sita kutoka asilimia 99.9 mwaka 2024 hadi kufikia asilimia 100 mwaka 2030.

#### 3.4.1.4 Elimu ya Juu

i. Kutanua miundombinu ya Chuo kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) kwa kujenga skuli ya afya na meno, skuli ya kilimo na maabara za sayansi, skuli ya biashara, taasisi ya utalii na dakhalia za wanafunzi wa kike na kiume zenye uwezo wa kuchukuwa wanafunzi 1,100 pamoja na kuendelea na ujenzi wa chuo cha ubaharia;

ii. Kuongeza idadi ya wanafunzi wanaodahiliwa katika Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) kutoka wanafunzi 7,045 mwaka 2024 na kufikia wanafunzi 9,000 mwaka 2030;

iii. Kuimarisha mitaala inayoendana na mahitaji ya soko la ajira kwa kuanzisha programu zinazozingatia na mwelekeo wa kiuchumi wa Taifa ikiwamo uchumi wa buluu;

iv. iv) Kufanya utanuzi wa Taasisi ya Karume ya Sanyansi na Teknolojia kwa kujenga tawi la taasisi hiyo Pemba, dakhalia ya wanafunzi wa kiume, nyumba za wafanyakazi na maktaba;

v. Kutanua chuo cha Tekonolojia cha India (IIT Madrasa) kwa kujenga awamu ya pili ya chuo hicho kwa kujumuisha ujenzi wa majengo ya utawala, madarasa, maabara, nyumba za walimu na migahawa;

vi. Kuimarisha utoaji na usimamizi wa mikopo ya wanafunzi ya elimu ya juu kupitia mifumo ya kieleketroniki; na

vii. Kuongeza idadi ya wanufaika wa mikopo ya elimu ya juu kutoka 8,870 mwaka 2024 na kufikia 20,000 mwaka 2030.

### 3.4.1.5 Elimu Mbadala na Mafunzo ya Amali

i. Kuendelea na ujenzi wa vyuo vinne vya Mafunzo ya Amali pamoja na kuvipatia vifaa vya kufundishia na kujifunzia

ii. Kuanzisha programu mpya 10 za mafunzo ya amali zinazoendana na soko la ajira

iii. Kuimarisha miundombinu ya Mamlaka ya Mafunzo ya Amali kwa kujenga jengo la Ofisi ya Mamlaka hiyo.

iv. Kuongeza asilimia ya watu wazima wanaojua kusoma na kuandika kutoka 92 mwaka 2024 hadi 98 mwaka 2030.

v. Kumairisha mafunzo ya amali kwa kuanzisha taasisi inayohusika na usimamizi wa vyuo vya amali na taasisi inayohusika na udhibiti wa mafunzo ya amali.

### 3.4.1.6 Mitaala na Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia

i. Kusambaza vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa skuli zote na kuhakikisha tatizo la uhaba wa madawati linamalizika;

ii. Kuongeza asilimia ya walimu wanotumia TEHAMA katika kufundisha kutoka asilimia 40.8 hadi asilimia 90;

iii. Kuongeza asilimia ya skuli zenye miundombinu na vifaa rafiki vya kujifunzia kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu kutoka asilimia 13 hadi kufikia asilimia 33; na

iv. Kuanzisha mitaala mipya kwa fani muhimu ambazo hazipo kwa sasa na kuimarisha mitaala iliyopo katika ngazi zote za elimu ili iendane na hali ya sasa.

### 3.4.1.7 Pogramu ya Ubora wa Elimu

i. Kujenga viwanja vya kisasa vya michezo katika skuli zenye michepuo ya michezo pamoja na kujenga vituo viwili vya michezo *(sport academy)* Unguja na Pemba;

ii. Kuimarisha miundombinu ya Baraza la Mitihani la Zanzibar kwa kujenga jengo la ofisi pamoja na kituo cha kuchapisha mitihani;

iii. Kuanzisha mfumo wa tathmini ya kitaifa (National Assessment) na kufanya tathmini hizo katika madarasa ya pili (STD II), tatu (STD III) na Kidato cha Pili;

iv. Kuanzisha huduma za maktaba mtandao pamoja na Hifadhi ya Taifa ya Taarifa;

v. Kuimarisha huduma za maktaba kwa kuendelea na ujenzi wa maktaba ya kuu ya kisasa;

vi. Kuziimarisha maabara 20 za kompyuta kuwa za kisasa pamoja na kuzipatia skuli vifaa vya TEHAMA zikiwamo kompyuta;

vii. Kuanzisha madarasa maizi 22 *(smart class)* ili kuimarisha ujifunzaji na ufundishaji kwa njia ya mtandao;

viii. Kuimarisha utekelezaji wa mtaala wa elimu ya sekondari kwa kuzipatia skuli vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa mkondo wa elimu ya amali na mkondo wa jumla;

ix. Kuimarisha utekelezaji wa mtaala rekebifu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu;

x. Kuimarisha mafunzo ya ualimu kwa kujenga chuo cha kisasa cha mafunzo ya ualimu;

xi. Kuwajengea uwezo walimu kwa kuimarisha mafunzo ya ualimu kazini kupitia vituo vya walimu na mafunzo katika ngazi ya skuli; na

xii. Kuimarisha ukaguzi wa elimu kwa kuongeza idadi ya walimu wanaokaguliwa kwa mwaka kutoka walimu 2,800 mwaka 2024 na kufikia walimu 10,000 mwaka 2030.

#### 3.4.1.8 Programu ya Utawala na Uongozi

i. Kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Elimu Zanzibar (ZDEF), ambao utasaidia kuboresha elimu kwa wote;

ii. Kuajiri walimu wapya 7,691, wakiwemo walimu wa maandalizi 2,466, walimu wa msingi 1,495, na walimu wa sekondari 3,730; na

iii. Kuimarisha ufundishaji katika skuli kwa kuajiri walimu wapya 3,500 katika ngazi ya elimu maandalizi, msingi na sekondari.

### *3.4.2 Afya*

93. CCM inatambua umuhimu wa kuimarisha sekta ya afya kwa lengo la kuboresha ustawi wa jamii na kupunguza vifo vinavyotokana na magonjwa ya kuambukiza na yasiyo ya kuambukiza. Katika kufikia malengo hayo CCM itailekeza ya Mapinduzi Zanzibar Serikali kutekeleza yafuatayo:

#### 3.4.2.1 Uimarishaji wa Miundombinu ya Afya:

i. Kuendeleza ujenzi na ukarabati wa hospitali ya rufaa ya Mnazi Mmoja kuweza kutoa huduma za kibingwa zaidi;

ii. Kujenga hospitali nne za mikoa katika Mkoa wa Kusini Unguja, Kaskazini Unguja, Kusini Pemba na Kaskazini Pemba;

iii. Kuboresha Maabara maalumuu ya Afya ya Jamii (ZPHL) iliyopo Binguni Unguja na Chake chake Pemba ili iweze kuchunguza maradhi mbalimbali ikiwamo ya mlipuko;

iv. Kuboresha uwezo wa udhibiti wa magonjwa ya mripuko kwa kujenga kituo cha usimamizi na udhibiti wa magonjwa ya miripuko kama vile UVIKO-19, Ebola, Homa ya Nyani n.k. katika eneo la Dunga Mkwaju Ngoma kwa Unguja na Mfikiwa kwa Pemba;

v. Kujenga hospitali ya rufaa na kufundishia katika eneo la Binguni Mkoa wa Kusini Unguja;

vi. Kuimarisha upatikanaji wa dawa, vifaa tiba, na vitendanishi;

vii. Kuimarisha mfumo mama wa taarifa za Afya (DHIS2) kwa kujumuisha taarifa za afya kutoka katika mifumo yote ya taarifa za afya iliomo ndani ya Wizara ya Afya;

viii. Kuimarisha miundombinu na upatikanaji wa huduma bora za afya ya msingi ikiwamo ujenzi na ukarabati wa vituo vya afya Zanzibar; na

ix. Kuendeleza na ujenzi wa hospitali maalumu itakayotoa huduma za magonjwa ya akili kisiwani Pemba.

#### 3.4.2.2 Uimarishaji wa Huduma za Afya

i. Kuendelea kushirikiana na sekta binafsi katika kutoa huduma bora za uchunguzi na matibabu kwa wananchi;

ii. Kuongeza wigo wa usajili wa wanufaika wa Mfuko wa Huduma za Afya

iii. Kuongeza utoaji wa huduma za afya ngazi ya jamii kwa kuwatumia wataalamu wa afya katika ngazi ya jamii (Community Health Workers) kwa lengo la kuwafikia wananchi wote wenye uhitaji;

iv. Kuongeza idadi ya wataalamu wa afya wabobezi katika kada yenye upungufu wa wataalamu;

v. Kuanzisha na kutekeleza mpango wa lishe ambao utazingatia utoaji wa elimu ya lishe kwa jamii na mipango ya chakula kwa wanafunzi wa skuli za maandalizi na msingi;

vi. Kuandaa na kutekeleza mkakati wa kitaifa wa kukabiliana na maradhi yasioambukiza;

vii. Kuongeza matumizi ya mifumo na vifaa vya kielekroniki katika utoaji wa huduma za uchunguzi na matibabu ya maradhi mbali mbali;

viii. Kuimarisha uwiano kati ya daktari na wagonjwa kutoka daktari moja kwa wagonjwa 6,272 hadi daktari mmoja kwa wagonjwa 3,100;

ix. Kupunguza idadi ya vifo vya mama wakati wa kujifungua hadi vifo 123 kwa kila wanawake 100,000 kwa mwaka;

x. Kupunguza idadi ya vifo vya watoto wanaofariki kabla na baada ya kuzaliwa hadi vifo 34 kwa kila watoto 1,000 wanaozaliwa hai kwa mwaka;

xi. Kupunguza vifo vya watoto wachanga ndani ya mwezi mmoja wa kwanza baada ya kuzaliwa hadi vifo 26 kwa kila watoto 1,000 wanaozaliwa hai kwa mwaka;

xii. Kuanzisha kituo cha kudhibiti na kusimamia matukio ya sumu katika maeneo ya chakula, kemikali hatarishi na sumu asilia;

xiii. kupunguza vifo vya watoto ndani ya mwaka mmoja hadi kufikia vifo 32 kwa kila watoto 1,000 wanaozaliwa hai; na

xiv. Kuimarisha upatikanaji wa chanjo na huduma za kinga kwa watoto ili kuhakikisha wanakua wakiwa na afya bora.

### *3.4.3 Maji*

#### 3.4.3.1 Maji Safi, Salama na Usafi wa Mazingira

94. CCM imelenga kuhakikisha upatikanaji wa uhakika wa maji safi, na salama. Katika kufikia malengo hayo, CCM itaielekeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutekeleza yafuatayo: -

i. Kuandaa na kutekeleza Mpango Mkakati wa Usimamizi wa Rasilimalimaji ambao pamoja na mambo mengine utazingatia ushirikishwaji wa jamii katika uhifadhi na usimamizi wa vyanzo na miondombinu ya maji;

ii. Kuimarisha miundombinu ya uzalishaji, usambazaji na upatikanaji wa maji safi na salama na kuwafikia asilimia 80 ya wananchi;

iii. Kuendelea kuimarisha Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA);

iv. Kufanya tafiti na kutumia teknolojia za kisasa katika kutafuta vyanzo vipya vya upatikanaji wa maji safi ikiwamo uchimbaji wa maji ya chini ya bahari, uvunaji wa maji ya mvua na matumizi ya teknolojia ya kuondoa chumvi kwenye maji ya bahari;

v. Kuandaa na kutekeleza mpango wa uvunaji wa maji ya mvua kwa matumizi ya sekta ya kilimo;

vi. Kutumia teknolojia ya uvunaji na utumiaji tena wa maji yaliyotumika ili kuhakikisha maji yanapatikana kwa ajili ya shughuli za kiuchumi kwa njia endelevu;

vii. Kuanzisha programu maalumu ya kuwaungia wananchi maji majumbani;

viii. Kuongeza kasi ya ukusanyaji wa mapato ya mauzo ya maji;

ix. Kuhamasisha matumizi ya umeme mbadala katika visima vya maji ili kupunguza gharama ya matumizi ya umeme kwa kuongeza idadi ya visima vya maji vinavyotumia nishati mbadala; na

x. Kuhakikisha upatikanaji endelevu wa maji safi na salama pamoja na mifumo madhubuti na endelevu ya uondoaji wa maji taka mijini na vijijini.

### *3.4.4 Ustawi wa Makundi Maalum*

#### 3.4.4.1 Watu Wenye Ulemavu

95. CCM inatambua kuwa kuwashirikisha na kuwawezesha Watu Wenye Ulemavu ni muhimu kwa kuhakikisha usawa na haki kwa kila mtu katika jamii. Ili kuhakikisha jamii inajumuisha na kuzingatia watu wote bila kujali aina ya ulemavu wao, CCM itaielekeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutekeleza yafuatayo: -

i. Kushajiisha upatikanaji wa ajira zenye staha kwa Watu Wenye Ulemavu;

ii. Kuendelea kutoa vifaa saidizi na mafunzo ya amali kwa Watu Wenye Ulemavu;

iii. Kuongeza uwiano wa Watu Wenye Ulemavu katika nafasi za maamuzi ya umma hadi asilimia 5;

iv. Kuendelea kutoa ruzuku kwa jumuiya za watu wenye ulemavu ili kuwapa fursa ya kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi;

v. Kuimarisha mfumo na usajili wa Watu Wenye Ulemavu ili kuwezesha ufuatiliaji na utoaji wa huduma; na

vi. Kuimarisha ushiriki wa Watu Wenye Ulemavu katika nafasi za maamuzi kutoka asilimia 2 hadi asilimia 5.

#### 3.4.4.2 Wanawake

96. CCM inatambua kuwawezesha wanawake ni muhimu kwa kukuza usawa na haki katika jamii. Ili kufikia malengo hayo, CCM itaielekeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutekeleza yafuatayo: -

i. Kuimarisha mifumo ya uwezeshaji wanawake kiuchumi;

ii. Kuimarisha mifumo ya kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia ikiwamo madawati ya jinsia;

iii. Kuanzisha na kuimarisha mitandao ya wanawake ili kusaidia kubadilishana maarifa na fursa za maendeleo; na

iv. Kuendelea kuimarisha ushiriki wa wanawake katika nafasi za maamuzi katika sekta za umma na binafsi.

#### 3.4.4.3 Watoto

97. CCM inatambua watoto ndiyo Taifa la kesho na ni muhimu kuhakikisha wanalindwa dhidi ya changamoto zote ikiwamo udhalilishaji na kupatiwa malezi bora yatakayowajenga kuwa raia wema wenye uzalendo na upendo kwa nchi yao. Kutokana na umuhimu huo, CCM itaielekeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutekeleza yafuatayo: -

i. Kuimarisha mifumo ya hifadhi ya mtoto na kutoa ulinzi kwa wanaohitaji ulinzi na malezi bora ili kuwa na mustakabali mzuri;

ii. Kuwahamasisha wazazi kuwalea watoto katika misingi bora na kuwaepusha na mazingira hatarishi; na

iii. Kudhibiti ajira na ndoa za utotoni.

### 3.4.5 *Hifadhi ya Jamii*

#### 3.4.5.1 Hifadhi ya Jamii

98. CCM inatambua umuhimu wa hifadhi ya jamii kama sehemu muhimu ya kinga ya kiuchumi na kijamii kwa wananchi wa Zanzibar kwa lengo la kupunguza ugumu wa maisha, kuwainua wananchi kiuchumi kupunguza umasikini, kuleta utulivu na ustawi wa jamii. CCM itailekeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutekeleza yafuatayo: -

    i. Kuimarisha mifumo ya huduma ya hifadhi ya jamii ili iwafikie wananchi wengi zaidi pamoja na kuhamasisha watumishi katika sekta rasmi na isiyo rasmi kujiunga na huduma za hifadhi ya jamii;

    ii. Kulipa mafao kwa wakati na kuboresha huduma kwa wastaafu ikiwamo mifumo ya uhakiki na upatikanaji wa taarifa na malipo ya mafao kwa wastaafu;

    iii. Kuimarisha Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF) ili uweze kuwekeza katika miradi yenye tija kwa lengo la kuongeza uwezo wake wa kifedha na hivyo kuendelea kulipa mafao ya wanachama kwa wakati;

    iv. Kuendelea kutekeleza Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini ili kufikia wananchi wengi zaidi wa kipato cha chini kwa kuwapatia misaada ya kifedha na fursa za kujiongezea kipato kwa njia endelevu;

    v. Kuongeza asilimia ya kaya zenye kupata huduma za hifadhi ya jamii kutoka asilimia 41.7 hadi asilimia 60 kwa mwaka;

    vi. Kuibua na kutekeleza miradi inayolenga kuzalisha ajira, kukuza uchumi wa kaya masikini, na kuendeleza rasilimali watu kwa kuwajengea uwezo na ujuzi unaowawezesha kushiriki kikamilifu katika uchumi wa Taifa;

    vii. Kuimarisha Mfuko wa Huduma ya Afya Zanzibar na kuweka mikakati mahususi ya kuhamasisha wananchi wengi zaidi kujiunga na mfuko wa huduma Afya Zanzibar ili kuweza kufikia malengo ya Afya kwa wote "Univesal Health Coverage";

    viii. Kuimarisha mfumo wa kuwapa wazee vipaumbele katika huduma za kijamii.

    ix. Kuendelea kulipa kwa wakati malipo ya pencheni jamii kwa wazee waliotimiza miaka 70 ambapo wazee hao hulipwa Shilingi Elfu sabini kwa kila mwezi;

    x. Kuendelea kuwalea na kuwatunza watoto yatima na walio katika mazingira magumu kwenye nyumba maalumu za kulelea watoto za Serikali na zisizo za kiserikali; na

    xi. Kuendelea kuwatunza wazee wote wanaoishi katika nyumba za kulelea wazee kwa kuboresha makazi yao na kuwapatia huduma muhimu.

#### 3.4.5.2 Maendeleo ya Jamii

99. Maendeleo ya jamii yanahusisha uwezo wa wananchi mmoja mmoja na katika vikundi vyao kutumia fursa na rasilimali zinazowazunguka ili kuboresha hali zao za maisha. Kwa kutambua mchango wa sekta hiyo katika maendeleo, CCM itaielekeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutekeleza yafuatayo: -

    i. Kuongeza ushirikishwaji wa wananchi katika mipango ya kijamii na kiuchumi kwa asilimia 25 kwa mwaka;

    ii. Kusimamia juhudi za kuwawezesha wananchi kutambua na kutumia fursa zilizopo, pamoja na kuwapatia elimu ya matumizi bora ya rasilimali zilizopo;

iii. Kuongeza ufahamu wa wananchi kuhusu matumizi bora ya rasilimali zao na uwezo wa kujitegemea kiuchumi kwa asilimia 40 kwa mwaka;

iv. Kuimarisha ushiriki wa jamii katika kuibua, kupanga, na kutekeleza mipango ya maendeleo ili kuhakikisha ushirikishwaji wa kila mwanajamii katika maamuzi yanayogusa maendeleo yao; na

v. Kuimarisha mifumo ya utambuzi na kuwafikia walengwa ili kuhakikisha huduma zote zinawafikia wahitaji.

### 3.4.6 *Maendeleo ya Mipango Miji, Nyumba na Makazi*

100. Sekta ya Maendeleo ya Mipango Miji, Nyumba na Makaazi ni nguzo muhimu katika kuboresha maisha ya wananchi. Lengo ni kuimarisha mipango miji, kuimarisha usimamizi wa ardhi, kuwapatia wananchi makaazi rasmi. Ili kufikia malengo hayo CCM itaielekeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutekeleza yafuatato: -

i. Kukamilisha ujenzi wa nyumba mpya za makaazi 4,715 katika maeneo ya Chumbuni, Nyamanzi, Kisakasaka kwa Unguja na Mfikiwa Pemba kwa ajili ya wananchi wa kipato cha chini na kati;

ii. Kuandaa sera maalumu ya makaazi bora yenye kufuata mpangilio na kupendezesha miji ya Unguja na Pemba;

iii. Kukuza ushirikiano baina ya sekta ya Umma na sekta binafsi katika uwekezaji wa makaazi na nyumba za kisasa;

iv. Kuandaa mpango kabambe wa matumizi ya ardhi;

v. Kuendelea kuimarisha makaazi ya majengo yenye umiliki wa pamoja;

vi. Kufanya matengenezo ya nyumba 31 za Shirika la Nyumba zilizopo mji mkongwe; na

vii. Kuongeza asilimia ya watu wanaoishi katika makaazi yaliyofuata mipango miji kutoka asilimia 18 mwaka 2025 kufikia asilimia 40.

### 3.4.7 *Utamaduni Sanaa na Michezo*

101. CCM inatambua na kuthamini umuhimu wa utamaduni, sanaa na michezo katika kuimarisha ustawi na maendeleo ya jamii. Ili kufikia malengo hayo, CCM itaielekeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutekeleza yafuatayo: -

#### 3.4.7.1 Sanaa na Utamaduni

i. Kuendelea kuhifadhi na kuendeleza urithi wa Kiswahili, historia, sanaa na utamaduni wa Mzanzibari ili kuvutia watafiti, wanafunzi na watalii wa kitamaduni kutoka pande zote za dunia;

ii. Kutangaza rasmi Zanzibar kuwa kituo kikuu cha lugha na utamaduni wa Kiswahili duniani, kwa kuvutia watafiti, wanafunzi, na watalii wa kitamaduni;

iii. Kujenga vituo viwili (2) vya utamaduni kwa ajili ya kuendeleza sanaa na urithi wa kitamaduni katika maeneo ya kimkakati Unguja na Pemba, ambapo wageni watajifunza historia na mbinu za mapishi na mavazi ya Mzanzibari, huku wakipata fursa ya kushiriki katika mafunzo ya vitendo;

iv. Kuandaa Matamasha ya Kimataifa ya Utamaduni ikiwamo chakula na mavazi ya Mzanzibari ili kuvutia watalii na kufanikisha utangazaji wa utamaduni wa Mzanzibari;

v. Kuanzisha fani ya sanaa katika vyuo vya elimu ya juu kwa ajili kuwaendeleza vijana katika tasnia ya sanaa;

vi. Kuhamasisha jamii kulinda mila, silka na utamaduni wa Mzanzibari na kushiriki katika michezo ya asili ikiwamo michezo ya ng'ombe na mashindano ya ngalawa;

vii. Kuhamasisha uwekezaji katika tasnia ya Sanaa na filamu kwa kujenga studio za kisasa za filamu na muziki na ukumbi wa kisasa wa shughuli za kijamii (arena);

viii. Kuanzisha na kuratibu mfuko wa maendeleo ya Sanaa na utamaduni utakaowezesha kupatikana kwa mikopo ya masharti nafuu kwa wazalishaji, watengenezaji wa kati na wadogo katika kuharakisha maendeleo ya utamaduni na Sanaa; na

ix. Kuendeleza chuo cha Sanaa kwa lengo la kuibua na kuwaendelea wabunifu wa kazi za Sanaa na kuwapatia mikopo. .

### 3.4.7.2 Michezo

i. Kujenga na kukarabati miundombinu ya michezo na burudani ikiwamo viwanja, vituo vya michezo, na vituo vya utamaduni vinavyokidhi hadhi ya kitaifa na kimataifa kwa kila Wilaya;

ii. Kufundisha wataalamu wa michezo watakaoweza kutambua, kukuza na kuendeleza vipaji vya michezo;

iii. Kuanzisha skuli za akademia za michezo mbili (2) kwa lengo la kukuza na kuendeleza vipaji vya michezo;

iv. Kuanzisha chuo cha michezo ili kutoa mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa viongozi wa michezo na wanamichezo ili kufikia viwango vya kitaifa na kimataifa;

v. Kuvijengea uwezo vyama vya michezo ili viweze kujiendesha kwa ufanisi;

vi. Kufanya mapitio ya sera ya michezo ili kuweka mageuzi ya kuibua njia ya kukuza michezo nchini itakayoweza kuwainua vijana na kuonesha vipaji walivyo navyo kwa kuonekana ndani na nje ya nchi;

vii. Kuimarisha utendaji wa Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar (BTMZ) ili kurahisisha usimamizi na uendelezaji wa shughuli za michezo hasa kwa vijana kupitia usajili wa vyama na vilabu vya michezo;

viii. Kuhamasisha uanzishwaji wa utalii wa kimichezo (sports tourism) ikiwamo michezo ya ufukweni;

ix. Kukamilisha kiwanja kimoja cha michezo kwa kila Mkoa na Wilaya;

x. Kuandaa na kufanikisha matukio kumi (10) ya kimataifa ya michezo na utamaduni, ili kuvutia wageni na kukuza chapa ya utalii wa Zanzibar kupitia michezo na utamaduni;

xi. Kuongeza ushiriki wa wanamichezo wa Zanzibar katika mashindano ya Kikanda na kimataifa; na

xii. Kukamilisha maandalizi ya nchi kuwa mwenyeji wa mashindano ya mpira wa miguu Barani Afrika (AFCON-2027) kwa kujenga na kuimarisha miundombinu ya michezo, kuhamasisha na kuboresha miundombinu wezeshi, ikiwamo malazi na usafiri.

## 3.5 Kuimarisha Miundombinu ya Usafiri na Usafirishaji

### *3.5.1 Miundombinu na Usafirishaji*

102. CCM imeweka kipaumbele katika kuimarisha miundombinu ya barabara na usafiri wa anga kwa lengo la kuchochea ukuaji wa uchumi, kuimarisha huduma na kuchochea uwekezaji wenye tija. Ili kufikia azma hiyo, Chama kitaielekeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutekeleza yafuatayo: -

#### 3.5.1.1 Usafiri wa Anga na Viwanja vya Ndege

i. Kuongeza idadi ya abiria wanaotumia viwanja vya ndege vya Unguja na Pemba kwa mwaka kutoka abiria 2,140,986 kufikia abiria 2,824,011 na hivyo kuongeza ajira na kipato;

ii. Kujenga karakana ya kufanyia matengenezo ya ndege za nje na ndani (aircraft maintenance hungar) zinazotoa huduma katika viwanja vya ndege vya Unguja na Pemba;

iii. Kujenga mnara mpya wa kuongozea ndege katika uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume;

iv. Kujenga kituo cha biashara katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Aman Karume utakaojumuisha jengo la ghorofa tatu (3) la ofisi, mikahawa, taasisi za fedha na maduka;

v. Kuendelea na ujenzi wa vituo viwili vya mafuta ya ndege (Jet A1) katika uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume na kufikia idadi ya vituo vinne (4) vya kutoa huduma ya mafuta katika uwanja huo ili kukuza ushindani na ufanisi wa utoaji wa huduma hiyo;

vi. Kukamilisha ujenzi wa kituo cha kuhifadhia mizigo (logistic center) katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume kwa lengo la kuwa na huduma bora za kuhifadhia na usafirishaji bidhaa kikanda na kimataifa;

vii. Kujenga maegesho mapya yatakayowezesha kuweka ndege nane (4) kubwa kwa wakati mmoja aina Code C na Code E katika Uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume;

viii. Kufanya ukarabati na utanuzi wa jengo la kwanza la abiria (Terminal 1) katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Aman Karume kwa ajili ya matumizi ya viongozi wakuu wa kitaifa, viongozi mashuhuri wa Serikali (VIP), abiria wa kibiashara (CIP) na ndege binafsi (Private Jet Operations)

ix. Kukarabati na kuongeza eneo la maegesho ya ndege kwa mita za mraba 106,000;

x. Kuongeza idadi ya safari za ndege zinazoingia na kutoka nje kwa mwaka na kufikia 125,056 kwa mwaka;

xi. Kuanza kwa ujenzi wa jengo jipya la abiria namba 4 katika uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume;

xii. Kuendeleza ujenzi wa kiwanja cha ndege cha Pemba ikiwamo kuongeza urefu wa njia ya kurukia ndege (runway) kufikia mita 2,500 pamoja na ujenzi wa jengo jipya la abiria;

xiii. Kuendeleza ujenzi wa uwanja wa ndege wa Nungwi;

xiv. Kujenga uwanja wa ndege wa Paje utakaohudumia ndege ndogo zenye uwezo wa kuchukua abiria 70; na

xv. Kuanzisha miundombinu na mifumo ya kukabiliana na hali ya dharura ya ajali za ndege (Aircraft Accident Recovery (AAR).

### 3.5.1.2 Usafiri wa Ardhini na Miundombinu ya Barabara

i. Kujenga barabara ya Tunguu – Makunduchi (km 48), Fumba – Kisauni (km 12), barabara ya Mkoani – Chake (km 43.5) na Barabara ya Utalii Nungwi kilomita 12; Pamoja na kuweka taa za barabarani katika maeneo yote hayo ikiwamo na barabara za ndani;

ii. Kuweka taa za kuongozea gari kwenye makutano kumi ya barabara (Mpendae, Mkunazini, Malindi, Kinazini BOT, Mikunguni kwa Pweza, Mtoni na Saateni kwa Unguja. Machomane, Chanjaani (njia ya uwanja wa ndege) na Melitano kwa Pemba;

iii. Kujenga barabara lishe (feeder roads) zenye urefu wa kilomita 246; pamoja na kilomita 277.7 ya muendelezo wa ujenzi wa barabara za Unguja na Pemba;

iv. Kuendelea kujenga barabara za mijini zenye urefu wa kilomita 100.9; vijijini kilomita 275 barabara mpya za mijini kilomita 333.7

v. Kupanua barabara kuu za njia moja hadi njia mbili, kujenga barabara mpya, madaraja, na viwanja vya maegesho ili kupunguza msongamano na kuongeza ufanisi wa barabara;

vi. Kujenga barabara kuu zenye urefu wa kilomita 523.7 Unguja na Pemba;

vii. Kujenga Daraja litakalopita baharini la kuunganisha kijiji cha Chwaka na Charawe ili kuunganisha miundombinu ya barabara kutoka mkoa wa Kaskazini na Kusini Unguja;

viii. Kujenga njia za juu (flyover) na interchanger katika mji wa Zanzibar ili kuondoa msongamano wa magari na kurahisisha usafiri wa abiria na mizigo;

ix. Kufanya utafiti wa kuona uwezekano wa kujenga daraja la kuunganisha Mkokotoni na kisiwa cha Tumbatu;

x. Kujenga mfumo wa usafiri wa haraka wa mabasi, reli pamoja na kuboresha njia za daladala ili kuhakikisha huduma za usafiri wa umma zinawafikia wananchi wengi kwa haraka na ufanisi;

xi. Kuweka kamera (CCTV) maeneo ya barabara kwa ajili ya kuimarisha usalama; na

xii. Kuandaa Mkakati wa elimu ya usalama barabarani na kusimamia utekelezaji wa sheria kwa lengo la kupunguza ajali za barabarani.

SURA

# 04.

# *Ufuatiliaji* na *Tathmini* ya Utekelezaji wa *Ilani*.

103. Ili kutekeleza Ilani ya CCM kwa ufanisi, Kamati Kuu ya CCM itaweka mfumo imara wa kusimamia utekelezaji kuanzia katika ngazi ya tawi. Mfumo wa usimamizi utazingatia malengo mahususi ya Ilani na viashiria thabiti vya upimaji. Mfumo wa usimamizi wa Ilani utaanzia katika ngazi ya tawi na Kamati za Siasa za kila ngazi zitaratibu taarifa za utekelezaji kwa ngazi husika.

104. Mapema iwezekanavyo, na kwa vyovyote vile angalau mwezi mmoja kabla ya tarehe ya uchaguzi mkuu, Sekretariati ya Chama Makao Makuu itaandaa mpango kazi wa kutekeleza Ilani utakaoainisha malengo, malengo mahususi, viashiria vya upimaji na shabaha kwa kila kipaumbele cha Ilani. Aidha, Sekretariati itaandaa makadirio ya bajeti inayohitajika katika kutekeleza Ilani katika kipindi cha miaka mitano.

105. Kamati za Siasa za Matawi zitaandaa taarifa za utekelezaji wa Ilani kwa ngazi za Serikali za Mitaa na Vijiji. Kamati za Siasa za Kata/Wadi zitasimamia na kuandaa taarifa za utekelezaji wa Ilani katika ngazi ya Kata/Wadi. Kamati za Siasa za Wilaya zitasimamia na kuandaa taarifa za utekelezaji wa Ilani katika ngazi ya Wilaya na kushirikisha majimbo yote yaliyopo katika wilaya husika.

106. Taarifa za utekelezaji wa Ilani zitaandaliwa na kutolewa angalau mara mbili kila mwaka kwa kuzingatia viashiria vya upimaji vitakavyowekwa.

107. Kufikiwa kwa shabaha zilizowekwa katika mpango kazi ndicho kitakuwa kipimo kikuu cha utendaji wa viongozi wa Serikali na CCM katika ngazi husika. Viongozi na watendaji wa Serikali za CCM, yaani Wenyeviti na Watendaji wa Vijiji/Mitaa, Madiwani na Maafisa Watendaji wa Kata, Wabunge/Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, Makatibu Tawala wa Wilaya, Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi wa Halmashauri, Wakuu wa Taasisi za Umma, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakuu wa Mikoa, Makatibu Wakuu na Mawaziri watapimwa ufanisi wao kwa kuzingatia viashiria mahususi vya utendaji katika maeneo yao ya utendaji.

108. CCM itahakikisha inapiga vita vitendo vyote vinavyoweza kukwamisha utekelezaji wa malengo yaliyowekwa, ikiwamo rushwa, uzembe na umangimeza. CCM itahakikisha kuwa Serikali inaweka uongozi wenye dhamira thabiti, uwajibikaji, weledi, na umakini katika ngazi zote, katika Serikali Kuu na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Mkazo utawekwa katika kupata matokeo ya haraka badala ya kutumia muda mwingi katika kushughulikia michakato. CCM haitavumilia ucheleweshaji wa utekelezaji wa programu na miradi ya maendeleo iliyopangwa. Nidhamu ya utekelezaji, weledi na uwajibikaji zitakuwa nguzo muhimu katika utekelezaji wa Ilani hii.

109. Ili kupata matokeo ya uhakika, na kufanya uamuzi sahihi, utekelezaji wa Ilani utazingatia taarifa za kitafiti na matumzi ya sayansi na teknolojia.

110. Kwa kuzingatia uchache wa rasilimali na malengo ya Ilani ya CCM (2025-2030), uchaguzi wa sekta za kipaumbele utazingatia uwezo wa sekta katika kuleta mabadiliko makubwa na ya haraka ya kijamii na kiuchumi. Vigezo vya uchaguzi wa sekta hizi utazingatia uwezo wa sekta husika katika kukuza uwezo wa nchi kuuza bidhaa nje, kufungamanisha sekta, uzalishaji wa mapato, na uongezaji thamani ili kuongeza tija kiuchumi.

111. Kwa kuzingatia nafasi ya wananchi katika kuleta maendeleo, utekelezaji wa Ilani ya CCM utakuwa shirikishi ukihusisha wadau mbalimbali na wananchi kwa ujumla. Ubia kati ya sekta ya umma na binafsi utapewa msukumo wa pekee.

112. Utekelezaji wa Ilani utazingatia kikamilifu misingi mama ya CCM, ambayo ni utu, umoja, haki, na usawa. Aidha, CCM itahakikisha kuwa utekelezaji wa Ilani unazingatia kikamilifu misingi ya demokrasia na utawala wa sheria. Hakuna kiongozi atakayevumiliwa kwa kuvunja sheria kwa kisingizio chochote kile. Vilevile, utekelezaji wa Ilani utazingatia misingi ya falsafa ya R4 yaani Reconciliation (Maridhiano), Resiliency (Ustahimilivu), Reform (Mabadiliko) na Rebuilding (Kujenga upya) ili kuimarisha utawala bora, demokrasia na uchumi kwa kufungua milango ya mazungumzo na wadau wa kisiasa, kijamii na kiuchumi ikiwa ni pamoja na vyama vya siasa, asasi za kiraia na sekta binafsi.











*Dira ya CCM ni kuona Tanzania yenye ustawi kwa wote, nchi inayozingatia na kuheshimu utu, haki na usawa, na Taifa imara linalojitegemea.*

SURA

# 05.

# *Ubora, Uwezo* na *Uzoefu* wa CCM Katika Kutoa *Uongozi* wa Nchi.

113. Tangu kuanzishwa kwake hadi sasa, CCM imeendelea kuaminiwa na wananchi na kupewa ridhaa ya kuunda na kuongoza Serikali zote mbili; Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mafanikio makubwa na kuleta maendeleo ya kujivunia kwa wananchi.

114. Mafanikio na uimara wa Serikali za CCM yanategemea uimara wa Chama Cha Mapinduzi. Hivyo basi, katika kipindi cha utekelezaji wa Ilani hii, CCM itaendelea kujiimarisha kiitikadi, kiuchumi, na kiprogramu ili kuendelea kuwa daraja kati ya wananchi na serikali zao.

115. Katika kuendelea kutekeleza malengo na madhumuni ya kuanzishwa kwake, kama yalivyoainishwa katika Ibara ya 5 (1) – (19) ya Katiba ya CCM, katika kipindi cha miaka mitano ya utekelezaji wa Ilani hii (2025 – 2030), CCM itaendelea kusimamia na kutekeleza malengo makuu yafuatayo: -

    i. Kuendelea kujiimarisha kimuundo, kiuongozi na kiutendaji, ili kuendelea kuaminiwa na wananchi na kupewa ridhaa ya kuongoza Serikali Kuu na Serikali za Mitaa, katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa upande mmoja na Zanzibar kwa upande wa pili.

    ii. Kuendelea kusimamia Siasa ya Chama ya Ujamaa na Kujitegemea, kuimarisha mifumo ya Demokrasia ndani ya Chama na kusimamia misingi ya haki, usawa na uwazi kwa kuzingatia na kufuata Katiba, Kanuni na Taratibu za CCM.

    iii. Kuendelea kuwa chombo madhubuti kinachowaunganisha wananchi, hasa wanyonge na kuwaongoza katika mapambano dhidi ya adui ujinga, maradhi na umasikini na kuwa daraja madhubuti na imara la kuwaunganisha na Serikali zao, kulinda na kuimarisha Muungano na Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ya tarehe 12 Januari, 1964 kwa kusimamia bila kuyumba Sera ya Serikali mbili; Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

116. Aidha, ili kuendelea kutekeleza jukumu lake la kutoa uongozi bora na kwa kutambua kwamba, ***"kuongoza ni kuonesha njia"***, katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2025 – 2030), CCM itatekeleza na kusimamia malengo mahsusi yafuatayo: -

**a. *Kuimarisha uhai, nguvu na maendeleo ya Chama na Jumuiya zake*** (UWT, UVCCM na WAZAZI), kwa kutumia maarifa ya kisasa (TEHAMA) na kuweka malengo yanayopimika kwa kutekekeleza yafuatayo; -

    i. Kuongeza idadi ya wanachama wa CCM na jumuiya zake kwa kiwango kisichopungua asilimia 5 kila mwaka;

    ii. Kuongeza kiwango cha ulipaji wa ada za uanachama katika kila Mkoa na Wilaya, kutoka asilimia 11.1, hadi asilimia 75;

    iii. Kuongeza idadi ya matawi yenye ofisi za kudumu katika ngazi ya Mkoa kutoka wastani wa asilimia 58 na kufikia wastani wa asilimia 70;

iv. Kuhakikisha kuwa, idadi ya vikao vya kikatiba na kikanuni vinavyoitishwa katika ngazi ya tawi, kata/wadi na jimbo (Zanzibar), inaongezeka kutoka asilimia 30 hadi kufikia asilimia 60; na

v. Kuanzisha na kukamilisha ujenzi wa jengo la Ofisi za Makao Makuu, Dodoma na kuhakikisha kuwa, mikoa na wilaya inaongeza kasi ya ujenzi wa ofisi za kudumu, hususan katika ngazi ya wilaya, jimbo (Zanzibar), kata/wadi na matawi pamoja na nyumba za kuishi watendaji wa CCM na jumuiya zake (UWT, UVCCM na WAZAZI), ili kuwapunguzia gharama za maisha.

b. ***Kusimamia kwa vitendo dhana ya "Siasa ni Uchumi na Uchumi ni Siasa" na utekelezaji wa Sera ya CCM ya Miradi na Uwekezaji***, Toleo la 2021 kwa kutumia rasilimali za Chama, hususan ardhi kwa kutekeleza yafuatayo: -

i. Kuhakikisha kuwa, rasilimali za Chama, zinatumiwa kwa ufanisi mkubwa na thamani yake inaongezeka kutoka wastani wa asilimia 8, hadi wastani wa asilimia 10;

ii. Kuhakikisha kuwa, kiwango cha mapato ya Chama na Jumuiya zake kinachokusanywa, kinaongezeka kutoka wastani wa asilimia 88 na kufikia wastani wa asilimia 92. Aidha, Chama na Jumuiya zake (UWT, UVCCM na WAZAZI) kinabuni na kuanzisha vyanzo vipya vya mapato, ikiwamo miradi ya uwekezaji wa hatifungani;

iii. Idadi ya mikoa inayojitegemea kimapato, inaongezeka kutoka tisa, hadi kufikia 18 na kuhakikisha kuwa, kila mkoa pamoja na wilaya zake, unatumia mifumo ya TEHAMA katika ulinzi, usimamizi na uendelezaji wa mali za chama na jumuiya zake;

iv. Idadi ya viwanja, mashamba na majengo ya Chama na Jumuiya zake, yaliyosajiliwa na kupatiwa Hati (za kawaida na kimila), inaongezeka kutoka asilimia 14 hadi kufikia asilima 50; na

v. Kubuni na kutekeleza Mpango wa kukuza mapato ya Chama na Jumuiya zake (UWT, UVCCM na WAZAZI), kwa kutumia rasilimali zisizotumika, hususan ardhi vikiwamo baadhi ya viwanja vya mpira na maeneo ya sabasaba;

vi. Kuendeleza na kukuza ushirikiano na vyama vingine vya siasa nchini, vyama vya kidugu na vyama vya kirafiki duniani, kwa lengo la kuimarisha na kuendeleza umoja, amani na maridhiano ya Kitaifa kwa kuzingatia falsafa ya Maridhiano, Ustahimilivu, Mageuzi na Kujenga Upya; na

vii. Kuendeleza na kuimarisha mapambano dhidi ya rushwa ndani ya Chama, hususan wakati wa chaguzi za ndani ya Chama na Jumuiya zake pamoja na chaguzi za Vyombo vya Dola.

c. ***Kuandaa na Kutekeleza Programu mbalimbali za mafunzo kwa Viongozi, Watendaji na Makada wa Chama,*** chini ya usimamizi wa Idara ya Itikadi, Uenezi na Mafunzo kwa kushirikiana na Jumuiya zote za CCM (UWT, UVCCM na WAZAZI). Aidha, Chama kitaendelea kutoa mafunzo juu ya siasa, Itikadi na Sera zake kwa viongozi, watendaji na wanachama wake (Makada) kupitia madarasa ya Itikadi yatakayoanzishwa katika mikoa, wilaya, jimbo (Zanzibar), kata/wadi na matawi. Mafunzo hayo yataratibiwa na kusimamiwa na Makatibu wa Siasa na Uenezi wa ngazi husika.

d. ***Kufuatilia Utekelezaji wa Ilani ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 unaofanywa na Serikali kwa kuzingatia utaratibu ufuatao: -***

   i. Katika ngazi ya Taifa, usimamizi wa utekelezaji wa Ilani ya CCM, utafanywa na Wabunge pamoja na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, kupitia Kamati zao za kudumu. Aidha, Mwenyekiti wa Kamati ya Wabunge wote wa CCM (Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania) na Mwenyekiti wa Kamati ya Wawakilishi wote wa CCM (Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar) wanao wajibu wa kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa Ilani, mbele ya vikao vya Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa;

   ii. Vikao vya Halmashauri Kuu za CCM vya ngazi ya mkoa, wilaya, majimbo, kata/wadi na matawi, vinapaswa kusimamia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi katika maeneo yao, kupitia taarifa kutoka kwa Wabunge, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na Madiwani wao;

   iii. Njia nyingine ya kufuatilia utelekezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ni kwa viongozi wa CCM kutembelea na kukagua miradi inayotekelezwa na Serikali katika maeneo yao ya uongozi. Hivyo, viongozi wa CCM wa ngazi zote, watajiwekea ratiba za kutembelea na kukagua miradi inayotekelezwa katika maeneo yao, na iwapo watabaini dosari au hitilafu zozote, watatoa taarifa kwa viongozi wa Serikali wa ngazi ya juu yao mara moja; na

117. Chama kitatenga siku maalumu kila mwezi, ili kusikiliza kero za wananchi na kuzifikisha serikalini, kwa ajili ya kupatiwa ufumbuzi.

# CCM inaahidi kuendelea kuboresha uchumi, kuimarisha ustawi wa wananchi



KAZI NA UTU, TUNASONGA MBELE